# Nipashe

Alhamisi Septemba 26, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580033

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

…om/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## DC aagiza Tanesco kukata umeme ofisi ya Mkurugenzi

UKURASA 2


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Watafiti wa sayansi walipowaingiza wadau wao darasa la wadudu, udongo

Mporomoko maadili unageuza uzazi sehemu moja hadi nyingine

Wanasaikolojia waja na majibu ya vitambi

Tembo mharibifu anafuatiliwa na 'CCTV' inayorusha taarifa akitaka kuvuka mpaka

UKURASA 13

# RC Makonda sasa awatangazia vita ma-DC, watendaji



• **Ni** baada ya JPM kutoridhishwa utendaji wake, adai wanamhujumu, atawachongea kwa wakubwa...*Uk.2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MOTO COCO BEACH WATIA HASARA BIL. 1/-**

MMILIKI wa maeneo ya biashara katika ufukwe wa Coco, Alphonce...

UKURASA WA 3

**TCU YAONGEZA MUDA UDAHILI**

TUME ya Vyuo Vikuu (TCU) imetangaza kuongeza muda wa udahili kwa siku nne kuanzia...

UKURASA WA 4

**AHUENI UDHIBITI WA BIDHAA ZA NJE**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ya awamu ya tano itaendelea...




Askofu Mkuu Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, akifanya maombi na madaktari wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuruhusiwa. Kushoto ni Askofu Msaidizi wa Jimbo hilo, Eusebius Nzigilwa, Mkurugenzi Mtendaji MOI, Dk. Respicious Bonface na kulia ni Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu, Prof. Joseph Kahamba. **PICHA: MARY GEOFREY. HABARI KAMILI UK.2**

## Wamiminika kwa DPP kutafuta msamaha

UKURASA 3



## Vigogo Chadema wagonga mwamba

UKURASA 4


**MICHEZO** MAXIME: SIMBA HII NI ZAIDI YA STARS UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Makonda adai kuhujumiwa na watendaji

**Na Mary Geofrey**

SIKU chache baada ya Rais John Magufuli kumshukia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuwa haridhishwi na utendaji wake, kiongozi huyo wa mkoa amekutana na viongozi na watendaji wote walio chini yake huku akieleza wanavyomhujumu.

Jumapili iliyopita, wakati wa kuwaapisha viongozi aliowateua, akiwamo Mkuu wa Morogoro, Rais Magufuli alionyeshwa kusikitishwa na kusuasua kwa miradi ya maendeleo ilhali mkuu huyo wa mkoa yupo.

Kutokana na madai hayo ya kuhujumiwa, Makonda ametangaza kuwa atawachongea watendaji hao kwenye ngazi za juu za utawala.

Pia amelalamika kuwa amekuwa akitoa maagizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo lakini badala ya kutekeleza, baadhi ya watendaji hao wamekuwa wakitafuta uhakika kutoka kwa wakuu wa idara.

Makonda aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na wakuu wa wilaya zote tano za mkoa wa Dar es Salaam, wakurugenzi wa manispaa, viongozi wa jiji na watendaji wote katika kikao cha kujadili sababu za kukwama kwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Haina maana kama mimi natoa maagizo na nyie viongozi badala ya kuyafuata mnaanza kupitisha vimemo kuuliza kama mtafanyaje ili kutafuta uhakika, ina maana mkuu wa mkoa hana washauri wazuri ndio sababu ya kutofuata maelekezo yake," alisema Makonda.

Alimtaja Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Happi, ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kuwa alikuwa akifuata maelekezo yake bila vikwazo tofauti na viongozi wengine walio chini yake, akiwamo anayeshika nafasi hiyo kwa sasa. Kwa sasa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ni Daniel Chongolo.

"Nilikuwa nikifanya vikao ofisini kwangu na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Ally Hapi na wa Ilala Sophia Mjema. Walikuwa wakifuata ninachowaeleza lakini hawa wengine kila nikiwaambia lazima waanze kupita pita na kuuliza hapa sijamwelewa. Mnapiga majungu yenu, sasa inatosha na mimi nitaanza kuwashughulikia," Makonda alisema.

Alisema viongozi na watendaji wa mkoa huo, wanapaswa kufuata maagizo yake kwa sababu ndiye aliyepewa jukumu la kusimamia mkoa huo.

"Haijalishi kama umenipita umri au nilikukuta serikalini lakini uko chini yangu tu," alisema Makonda na kuongeza kuwa ili kumaliza utata na fitina hizo, naye atakuwa akitoa taarifa za viongozi wasiotimiza wajibu wao kwa viongozi wa juu yake.

Alisema pia kila maagizo atakayokuwa akiwapatia, atakuwa akituma nakala kwa uongozi wa juu ili kuondokana na changamoto ya kuonekana mzembe ilhali anatimiza wajibu wake.

"Tangu nimekuwa mkuu wa mkoa huu, sijawahi kuandika barua kwa viongozi wa juu kumsema kiongozi yeyote, awe mkuu wa wilaya au wakuu wa idara. Lakini sasa nitaanza kuwasema. Nimeshamwambia Katibu Tawala wa Mkoa kila ninapotoa maagizo atoe na nakala kwenda kwa viongozi wa juu," alisema Makonda.

Aidha, aliwataja viongozi wa wilaya ya Kinondoni ambao mradi wa fukwe za Coco umekwama na anapowapa maagizo hawayafuati na kusababisha mkoa kupata sifa mbaya za kukwama kwa miradi.

"Natoa ushauri nyie mnafuata wa kwenu. Nikiuliza mnaitisha vyombo vya habari kusema mnafuata sheria. Mnapindua maagizo yangu na kufuata yenu. Tusishindane, tunapozidiana madaraka kila mtu atimize wajibu

INAENDELEA UK.8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa Nelson Venance Mabeyo, ambaye ni mtoto wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, nyumbani kwa baba yake, Msasani jijini Dare s Salaam jana. Nelson alifariki kwa ajali ya ndege. **PICHA: OMR**

# DC aagiza ofisi ya DED kukatiwa umeme

**Na Gidion Msabula**

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ameagiza kukatwa umeme Ofisi ya Halmashauri ya wilaya hiyo, baada ya kushindwa kulipa bili ya umeme katika Soko Kuu la Hai.

Ofisi hiyo ya halmashauri ndipo ilipo pia ofisi ya Mkuu wa Wilaya huyo. Alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea soko hilo akimtaka Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) kurejesha huduma ya umeme sokoni hapo iliyoondolewa na shirika hilo kutokana na halmashauri kutolipa bili.

"DED (Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya) na watu wako mnakuja kukusanya fedha kwa miezi mitatu mfululizo, mnasahauje kulipa bili kupitia fedha hizo?

"Hili nalo Rais asimamishwe aambiwe? Mimi na wewe tuwaombe radhi hawa wananchi, ila wakati huo nakuagiza Meneja wa Tanesco ukate umeme Ofisi ya Mkurugenzi na uwashe hapa sokoni na alipe deni hilo, na alipe bila za miezi sita ijayo.

"Umeme uwake hapa leo (jana) na 'go ahead' (maelekezo) ya kuwasha umeme kwa DED nitakupa baada ya kuona risiti. Na kwa kuwa ofisi yangu iko kwenye jengo hilo (la DED) tukapambane wote na hilo joto la kuwapuuza hawa wananchi tunaoambiwa kila siku kuwasikiliza na kuwahudumia."

Hata hivyo, Ole Sabaya alimweleza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Yohane Sintoo, kuwa hayuko tayari kufanya kazi kwenye ofisi ambayo haina huduma ya umeme na hayuko tayari kuona wananchi wanatozwa kodi ambayo hairudi kulipa deni la umeme. Kutokana na agizo hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo (Sintoo) alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kuwaomba radhi wananchi kutokana na kukatwa kwa umeme kwenye soko hilo.

"Ni kweli mkuu tulipaswa kuwa tumelipa deni la Sh. 262,000 na nawaomba radhi wananchi. Ofisa Biashara na watendaji wengine wanaohusika, ninapopokea maelekezo haya kwa Mheshimiwa 'DC' (Mkuu wa Wilaya) nanyi mjiandae kubeba uwajibikaji wenu," alisema.

# Askofu Ruwa'ichi atoka hospitali

**Na Mary Geofrey**

WIKI mbili tangu, Askofu Mkuu wa Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, kufanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo, jana aliruhusiwa kutoka hospitali.

Askofu Ruwa'ichi, alipokelewa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) Septemba 9, mwaka huu, akitokea katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC na kufanyiwa upasuji huo, uliochukua saa nne chini ya madaktari bingwa wanne.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, baada ya kuruhusiwa, Askofu Ruwa'ichi, aliishukuru MOI kwa matibabu waliyompatia wakati wote akiugua.

Pia alimshukuru Rais John Magufuli kwa msaada aliompatiwa wa ndege ya kuwahishwa kupatiwa matibabu MOI.

"Kipekee nimshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa ndege ya Rais iniwahishe kuja kupata huduma hapa MOI, naona sifa hii sikustahili. Mungu aendelee kumbariki, aibariki kazi yake iendelee kuwa njema kwa ustawi wa taifa letu," alisema.

Alisema matamanio yake ni kuona huduma aliyopatiwa wanapatiwa Watanzania wote.

Askofu Ruwa'ichi ambaye alikuwa amevalia vazi la kanisa, pia alipata fursa ya kutoa baraka kwa madaktari na watumishi wote wa MOI walioshiriki katika mkutano huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema wamemruhusu Askofu Ruwa'ichi baada ya afya yake kuimarika.

Alisema walifanya kazi yao kikamilifu, lakini wanaamini Mungu ndiye anatenda, na kwamba anaamini hivi karibuni atarejea katika majukumu yake ya kila siku.

"Tukimaliza hapa anaruhusiwa. Tuaamini Mungu katenda maana sisi tunafanya kazi, lakini yeye ndiye mtendaji. Tunawashukuru pia kwa kutuamini mngeweza kwenda popote kuhudumiwa, lakini mmekuja MOI na kuitangaza hospitali yetu," Dk. Boniface alisema.

Naye Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu, Prof. Joseph Kahamba, alisema hali ya Askofu Ruw'aichi imeimarika, baada ya kupatiwa

INAENDELEA UK.8



Mkurugenzi wa Kavazi la Mwalimu Nyerere, Prof. Issa Shivji (kushoto), akifafanua jambo kwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwl. Nyerere, Joseph Butiku (wa pili kulia), Prof. Sylvia Tamale wa Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda (kulia) na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Chriss Maina, wakati wa mhadhara wa sita wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wamiminika kwa DPP kutafuta msamaha

**Salome Kitomari na Romana Mallya**

ZIKIWA zimebaki siku mbili tangu Rais John Magufuli amuagize Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, kuwasikiliza watuhumiwa wa uhujumu uchumi ili ikiwezekana wasamehewe, mwenyewe amesema waombaji wajitokeza.

Naye, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, amesema uchambuzi wa kina utafanyika kwa kila kosa kwa kushirikiana na mamlaka nyingine.

Akizungumza na Nipashe jana DPP Mganga alisema tangu yatolewe maagizo hayo waombaji wamekuwa wakiendelea kuomba.

"Wapo waliojitokeza kuomba, idadi ya walioomba siwezi kukutajia, ila jua wapo," alisema.

Baada ya maagizo ya Rais Magufuli siku iliyofuata, Mganga alieleza utaratibu ambao watuhumiwa wa uhujumu uchumi wanatakiwa.

Alisema utaratibu ni kwamba mtuhumiwa mwenyewe aliyeko mahabusu anatakiwa aandike barua kupitia kwa mkuu wa gereza akikiri kosa na kuomba kutubu haraka iwezekanavyo na wao watachukua hatua.

"Jambo hili linatakiwa kufanywa na mtuhumiwa mwenyewe aliyeko gerezani na siyo wakili kwani kukiri kosa na kuomba toba ni jambo zito linalohitaji utashi binafsi na siyo kuwakilishwa," alisema Mganga.

"Ni mtuhumiwa mwenyewe ndiye anayetakiwa kuandika barua siyo wakili, unajua wakili anaweza kubadilika na hata mtuhumiwa kumkana kuwa sijamtuma afanye alichokifanya kwa niaba yangu," alisema na kuongeza:

"Ndiyo maana mara zote watuhumiwa wanaomba msamaha na kukiri kuandika barua wenyewe kwa mkono wao kupitia kwa mkuu wa gereza."

Waziri Mahiga akihojiwa na kituo kimoja cha luninga, alisema:

"Makosa haya makubwa yalikuwapo na yametungiwa na sheria na lazima yashughulikiwe kama makosa makubwa na hayana dhamana. Bungeni tumepitisha utaratibu wa kisheria wa mhalifu kuzungumza na Mahakama na DPP yakatazamwa na kama wako tayari kukiri wanaweza kusamehewa."

Aidha, Waziri alisema katika kipindi cha siku saba kilichotolewa watu wengi ambao wana makosa hayo wamepeleka maombi ili yasikilizwe na yachambuliwe.

"DPP kwa sasa yupo kazini na wasaidizi wake anatazama maombi moja baada ya jingine ili aone na kupima lipi lisamehewe na akadirie kiasi gani kilipwe," alisema Waziri Mahiga.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, DPP alimueleza kuwa maombi yanaingia kwa kasi, na kwamba lazima uchambuzi wa kina ufanyike.

"Si suala la kutazama kesi moja, lazima kutazama mafaili, chimbuko lake, kushirikiana na idara za upelelezi ili kukamilisha," alisema.

Jumapili, Rais Magufuli wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali wa serikali aliowateua Ijumaa, alisema watuhumiwa hao kama wako tayari kuomba msamaha, kukiri makosa yao pamoja na kurudisha fedha walizotakatisha, wasikilizwe na hata kusamehewa.

Rais Magufuli alimwagiza DPP kwenda kuwasikiliza watu hao kwa siku saba hadi Jumamosi.

# TCU yaongeza muda wa udahili

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu (TCU) imetangaza kuongeza muda wa udahili kwa siku nne kuanzia Oktoba Mosi kwa baadhi ya vyuo ambavyo bado vina nafasi.

Imesema uamuzi huo umelenga kutoa nafasi kwa wanafunzi ambao hawakufanikiwa kudahiliwa katika awamu tatu zilizopita za udahili kwa mwaka wa masomo 2019/20.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa wamechukua uamuzi huo baada ya kupokea na kuyafanyia kazi maombi ya waombaji wa udahili ambao hawakupata nafasi kutokana na sababu mbalimbali.

"Tumeamua kufungua dirisha la udahili la awamu ya nne baada ya kukamilika kwa awamu zote tatu za udahili kwa mujibu wa ratiba iliyoidhinishwa," alisema.

Prof. Kihampa alisema TCU imepokea maombi ya kuongeza muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya vyuo ambavyo bado vina nafasi za udahili katika baadhi ya programu za masomo kwa mwaka 2019/20.

"Tume inaongeza muda wa udahili kwa kufungua nafasi za udahili kwa awamu ya nne itakayofanyika kwa siku nne kuanzia Oktoba 1-4," alisema.

Kuhusu awamu zilizopita, kiongozi huyo wa TCU alisema: "Jumla ya waombaji 96,338 walituma maombi katika awamu zote tatu kwa vyuo 75 vilivyoruhusiwa kudahili kwa mwaka wa masomo 2019/20.

"Waombaji 82,758, sawa na asilimia 85.9 wamedahiliwa katika vyuo hivyo. Kati ya hao, waombaji 37,450, sawa na asilimia 45 ya wadahiliwa wote, walidahiliwa na zaidi ya chuo kimoja.

"Mpaka sasa, waombaji 33,453, sawa na asilimia 89.3 wameshajithibitisha katika chuo kimoja na wengine wanaendelea kujithibitisha hadi Septemba 30."

Aliongeza kuwa Tume inaendelea kuwasisitizia waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja ambao bado hawajajithibitisha, wafanye hivyo katika vyuo wanavyovitaka kusoma mapema iwezekanavyo ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

"Tume inatoa wito kwa vyuo vyote vya elimu ya juu kubainisha programu zenye nafasi ili kuwawezesha waombaji kufanya uamuzi sahihi wakati wa kutuma maombi ya udahili na kuepusha usumbufu kwa waombaji kuomba programu ambazo hazina nafasi," alisema.

Prof. Kihampa pia alivitaka vyuo vyote kuzingatia idadi ya wanafunzi iliyoidhinishwa katika programu husika.

"Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili ama kujithibitisha, yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo na siyo TCU," alisema.

Prof. Kihampa alisema kwa wale ambao wana changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupoka taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

# Moto Coco Beach watia hasara bil. 1/-

**Na Frank Monyo**

MMILIKI wa maeneo ya biashara katika ufukwe wa Coco, Alphonce Buhatwa, amesema hasara iliyopatikana baada ya eneo hilo kuungua moto Jumapili ni zaidi ya shilingi bilioni moja.

Amesema kuwa majengo yaliyokuwa katika eneo hilo yaliyoungua yana thamani ya zaidi ya Sh. milioni 900 na vifaa vilivyokuwamo vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 300.

Alitoa maelezo hayo jana wakati akizungumza na wanahabari kutoa pongezi kwa Rais John Magufuli kwa kuwaruhusu kuendelea na biashara katika eneo hilo, huku mradi wa ujenzi wa Coco Beach ukiendelea.

"Katika tukio la moto zaidi ya asilimia 80 ya majengo yaliungua moto pamoja na vifaa vyake vyote vilivyokuwamo ndani kwa hiyo thamani ya vitu vyote ni zaidi ya shilingi bilioni moja," alisema.

Aliongeza kuwa anaamini kamati iliyoundwa kuchunguza tukio hilo itatoa majibu kamili ya chanzo cha moto huo kwa sababu wao ni wataalamu wa majanga ya moto.

Alisema anasikitishwa na taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikidai kuwa kwa vile manispaa imepanga kuendeleza eneo hilo, wafanyabiashara wameamua kuchoma kwa makusudi ili walipwe na bima.

"Kumekuwa na mgogoro kwa muda mrefu, hivyo hili eneo mimi sikuwahi kulikatia bima, na si rahisi kwa mtu asiye na bima achome mali yake, lakini kweli Manispaa walikuwa na mipango ya kuendeleza eneo hili... naiamini serikali ya Rais Magufuli haki yangu itapatikana katika njia stahiki," alisema Buhatwa.

Aliongeza kuwa wanaosambaza kuwa eneo hilo limechomwa kwa makusudi wakijua kuwa eneo hilo halikuwa na bima, wataelewa kilichotokea, hivyo anaamini mgogoro uliopo unaendelea kushughulikiwa na viongozi wa serikali na atapata haki yake.

Mwenyekiti wa Uokoaji, Utunzaji Mazingira na Usalama katika eneo hilo, Ahmed Ahmed, alimpongeza Rais Magufuli kwa kuwajali wafanyabiashara wa Coco Beach kwani juzi walisikia hotuba yake ikizungumzia suala la ufukwe huo na kuwataka wafanyabiashara hao wasiondoke.

# Vijana 400 wapata ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Antony Mavunde, ameipongeza kampuni ya RoutePro kwa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kutengeneza ajira kwa zaidi ya vijana 400 nchini.

Mavunde aliyasema hayo jana wakati wa hafla fupi ya kuwakabidhi vijana 30 pikipiki kwa ajili ya kusambazia bidhaa mbalimbali.

Vijana hao waliokabidhiwa pikipiki na kampuni hiyo ni kutoka katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida, Moshi na Dar es Salaam.

Akikabidhi pikipiki hizo, Mavunde alisema zitawasaidia vijana hao kuondokana na changamoto ya ajira na kujiongezea kipato.

"Niwapongeze ndugu zangu wa kampuni ya RoutePro kwa hiki ambacho mmekifanya hapa pamoja na kutoka pikipiki hizi leo, lakini mpaka sasa mmeshatoa kwa vijana wengine nchi nzima zaidi ya 400," alisema Mavunde.

Aidha, aliwataka vijana hao kuzitunza pikipiki hizo ili kutoa imani kwa kampuni, hiyo kuwasaidia vijana wengine nchini.

Naye Meneja Uratibu wa kampuni hiyo, Jaja Mbazila, alisema wamewachagua vijana kutokana na rekodi yao ambao wamewahi kufanya nao kazi katika miradi mbalimbali ya usambazaji wa bidhaa wenye bidii ya kutaka kukuwa kibiashara.

"Tumelenga kuwawezesha vijana wenye bidii ya kazi na kujituma kupata fursa kuwa na biashara zao. Tumefanya nao kazi kwa karibu katika miaka iliyopita na wameonyesha kuwa na nia ya kufanya biashara ya usambazaji," alisema Mbazila.

Alisema mbali na kuwapa pikipiki pia watawasaidia vijana hao kiasi cha Sh. 100,000 kwa kila mmoja ili ziwasaidie kwa kila kuanzia kazi.

Pia alisema vijana hao 30, watapatiwa mafunzo ya elimu ya biashara na usambazaji pamoja kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa ya kusaidia kuratibu usambazaji na taarifa.

"Vijana hao pia wataunganishwa na wadau wake katika biashara na wazalishaji wengine na kushirikiana nao kusambaza bidhaa za wateja katika masoko, mkakati ambao utawanufaisha vijana hao na kampuni kwa kugawana faida itakayo patikana nusu kwa nusu," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Taifa, Freeman Mbowe (wa pili kushoto), akijadiliana jambo na viongozi wengine wa chama hicho, wakitoka kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayowakabili kuahirishwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maombi vigogo Chadema yagonga mwamba

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu ya Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imekataa maombi ya Katibu Mkuu Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko ya kusafiri nje ya nchi kuhudhuria mikutano kupitia nyadhifa zao.

Kadhalika, mahakama hiyo imesema ikiruhusu maombi ya namna hiyo, ikizingatia washtakiwa wengi wao ni wabunge, kesi haitaendelea. Kwa mantiki hiyo, mahakama imesema washtakiwa lazima wafuate ratiba ya mahakama inavyoelekeza.

Akisoma uamuzi huo, Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba alisema bila kujali nyadhifa za, viongozi hao wako mahakamani kama washtakiwa wengine.

"Mahakama hii imekataa kuwaruhusu washtakiwa kusafiri kwenda nje ya nchi kwa sababu ikiruhusu utaratibu huu ukaendelea, kesi haitakwisha. Kesi hii inatakiwa isikilizwe imalizike kwani inapigiwa kelele imekaa muda mrefu," alisema hakimu.

Alisema kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa utetezi mfululizo siku tano kuanzia Oktoba 7 hadi 11, mwaka huu, na mahakama inategemea kuwa hakutakuwapo na sababu zingine zozote zitakazosababisha isianze kusikilizwa.

"Mahakama imeona maombi ya utetezi hayana mashiko ya kisheria kwa sababu kesi hii kwa sasa haiko kwenye hatua ya kutajwa. Washtakiwa walikutwa na kesi ya kujibu na sasa wanatakiwa kuanza kujitetea dhidi ya mashtaka yanayowakabili," alisema Hakimu Simba.

Akifafanua zaidi alisema upande wa utetezi umesema mahakamani kwamba unatarajia kuita mashahidi wengi kupangua kesi ya Jamhuri hivyo inatakiwa kuwa na muda wa kutosha kusikiliza.

Juzi, Wakili wa washtakiwa, Profesa Abdallah Safari, aliwasilisha maombi mawili mahakamani hapo ya kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 7 na 8, mwaka huu, kwa sababu wanahitaji kupata muda wa kutosha kujiandaa na utetezi. Ombi la kwanza, waliarifu mahakama kwamba Dk. Mashinji ameshindwa kuhudhiria kesi hiyo kwa sababu ana kesi nyingine iliyopangwa Septemba 23, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Songea.

Ombi la pili, Matiko anakwenda kuwakilisha Bunge Kigali nchini Rwanda na Ubelgiji.

Alidai kuwa Dk. Mashinji anatarajia kusafiri Septemba 29 mpaka Oktoba 6, mwaka huu na Matiko mkutano utaanza Septemba 25 mpaka 28, mwaka huu na mkutano mwingine utaanza nchini Ubelgiji Oktoba 7 na 8, mwaka huu.

Hata hivyo, Nchimbi alidai kuwa wamepokea hati ya Dk. Mashinji kuitwa Mahakama ya Songea kwa hilo hawana pingamizi.

Alidai kuwa kuhusu ruhusa washtakiwa hao wanafahamu kwamba tarehe wanazosafiri kesi yao inasikilizwa hivyo Jamhuri inapinga mahakama kuwaruhusu.

Mbali na Dk. Mashinji, Matiko, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chadema, Freeman Mbowe; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya, na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama kwa madai kwamba Februari 1 na 16, mwaka jana, Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

# Ahueni wazawa udhibiti bidhaa za nje

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ya awamu ya tano itaendelea kudhibiti uingizwaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipotembelea kiwanda cha maziwa cha Asas, akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Iringa.

Alisema serikali imedhamiria kukuza uchumi na kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kupitia sekta ya viwanda.

Waziri Mkuu alisema serikali inaamini kuwa uchumi wa viwanda ukiimarika uchumi utakuwa kwa kasi kubwa na matokeo yake yataonekana wazi kwa kupanua wigo wa ajira, soko la huduma na shughuli zingine za kiuchumi.

"Serikali imefanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya mifugo ili kuhakikisha inaleta tija kwa wafugaji na taifa kwa ujumla, hivyo wafugaji endeleeni kuimarisha ushirika wenu.

Wizara ya Mifugo iendelee kuwaelimisha wafugaji ili wafuge kitaalamu," alisema.

Waziri Mkuu ameipongeza kampuni ya Asas kwa sababu ni miongoni mwa kampuni chache ambazo zimeanza kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni bora za ufugaji wa kisasa na kuwapa uhakika wa soko.

Kwa mujibu wa Majaliwa, serikali inathamini sana uwekezaji uliofanywa na kampuni ya Asas kwa sababu imeitikia wito wa serikali wa ujenzi wa uchumi kupitia sekta ya viwanda, hivyo itahakikisha wawekezaji wote wanufaika na uwekezaji wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asas Dairies Limited, Fuad Abri, alisema kiwanda kina mpango wa kupanua uzalishaji kwa kujenga kiwanda kingine cha kusindika maziwa katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya na kiko katika hatua za mwisho kukamilika.

Awali Waziri Mkuu alizindua kiwanda cha maji cha Mkwawa cha mjini Iringa na kusema ujenzi huo ni njia ya uhakika ya kupunguza tatizo la ajira na kwamba itaendelea kushawishi wawekezaji wa ndani na nje ili wananchi wengi wapate ajira.

"Serikali imetoa wito kwa wawekezaji wawekeze katika viwanda mbalimbali nchini, hivyo ni muhimu wawekezaji hao wakalindwa na wasibugudhiwe ili kuendelea na uzalishaji wa bidhaa zao. Watumishi mlioajiriwa fanyeni kazi kwa uaminifu," alisema.

Naye Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Maji cha Mkwawa, Ahmed Huwel, alisema kiwanda chao kilianzishwa mwaka 2017 kwa lengo la kuzalisha na kufanya biashara ya maji safi na salama na kuunga mkono mkakati wa serikali wa ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema kiwanda chao kimeajiri watumishi 158 kati yao wanaotoka nje ya nchi ni watatu tu na kwa upande wa ajira zisizo rasmi ni zaidi ya 3,000 na kwamba wanatarajia kuongeza ajira kwa wananchi wengi zaidi baada ya kukamilisha ujenzi wa kiwanda kingine cha kutengeneza vinywaji baridi.

# Serikali yataka sheria za uwekezaji zifuatwe

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGEA

SERIKALI imewataka wawekezaji wanaotaka kuwekeza nchini kufuata sheria na taratibu za nchi ili kuepuka matatizo katika ulipaji kodi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alitoa tahadhari hiyo wilayani Mbinga mkoani Ruvuma alipotembelea mgodi mpya wa uchimbaji makaa ya mawe wa Mil coal. Alisema baadhi ya wawekezaji wanatumia njia za mkato na kukwepa kulipa kodi hali inayosababisha kuingia kwenye migogoro isiyokuwa na tija.

Waziri Kairuki alisema serikali haipendi kuona matatizo katika uwekezaji wowote nchini kwa kuwa lengo ni kuhakikisha uwekezaji unaleta tija kwa taifa na kwa jamii inayowazunguka.

Pia, aliwataka wawekezaji kutoa taarifa kwa ngazi nyingine endapo wataona kuna mahali wanakwama au kukwamishwa na mtumishi yeyote wa serikali au taasisi na kuitaka sekta binafsi kuchangamkia fursa zilizopo nchini kuwekeza na pale wanapoona uwezo wao ni mdogo ni vyema wakatafuta wageni wenye uwezo wakashirikiana nao.

Alisema serikali itaendelea kusimamia stahiki za wawekezaji wazawa ambao wanashirikiana na wawekezaji kutoka nje kuhakikisha wanapata asilimia zao za uwekezaji kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Kwa upande wao wawekezaji wa mgodi huo, Mussa Charles na Vidya Sagar, wameeleza mipango ambayo tayari wameanza kutekeleza hasa upande wa kutoa huduma za jamii ikiwamo ujenzi wa barabara.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mkewe Mary, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kiwanda cha Maji cha Mkwawa, Ahmed Huwel (kulia), kutembelea kiwanda baada ya kukizindua mjini Iringa jana. Wa pili kushoto ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tamisemi, Josephat Kandege. **PICHA: OWM**

## Madaktari bingwa kufanya upasuaji wa magoti, nyonga

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa kutoka nchini India wameanza kuwafanyia uchunguzi na upasuaji wagonjwa wenye matatizo ya magoti na viungo nchini.

Huduma hiyo ya uchunguzi na upasuaji inafanywa katika Hospitali ya Regency ambayo inashirikiana na Hospitali ya HCG Group ya India kwa siku tatu kuanzia leo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Hospitali ya Regency jana, wataalamu hao wataendesha kambi hiyo kwa watu wenye matatizo ya viungo kama magoti na mgongo.

Iliwataja wataalamu watakaoendesha kambi hiyo ya siku tatu ni Dk. Yuvraj Lakum ambaye ni daktari bingwa wa nyonga na magoti akisaidiana na Dk. Kuastubh Chauhan.

Taarifa hiyo ilisema wataalamu hao watatumia mbinu mpya kwenye upasuaji ambayo ni kukata sehemu ndogo kuhakikisha mgonjwa anapona mapema.

Ilisema ujio wa wataalamu hao utapunguza gharama za wagonjwa kwenda nje ya nchi kufuata tiba hiyo.

"Katika jitihada za kupunguza rufani za wagonjwa kwenda matibabu nje ya nchi na kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo zimekuwa zikitumika tumeona ni vyema kuita mara kwa mara mtaalamu huyu kufanya upasuaji hapa Dar," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, ujio wa wataalamu hao umekuwa ukisaidia kuwapa ujuzi wataalamu wa ndani ili mwishowe wawe na utaalamu wa kufanya upasuaji wa aina hiyo wenyewe.

Aidha, ilisema mpango wa kuita madaktari hao bingwa wa magoti na viungo umekuwa ukiratibiwa na Hospitali ya Regency kwa kushirikiana na Hospitali ya HCG Multi-Specialty iliyoko Ahmedabad, India.

"Tunatarajia mtaalamu huyo atafanya uchunguzi kuanzia tarehe nane Juni hadi tarehe kumi na wale watakaobainika kuwa na matatizo hayo watafanyiwa upasuaji baada ya wiki sita.

"Hii ni fursa ya kipekee kwa Watanzania wenye matatizo kama haya kuchangamkia fursa hii kwani badala ya kwenda nje na kutumia gharama kubwa kusafiri na wasaidizi wao kwenda nje ya nchi sasa wanafanyiwa upasuaji hapa hapa nchini," ilisema taarifa hiyo.

## Mbunge ashangazwa DC kumsweka ndani

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro, Lucy Owenya (Chadema), amedai kushangazwa na amri ya kukamatwa iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akidaiwa kufanya siasa kinyume cha utaratibu. Owenye anasema kwamba alifuata taratibu zote na kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

Mbunge huyo jana alisema kuwa kabla ya kuitembelea Shule ya Sekondari ya Rundugai alitoa taarifa kwa mamlaka husika ikiwamo

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai na Mkuu wa Shule hiyo na kuongeza kuwa yeye kama mbunge wa Mkoa eneo lake la kazi ni mkoa wa Kilimanjaro, na kwamba anayo haki ya kuleta maendeleo katika mkoa wake.

"Nilishangaa tulikamatwa kwa sababu wiki iliyopita niliwasiliana na Katibu wa Mbunge (Jimbo la Hai) ambaye ni Irene Lema, nikamwambia aende halmashauri kumjulisha mkurugenzi kuwa tutaitembelea ile shule na alipomjulisha alikubali na kumwambia Irene amjulishe na mkuu wa shule wa hiyo shule na Irene akafanya hivyo," Owenya alisema. Mbunge huyo alikamatwa na Polisi Wilaya ya Hai na kupelekwa katika Kituo cha Polisi cha Bomang'ombe alipokwenda kuitembelea shule hiyo kwa amri ya Mkuu wa Wilaya hiyo akidaiwa kufanya siasa kinyume cha utaratibu.

Akizungumza na gazeti hili wiki iliyopita Mkuu huyo wa Wilaya alidai kukamatwa kwa mbunge huyo ni kutokana na kutokufuata taratibu ikiwamo kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Wilaya. Sabaya akidai upo utaratibu kwa mbunge anapotaka kutoa msaada katika shule ili kuwezesha misaada hiyo kuratibiwa na serikali.

"Yapo maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kuwa yeyote anayetaka kutoa misaada katika shule yoyote atoe taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili misaada hiyo ijulikane lengo lake na Kuratibiwa," Sabaya alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kurejea maazimio Beijing ni muhimu kufikia usawa

**SUALA** la usawa wa kijinsia na haki sawa kwa wote ndiyo msingi wa maendeleo ya kila kitu.

Ndiyo maana wakati wote suala la kuwa na usawa wa kijinsia na heshima kwa haki za binadamu linatajwa kuwa kipaumbele cha maendeleo. Haiwezekani kuwa na mafanikio katika jamii iwapo baadhi ya makundi hasa wanawake, walemavu na wanyongwe wataachwa na haki zao kupuzwa.

Tunayasema haya kwa kurejea Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake uliofanyika Beijing China mwaka 1995, ambao pamoja na kuzungumzia madhila ya wanawake, ulitaka usawa wa kijinsia, wanawake kuthaminiwa haki na utu wao na pia ushirikishwaji kupewa kipaumbele ili kuleta maendeleo kwa wote. Leo hii tunapotizama nyuma miaka 24 iliyopita na kufuatilia maazimio ya Mkutano wa Beijing tunaona kuwa kuna mambo mengi yanayoendeleza unyanyasaji wa wanawake na watoto ndiyo maana linakuwa kama jukumu endelevu la kuhamasisha usawa na haki za binadamu na hasa usawa wa kijinsia na haki za wanawake.

Ndiyo sababu vikundi vya wanaharakati wanawake nchini vinataka kutafsiri kwa Kiswahili Azimio la Mpango Kazi wa Beijing, ili kuwawezesha watu wengi kuuelewa na kufuatilia utekelezaji wake. Tafsiri hiyo ya Kiswahili inaweza pia kutumika katika nchi jirani ambazo zimeanza mpango wa kutumia lugha hiyo, hasa baada ya mkutano wa hivi karibuni wa nchi wanachama wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Balozi, mwanasiasa na mwana diplomasia, aliyeongoza Mkutano wa Beijing, Getrude Mongella, ni miongoni mwa wanaohamasisha kuwa na tafsiri hiyo ambayo ni muhimu katika kujenga usawa wa kijinsia.

Ni wazi kuwa mpango kazi la Beijing ndiyo unaoeleza kwa undani jinsi ya kuendeleza harakati za kuwakomboa wanawake. Ni chapisho ambalo linaainisha jinsi ya kudhibiti ukatili dhidi ya wanawake kwa mfano, ndoa za mabinti wanaoozwa utotoni na kuwakatisha masomo huku wakilazimishwa kuwa mama katika umri mdogo.

Hali kama hiyo inachangia na kuongeza umaskini kwa vizazi vingi. Kwani mama mtoto tena ni maskini, bila shaka na mwanae atakuwa maskini lakini pia vijukuu na vitukuu vitaendelea kuwa maskini kwa miongo mingi.

Tunaona kuwa iwapo mpangokazi huo utaandaliwa kwa Kiswahili kama anavyosena Balozi Mongela utasomeka kila mahali hasa vijijini na watu wengi wataufahamu na kuutumia kudai na kutetea haki za wanawake na usawa wa kijinsia kuanzia mabinti kusoma bila kuozwa utotoni.


Yote hayo yatafanikisha malengo ya dunia ya kuutokomeza ujinga.

Tunaelezwa kuwa Azimio la Mpango Kazi wa Beijing linabeba mambo yote yanayohusu uwezeshaji wa wanawake ili kuondoa vizuizi vyote vya ushiriki wao katika sekta zote zote za maisha. Ndiyo maana tunajiunga na wanaharakati kuukubali wito wa kuutafsiri mpango huo kwani, iwapo utatafsiriwa utawafikia wengi kwa lugha ya taifa na kulifanya suala la usawa wa kijinsia kueleweka na kutekelezwa na wengi.

Tunaamini kuwa mpango kazi huu unaposomwa na wengi utawaandaa wanawake kufanya mambo mengi yanayohusu ustawi, ushirikishwaji na ushiriki wa wanawake kwenye uchumi, siasa, uwekezaji na kwenye majukwaa yanayohitaji uwakilishi wa wote. Wanawake watajua tena watakuwa na haki ya kuhoji na kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa kwa kuwa kuna maridhiano ambayo taifa limeyakubali kuhusu maendeleo yao.

Tunapongeza na kushauri kazi ya kutafsiri ifanywe ili kuleta uwajibikaji wa pamoja katika utetezi wa haki za wanawake mahali popote katika taifa letu ili kujipatia maendeleo endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Nimeuhusudu mradi wa 'Dreams' unavyofunda hatari waliopevuka

Na Sabato Kasika

**MAAMBUKIZI** mapya ya ugonjwa wa Ukimwi sasa mkongwe nchini, ukivuka umri wa ujana na uko katika mitaa ya miaka 40.

Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids), inasema waathirika wa ugonjwa huo, asilimia 40 ni kinamama, huku katika mtazamo wa umri kwa jumla ya wanajamii, asilimia 80 ni vijana.

Tacaids inaeleza kujitahidi kutoa elimu ili waepuke maambukizi hayo, pia kukwepa vishawishi katika maeneo mbalimbali.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji tume hiyo, Jumanne Issango, aliwahi kusema katika mkutano wa mwaka wadau wanaotekeleza afya za wasichana balehe na wanawake vijana nchini.

Mkutano ulifanyika Aprili mwaka huu, jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa tume hiyo, itapanua mipaka katika mikoa mingine nchini, ikiwa miradi inayoendelea ukiwamo wa 'dreams' wa kumjengea uwezo msichana ajitambue.

Kwa upande wake akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, anasema tafiti zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya ugonjwa wa Ukimwi, yanaongezeka sana katika makundi ya wanawake vijana.

Anaongeza kwamba, lengo lililopo sasa ni kuendelea kutoa elimu kwa vijana, ujuzi na elimu ya uzazi na masuala yote ya mahusiano, ili kulipunguza kundi hilo kutoka matatizo ya kukumbwa na Ukimwi.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, kwa tume inaposema itapanua mipaka katika mikoa mingine nchini, basi ni wakati muafaka kuifikia mikoa inayokabidiliwa na changamoto za mimba kwa wanafunzi.

Baadhi ya mikoa inayokabiliwa na changamoto hizo na kusababisha wanafunzi kutotimiza ndoto zao za baadaye kielimu, jambo kubwa zaidi kwao ni kwamba wako kwenye hatari ya kukumbwa na maambukizi mpya ya virusi vya Ukimwi. Suala la wanafunzi kupata mimba, ni kiashiria cha wazi kwao wanaendekeza ngono isiyo salama, hali inayowaweka kwenye hatari zaidi ya kukumbwa na magonjwa ya zinaa, ukiwamo Ukimwi.

Kundi linalotajwa kuwa kwenye hatari hiyo, ni la kuanzia miaka 15 hadi 24 na ndio maana tume inasema, mradi wa 'Dreams' unalenga kuwajengea uwezo wasichana wajitegemee katika nafasi ya umri wao.

Kikubwa zaidi kinacholengwa hapa, ni kutaka kuwasaidia ili wasijiingize katika hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi, ambayo mwisho wa siku ni kupoteza maisha.

Ukimwi upo kote nchini, lakini pia nguvu kubwa ingeelekezwa kwenye mikoa inayokabiliwa na changamoto ya mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Kwa mfano, Lindi na Ruvuma ni miongoni mwa mikoa, inayokabiliwa na changamoto ya mimba kwa wanafunzi, hali inayosababisha baadhi ya wanafunzi washindwe kuendelea na masomo. Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, amewahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema kwamba kwa kipindi cha miezi nane tu mwaka huu, wanafunzi 100 mkoani kwake wamekatisha masomo kwa sababu ya mimba. Wakati Mkoa wa Lindi kukiwa hivyo, Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, imekuwa imetia fora kutokana na mkuu wa wilaya hiyo, Julius Mtatiro, kusema wanafunzi zaidi ya 100 wamekatisha masomo kwa tatizo hilo.

Hali hiyo ndio inayonisukuma niseme kuwa mradi wa 'Dreams' uelekezwe kwenye mikoa yenye tatizo la mimba kwa wanafunzi, kwa kuzingatia kwamba kitendo kinachosababisha mimba, pia ndio chanzo cha Ukimwi.

Vitendo vya kuwapo idadi kubwa ya mimba kwa wanafunzi, ni dalili tosha kwamba wahusika hawana elimu ya kuwawezesha kujitambua na kuwa makini katika masuala ya kujamiiana. Tume imeshaweka wazi kuwa elimu hiyo inalenga kuwasaidia vijana kuwa na ujuzi ia kupata kazi za kufanya kiuchumi na kuona umuhimu wao kama binadamu, ili kupunguza kundi hilo kutoka katika tatizo la Ukimwi.

Ninaamini kwamba, inaweza kuwasaidia wanafunzi kutulia na kuelekeza nguvu kwenye masomo, ili hatimaye watimize ndoto za baadaye, kuliko kuendelea kutenda pasipo tahadhari.

Hivyo, Tacaids inapopanga mikakati mbalimbali ya kueneza mradi wa 'Dreams' iwakumbuke wanafunzi, waliokuwa wakikatisha masomo, kwa sababu ya mimba ili kuepusha na madhara ya Ukimwi.

BARUA/MJADALA

# Hii kero Mikese hadi lini?

**Ndugu Mhariri**

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je, kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*

*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

**Ahsante ni sisi wanakitongoji, Ukomanga-Fulwe, Mikese.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Ushabiki wa kikandanda uhamie uchaguzi S/Mitaa



Wananchi wakiwa katika foleni ya kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wao, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

KATI ya mambo yanayosisimua watu duniani zama hizi ni mpira wa miguu. Kandanda huwavuta wengi na wakati mwingine huondoa mipaka baina ya mataifa.

Lakini pamoja na kandanda, jambo jingine linalowaweka watu karibu tena nyakati hizi, linaweza kuwa mchakato wa uchaguzi.

Uchaguzi mkuu unaohusisha kupata viongozi wa mataifa mbalimbali na hata ule wa wabunge, madiwani na wa serikali za mitaa na vijiji kwa Tanzania ni mambo yanayowasogeza watu karibu hasa kujua hatima ya mgombea ama yule wanayemtaka.

Au pengine chama wanachokishabikia na kupigia kura ili kiongoze.

Uchaguzi huwafanya watu wengi kufuatilia na kupata matokeo kama ilivyo kwa mpira wa miguu.

Kwa hiyo kama ambavyo Watanzania wengi wanasisimka kwenye kufuatilia washindi wawe wa kombe la dunia na klabu bingwa Afrika ndivyo hivyo waelekeze hamasa hiyo kuwachagua viongozi wa serikali za mitaa mwezi Novemba.

Ni wakati wa kufahamu kuwa uongozi bora kama zilivyo timu bora kwenye kandanda, ndicho chanzo cha mafanikio kimaendeleo.

Kwa hiyo uchaguzi wa serikali za mitaa usiwe tena suala la kulemaa, kwani ni wajibu wa kila mtu kama watu wanavyofurahia ushindi wa Taifa Stars na Kilimanjaro Heroes, ndivyo pia inavyofaa kusisimka na kupiga kura na kuwafurahia viongozi bora watakaowachagua.

Kuna maelezo ya baadhi ya watu wakisema kwamba hawatashiriki uchaguzi. Mambo hayo hayana sababu. Ni vizuri kushiriki kwenye uchaguzi wa viongozi watakaowakilisha maslahi ya wananchi.

Si vyema watu kuzizungumza changamoto na kasoro za uchaguzi kwa nyakati zote, badala yake ni vizuri kuziweka pembeni na kutambua kuwa jukumu la kupata maendeleo ndilo kipaumbele.

Kwa hiyo ni vyema tena ni haki kikatiba kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwachagua viongozi ambao watayawakilisha maslahi ya wote.

Ya wote kwa maana ya vijana, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee na wahitaji wengine kwenye jamii wasio na sauti ili wote wapate maendeleo.

Ni vyema kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na kuchagua watu ambao wananchi wanawaamini kuwa wanaweza kuwaongoza, badala ya kulalamikia utaratibu na changamoto za uchaguzi.

Watanzania wanaposhiriki uchaguzi wa serikali wa mitaa ndiyo wakati wa kuwa na viongozi katika ngazi za chini wanaoweza kuzungumzia vipaumbele vya maendeleo.

Leo hii tatizo kubwa linaloikabili jamii ni umaskini na vijana wengi kukosa ajira. Viongozi hawa wanaochaguliwa wabanwe ili kuwasaidia vijana kukabiliana na tatizo hilo la kukosa kazi.

Wanatakiwa viongozi wanaotatua kero hizo kwa kutekeleza sera na mipango inayoandaliwa na serikali kwenye maeneo yao.

Zama hizi si suala la kuomba wafadhili, ni muda wa kutumia rasilimali zilizoko kwa ajili ya maendeleo. Je, viongozi wanalitizamaje hilo?

Lakini si hivyo tu kuna matatizo ya chakula kwa ajili ya watoto shuleni, maana bila chakula watoto hawawezi kufanya vizuri kimasomo.

Wakati huu wa kuchagua viongozi wa vijiji na mitaa, suala la kuwahudumia watoto shuleni kwa chakula ili wasome kikamilifu nalo ni kipaumbele.

Aidha, matatizo ya mimba za utotoni unyanyasaji watoto, wanawake pamoja na wazee ni majukumu ambayo viongozi wa vijiji na mitaa wanatakiwa kuyasemea.

Kwa hiyo si wakati wa kujiweka nyuma ni muda wa kuwachagua viongozi wanaosaidia kushughulikia changamoto nyingi katika vijiji na mitaa ambayo ndiyo yenye watu wengi na matatizo hayo yanaripotiwa kwa wingi.

Dunia leo inakabiliwa na tatizo la mabadiliko ya tabianchi. Ni jambo linalotikisa karibu kila taifa. Viongozi wanaochaguliwa wana hamasa kiasi gani kuhusu ulinzi wa mazingira na kutunza rasilimali za nchi ili kuwa na Tanzania salama.

Uchaguzi wa serikali za mitaa, ndiyo utakaozalisha viongozi wa kuisimamia Tanzania, isiyogeuka jangwa kutokana na kuchoma mkaa, kuhujumu misitu na kukausha vyanzo vya maji.

Wakati watu wanajitizama kuwa wanatarajia kuchaguliwa kuwa viongozi, wanatakiwa wale wanaojituma.

Kuna maeneo mengi hayana maji lakini viongozi wanashindwa kufuatilia kwenye mamlaka ili kupata ufumbuzi wa muda mfupi wakati ujenzi wa miundombinu ukiendelea.

Viongozi wa serikali za mitaa, waache kukaa ofisini na kusumbua wananchi wanapotaka kujenga nyumba zao, nao wawajibike kuhudumia wananchi badala ya kuwa wasumbufu na wakwamishaji wa maendeleo.

Maeneo mengi vijijini yanakabiliwa na ubadhirifu wa fedha za maendeleo kama michango ya miradi ya maendeleo kuliwa na wachache.

Aidha, kuna migogoro ya ardhi, wafugaji kukosa malisho na changamoto za ukosefu wa maji, kero kwenye kodi na tozo kwa wakulima na wazalishaji wengine.

Ni vyema wanaotarajia kugombea uongozi washughulikie kero hizo na nyingine badala ya kufikiria kuwa mamangimeza.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Chadema watia neno cheche za IGP Sirro

Na Enock Charles

SIKU moja baada ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kukemea kile alichokiita ubinafsi na kwenda kinyume cha taratibu za kazi kwa baadhi ya makamanda wa polisi, Chadema kimetaka kuwapo kwa mabadiliko ya vitendo ndani ya jeshi hilo.

Chama hicho cha Demokrasia na Maendeleo kimesema mabadiliko hayo yaende sambamba na kufanya uchunguzi wa matukio ya watu kupotea, kupigwa risasi na kutekwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, mabadiliko hayo pia yafanyike kwa kuhakikisha kunakuwa na mitaala ya mafunzo, sheria na utendaji ili kulifanya Jeshi la Polisi kuwa chombo hicho cha kutoa huduma badala ya chombo cha mabavu kama ilivyo sasa.

Katika taarifa yake hiyo, Makene alisema ndoto ya IGP Sirro kuona siku akiondoka madarakani analiacha jeshi hilo likiwa na heshima na utendaji wa kuridhisha, itatimia ikiwa ushauri wao huo utazingatiwa.

"Kwa kuanzia tunataka kuona wanashughulikia matukio mbalimbali yakiwamo ya watu kupotea, kushambuliwa, kutekwa, kuteswa na wengine kuokotwa wakiwa wamekufa, kwa kufanya uchunguzi, kuwabaini watuhumiwa na kuwafikisha mbele ya sheria," alisema.

Makene aliyataja baadhi ya matukio ya aina hiyo kuwa ni la kushambuliwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Chadema, Tundu Lissu, ambaye pamoja na kushambuliwa mchana, katika eneo la nyumba za serikali, akiwa anatokea kazini kwake bungeni, hadi sasa hakuna aliyekamatwa wala kesi kufunguliwa.

Alisema tukio lingine ni kupotea katika mazingira tatanishi kwa mwandishi wa habari wa magazeti ya Mwananchi na The Citizen, Azory Gwanda, Novemba 21, 2017. Alisema tukio lingine ni kupotea kwa Msaidizi wa Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Bernard Saanane, tangu Septemba mwaka 2017, ambaye pamoja na kuripoti kituo cha polisi juu vitisho vya maisha yake, jeshi hilo halikuchukua hatua dhidi ya wahusika.

Tukio jingine ambalo pia IGP aliligusia ni kuuawa kwa mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT) Akwilina Akwiline, ambaye alipigwa risasi akiwa kwenye daladala Februari 16, 2018.

Alisema tukio jingine ni kupotea kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo, Simon Kanguye, tangu Julai 20, 2017 ambaye pamoja na kuwapo maelezo ambayo yangeweza kusaidia Jeshi la Polisi kuanzisha uchunguzi na kubaini ukweli wa tukio hilo, hadi sasa jeshi hilo halijawahi kutoa taarifa rasmi ya maendeleo ya jambo hilo.

Alisema tukio lingine ni kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa aliyekuwa Kiongozi wa Chadema Kata ya Hananasif, John Daniel, aliyefuatwa nyumbani kwake na watu wasiojulikana na baadaye kukutwa amekufa maeneo ya Coco Beach jijini Dar es Salaam.

"Tumetaja matukio hayo kwa uchache ili kuonyesha namna ambavyo IGP Sirro anapaswa kujua kuwa tatizo la utendaji wa Jeshi la Polisi nchini linaangaliwa kwa mwonekano wake wa nje zaidi katika kutimiza wajibu wa kulinda raia na mali zao, kuliko masuala ya ndani ya kiutawala yanayoamua nani ashike nafasi ipi na wakati gani," Makene alieleza katika taarifa hiyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa, akikabidhi funguo za gari aina ya Toyota IST kwa Olen Misigaro, aliyeibuka kidedea katika kampeni ya DCB Lamba Kwanza iliyokuwa ikiendeshwa na wafanyakazi wa benki hiyo. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara, James Ngaluko na Evelyn Rugambo (kushoto) wote kutoka DCB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kujiunganishia umeme bila kulipa kwa miaka 2

Na Idda Mushi, MVOMERO

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Morogoro, limewataka wananchi kuwa makini na watu wanaojifanya ni wafanyakazi wa shirika hilo, baada ya kumkamata mtu mmoja akidaiwa kuiba umeme.

Anadaiwa kukutwa amejiunganishia nyaya moja kwa moja bila kupitia kwenye mita huko Turiani wilayani Mvomero.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa katika mtaa wa Mtoni Kata ya Sungaji, Turiani wilayani Mvomero na timu ya maofisa wa Tanesco waliokuwa kwenye ukaguzi.

Maofisa hao walibaini mtuhumiwa akiwa ameharibu mfumo wa luku na kujiunganishia umeme moja kwa moja bila kulipia gharama tangu mwaka 2017.

Mhandisi wa udhibiti mapato wa Tanesco Mkoa wa Morogoro, Salum Mgude, akabainisha hatua watakazo chukua dhidi ya watuhumiwa huyo, ikiwamo kumwandikia gharama na faini na gharama za matumizi ya umeme bila kulipia. "Huwa tunawapeleka pia polisi kwa sababu hii ni hujuma, uhujumu uchumi huu, kwa hiyo tunaomba wananchi wafute taratibu, wazingatie matumizi sahihi na bora ya umeme na waachane na vishoka... vishoka ndio hupeleka watu katika matatizo kama haya, utaratibu maalum," alisema na kuendelea:

"Na utaratibu rasmi wa kupata huduma unatolewa ofisini, unaweza mfuata mtu ama kwa kumfahamu au kwa kutomfahamu kumbe akawa sio mtu sahihi."

Ofisa Usalama wa Tanesco Mkoa wa Morogoro, Kevin Kapinga, akabainisha zoezi hilo litaendelea kufanywa mkoa mzima, hivyo aliwatahadharisha wananchi kuepuka wizi au hujuma zozote kwa shirika hilo.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kuwafichua wezi na wahujumu wa shirika hilo ambao wamekuwa wakisababishia hasara kubwa serikali.

"Mwananchi anayejua kunapofanyika hujuma atoe taarifa, toeni taarifa kwa maofisa watendaji, Tanesco au kwenye vyombo vya dola, na zaidi Tanesco tunatoa motisha kwa wanaoweza kutupa taarifa na ukweli na bila kumwonea mtu, nia ni kupunguza wizi na kuongeza mapato katika taifa," alisisitiza Kapinga.

Mmiliki wa nyumba iliyodaiwa kuiba umeme, Mwajabu Mdoe na Mwanae Wilson Matei wakijitetea kutohusika na wizi huo badala yake walisema walidanganywa na mtu aliyejifanya mfanyakazi wa Tanesco.

"Umeme ulikuwa hauwaki, tukawaeleza, wakasema inabidi tubadilishane mita, ndio wale Tanesco waliokuja wakasema watatuunganisha kwanza, umeme tuendelee kutumia hadi tutakapopata mita," alisema Wilson.

## Makonda adai kuhujumiwa na watendaji

INATOKA UK. 2

wake," alisema.

Makonda alisema mradi huo unamkosesha usingizi pamoja na machinjio, ujenzi wa vituo vya mabasi, masoko na barabara.

Kwa upande wao wakuu wa wilaya na watendaji wao, walieleza utekelezaji wa miradi hiyo na sababu za kukwama na ambavyo inaweza kutekelezwa na kuahidi kuondoa changamoto zilizokuwapo awali.

Sambamba na hilo, aliwaagiza wakuu wa idara zote kumpa ripoti za miradi waliyotekeleza tangu serikali ya awamu ya tano. Aliwataka ripoti hizo ziwasilishwe ofisini kwake kesho.

"Ijumaa saa 10 jioni kila mtendaji aniletee taarifa, ikiwezekana tupunguze bajeti kwa sababu kama tunatumia Sh. bilioni 480 kati ya bajeti yote ya mkoa ya Sh. bilioni 680 ya mishahara na watendaji hawafanyi kazi, ni heri tukavunja baadhi ya idara ili fedha hizo zitumike kuongezea kwenye miradi na wao wakapangiwa kazi nyingine," alisema Makonda.

Makonda pia alisema Oktoba 5, mwaka huu, watendaji wote wa mkoa huo watawasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na watakaoshindwa watawajibishwa.

## Askofu Ruwa'ichi atoka hospitali

INATOKA UK. 2

matibabu na jopo la madaktari ambao walianza kumhudumia tangu alipowasili usiku wa kuanzia Septemba 10, mwaka huu.

Alisema baada ya upasuaji waliunda jopo la wataalamu saba ambao ni madaktari bingwa watatu wa magonjwa Ubongo, Dawa za Usingizi na Magonjwa ya ndani, walaamu wa lishe, wauguzi wabobezi na wataalamu wa mazoezi tiba kwa ajili ya kuangalia maendeleo yake.

Naye Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Eusebius Nzigilwa, alisema licha ya kutiwa moyo na madaktari bingwa wa MOI kuwa Askofu Ruwa'ichi angepona, walipoteza tumaini kutokana na hali aliyokuwa nayo.

"Tunawashukuru wale wote waliomhudumia hadi leo hii anaruhusiwa, tuna furaha kubwa, alikuja hapa akiwa hajitambui, kaja kujua yupo MOI baada ya siku mbili, lakini leo hii ni mzima na amevaa hadi mavazi ya ibada," Askofu Nzigilwa alisema.

Alisema kutokana na hali aliyokuwa nayo awali akiwa Hospitali ya KCMC, waliamimi wangemsafirisha kwenda kutibiwa nje ya nchini, lakini haikuwa hivyo.

"Tunawashukuru sana madaktari walifanya kazi kubwa, Namshukuru Rais Magufuli kwa kutoa ndege iliyowezesha kumleta MOI ndani ya saa moja na wahudumu wa ndege walimpa huduma nzuri. Tulipofika MOI madaktari walitushauri kwa wanaweza kumfanyia bila shida, lakini bado sikuwa na amani," Askofu Nzigilwa alieleza.

# Balozi Mongella: Azimio la Beijing litafsiriwe Kiswahili

Na Mwandishi Wetu

VIKUNDI vya wanaharakati wa wanawake nchini vimeshauriwa kutafsiri kwa Kiswahili Azimio la Mpango Kazi wa Beijing, ili kuwawezesha watu wengi kulielewa.

Tafsiri hiyo ya Kiswahili inaweza pia kutumika katika nchi jirani ambazo zimeanza mpango wa kutumia lugha hiyo, hasa baada ya mkutano wa hivi karibuni wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye Tamasha la 14 la Jinsia lililoandaliwa na TGNP Mtandao jijini Dar es Salaam juzi, balozi, mwanasiasa, mwana diplomasia, na mwanaharakati aliyeongoza Mkutano wa Nne wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake huko Beijing mwaka 1995, Getrude Mongella, alisema tamko hilo ni muhimu katika kujenga usawa wa kijinsia.

"Azimio la Mpango Kazi la Beijing linazungumzia kwa undani jinsi ya kuendeleza harakati za kumkomboa mwanawake. Kukiwa na toleo la Kiswahili watu wengi zaidi wataweza kulielewa na kulitekeleza," alisema.

Wakati Tanzania inapambana kupata uchumi wa viwanda, alisema Balozi Mongella, vijana zaidi wanapaswa kuelewa mada ya tamasha la jinsia la mwaka huu lenye mada isemayo "Wanaharakati wa jinsia katika harakati za kuubadilisha ulimwengu." Balozi Mongella aliwataka wanawake kuandaa manifesto (ulani) yao mapema kabla ya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu, ili waweze kuutekeleza baada ya uchaguzi.

Azimio la Mpango Kazi wa Beijing linabeba mada kuhusu uwezeshaji wa wanawake ili kuondoa vizuizi vyote vya ushiriki wao katika nyanja zote za maisha.

Hii inafanywa kupitia kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika maamuzi ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa.

Kanuni ya nguvu ya pamoja na uwajibikaji inapaswa kuanzishwa kati ya wanawake na wanaume majumbani, mahali pa kazi, na katika jamii pana ya kitaifa na kimataifa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, alisema nguvu ya wanawake inapaswa kudhihirishwa katika umoja na mshikamano wao.

Aliwahimiza wanaharakati wa kijinsia kufanya kazi pamoja kama timu na waepuke masuala yanayowatenganisha kama ukabila, dini na siasa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (katikati), akizungumza na Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema (wa pili kulia), baada ya kumaliza ziara yake ya siku moja kwenye bandari hiyo. Kushoto ni Dk. Ruth Rugwisha, Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira NEMC. **MPIGAPICHA WETU**

# Siku 14 za Simbachawene mifuko mbadala kuwekwa nembo

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, ametoa siku 14 kwa watengenezaji na wasambazaji wa mifuko mbadala hapa nchini kuhakikisha mifuko hiyo inakidhi vigezo vyote stahiki ikiwamo uwekaji wa nembo ya mmiliki au kampuni.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara Bandari ya Dar es Salaam, Simbachawene alisema uwapo wa wazalishaji wa mifuko mbadala ambao hawakidhi vigezo na masharti yaliyoweka na mamlaka husika inasababisha wazalishaji wa ndani kukosa soko na kupoteza mapato la serikali.

"Ni lazima tujue nani anazalisha na kusambaza mifuko hii mbadala, hawa wanaozalisha ndani na kufuata taratibu zote wanakosa soko kwa sababu ya wengine wanaofanya biashara hii kiholela bila kufuata taratibu." alisema Waziri Simbachawene.

Mbali ya agizo hilo, alisema baada ya muda kufika msako mkali utafanyika na kwa yeyote atakayekutwa akizalisha au kuuza mifuko mbadala isiyofikia na vigezo vilivyowekwa na mamlaka husika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo pia kuchomwa kwa mifuko hiyo.

Aidha, Simbachawene aliagiza watumishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kitengo cha ukaguzi bandarini kufanya kazi saa 24 wakishirikiana na watumishi kutoka taasisi nyingine za serikali ili kuongeza nguvu kazi katika suala zima la ukaguzi wa mizigo inayoingia nchini.

"Ufanisi wa bandari upo kwenye utoaji na uingizaji wa mizigo ndani na nje ya nchi. Ikibidi nguvu kazi iongezeke ila wale wenye taaluma zinazoendana na kazi hii ili ifanyike kwa haraka na uhakika," aliongeza waziri.

Aliongeza kuwa kanuni zimebainisha wazi kuwa mtu yeyote anayeingiza nchini, anayesafirisha nje ya nchi au anayezalisha vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiwa na kanuni hizi, anatakiwa kuhakikisha kwamba vifungashio hivyo vinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Tumejipanga kuhakikisha kuwa biashara hizi za ujanja ujanja zinatokomezwa. Wakati umefika kwa Watanzania kufanya kazi halali na kuzingatia sheria," alisema na kuzitaka mamlaka husika kuongeza ushirikiano zaidi.

## Watendaji wa kata wafundwa

Na Christina Haule, KILOSA

MKUU wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Adam Mgowi, amewataka watendaji wa kata wilayani humo kutambua kuwa wao ndio wakurugenzi kwenye kata zao na wanapaswa kufanya kazi zenye kuleta mafanikio hasa kwenye sekta ya elimu.

Akifungua kikao cha watendaji wa wilaya hiyo kilichoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na masuala ya kuelimisha jamii lijulikanalo kama Dira lililoendesha mradi elimu unaofadhili na The Foundation For Civil Society (FCS), mkuu huyo wa wilaya alisema, watendaji wa kata ndio wasimamizi wa rasilimali za umma zinazotolewa kwa ajili ya kuhakikisha elimu bora inapatikana shuleni na kuona wanafanikiwa kiwilaya na hatimaye kimkoa.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema watendaji kata wanatakiwa kusimamia vyema mambo yanayotolea na serikali ikiwamo rasilimali fedha, mali na watu na kuhakikisha kila jambo linatimia kwa wakati uliopangwa.

Aidha, aliwaasa viongozi waliopo kwenye ngazi za vijiji, kata na wilaya kutoa ushirikiano utakaosaidia watendaji kuhakikisha serikali, walimu na wazazi wanafanya kazi vyema yenye kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya elimu.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka watendaji hao wa kata kuhakikisha wanasimamia rasilimali za umma ikiwamo madawati shule na kuona yanakuwa kwenye ubora muda mrefu tofauti na ilivyo kwa sasa madawati hutengenezwa na kuharibika mapema kwa kukosa uangalizi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mwambambale Asajile Lukas, aliishukuru Dira kwa kuendelea kutoa elimu kwenye sekta ya elimu wilayani humo na kusema kuwa Dira wamekuwa wakitoa elimu ya PETS katika sekta ya elimu upande wa sekondari na wameona manufaa yake na kwamba wanategemea matokeo mazuri pia katika elimu ya msingi.

# Kahawa magendo yanaswa ikienda Uganda

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera limekamata kahawa zilizokobolewa gunia 115 zikiwa zinasafirishwa bila kibali (magendo) kwenda Uganda kupitia mwalo wa Bilolo Kata ya Kemondo katika Ziwa Victoria.

Mkuu wa polisi wilayani humo, Babu Sanare, alisema Jumanne majira ya usiku gari namba T.205DHX aina ya Fuso Mistubish lilikamatwa na askari waliokuwa doria maeneo ya kijiji cha Bulila Kata ya Kemondo.

Aidha, Sanare alisema baada ya kukamata gari hilo lililokuwa limetelekezwa na dereva askari G.9158 PC Joseph, aliendesha gari na kukamata watu wakiwa na mzigo huo.

"Askari wetu waliokuwa doria miongoni mwao G.9158PC Joseph walipatiwa taarifa na kufuatilia gari hilo na kukuta ukweli, na dereva alikimbia na yeye kuendesha gari na kuleta watuhumiwa hapa kituoni," alisema Sanare.

Sanare alisema watuhumiwa hao ni Sadick Charles, Jonizius Gerald, Lazaro Mdesa, na kwamba walifanyiwa mahojiano baada ya kufikishwa kituo cha polisi.

Alisema juhudi za kupata ukweli wa mzigo huo zinaendelea pamoja na kumtafuta dereva wa gari hilo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Deodatus Kinawilo, alisema wananchi wamekuwa na tabia za kujipatia pesa kwa njia isiyo halali na kuikosesha serikali mapato.

Kinawilo alisema amekuwa akipokea taarifa za kutumia Ziwa Victoria kufanya magendo kwani kufanya hivyo haisaidii katika kufanya biashara.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (wa kwanza kulia), akijadili jambo na wageni kutoka Slovakia baada ya kuwasilisha mada kuhusu nia yao ya kuwekeza kwenye mradi wa kutengeneza mbolea jijini Dodoma juzi. **PICHA: WMU**

# Kiwanda cha mbolea kunufaisha wafugaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI nchini mbioni kunufaika baada ya wawekezaji kuja na nia ya kuwekeza kwenye mradi utakaohitaji malighafi kutoka kwenye mifugo zikiwamo kwato, pembe, kinyesi na manyoya ambazo zitakuwa zikinunuliwa kama malighafi nyingine ili kutumika kwenye kiwanda cha kutengenezea mbolea.

Lengo la serikali ni kuendelea kufungua milango kwa wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo sekta ya mifugo nchini. Miradi kama hii itasaidia kuhamasisha wananchi kuendelea kufuga kwa wingi na kwa tija baada ya kuona fursa za uwekezaji zikiongezeka.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, wakati akiwakaribisha wawekezaji wa kampuni ya Rokosan inayojihusisha na utengenezaji wa mbolea kwa kutumia malighafi zitokanazo na mifugo kutoka Jamhuri ya Watu wa Slovakia kwenye makao makuu ya wizara hiyo jijini Dodoma.

Alisema wawekezaji walio tayari kuwekeza wanakaribishwa na wizara inawaahidi ushirikiano wa hali ya juu kwenye sekta ya mifugo kwa ajili ya kuinua hali za wafugaji wetu hapa nchini, kuongeza ajira, pia kuongeza ukusanyaji wa kodi kupitia bidhaa mbalimbali zikiwamo zitokazo na viwanda.

Katibu Mkuu alisema viongozi wa serikali wanahitaji uwekezaji wenye matokeo ya haraka na yenye tija kwa taifa ndio maana wizara yake iko tayari kutoa ushirikiano pale mwekezaji anapoonyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya mifugo nchini.

Aidha, Katibu Mkuu aliwahakikishia kuwa Tanzania ni mahali salama na sahihi kwa uwekezaji huo kutokana na rasilimali kubwa ya mifugo iliyopo nchini ambapo idadi ya ng'ombe ni takribani milioni.32.2 mbuzi milioni 20, kondoo 5.5, kuku milioni 79.1 na punda zaidi ya 600,000.

Prof. Gabiel aliongeza kuwa uwekezaji huo nchini Tanzania utakuwa na manufaa sio kwa Watanzania tu bali hata kwa wawekezaji wenyewe kwa kuwa soko la bidhaa la ndani ya nchi ni kubwa, Afrika ya Mashariki pia lipo, bila kusahau nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Akizungumzia mradi huo wa kiwanda cha kutengeneza mbolea kwa kutumia malighafi zitokanazo na mifugo, Prof. Gabiel alisema itakuwa ni faraja kwa wadau wa sekta kuona hakuna kinachotupwa kutoka kwenye mifugo bali kinaongezewa thamani na kuwa bidhaa.

Aliongeza kuwa hata kwenye Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini (TLMP) umeelekeza jinsi mnyororo wa kuongeza thamani malighafi zitokanazo na mifugo zitakavyoleta tija kuelekea uchumi wa viwanda nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Rokosan, Dk. Stefan Szoke, alishukuru kwa mwitikio wa serikali wa kuonyesha ushirikiano katika hatua za awali za uwekezaji wa mradi huo.

Alisema baada ya kufuatilia masuala ya uwekezaji waligundua kuwa Tanzania ni nchi yenye fursa kubwa za uwekezaji kutokana na rasilimali na mazingira mazuri yaliyopo katika sekta ya mifugo na kusisitiza kuwa nia yao ni kuanzisha miradi yenye manufaa kwa haraka baada ya kukamilisha taratibu husika.

Akitolea mfano nchi za Ulaya ambako pia wamewekeza miradi ya aina hiyo, Dk. Szoke alisema licha ya wafugaji kunufaika kwa kuuza malighafi hizo zitokanazo na mifugo, wakulima nao wamekuwa wakinufaika kwa kupata mbolea yenye ubora na kwa gharama nafuu.

# Mila, desturi zatajwa kikwazo ndoa utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UTAMADUNI wa kuendekeza mila na desturi kandamizi ambazo zilishapitwa na wakati kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, umetajwa kuendelea kuwa kikwazo katika kutokomeza tatizo la mimba na ndoa za utotoni mkoani humo.

Takwimu za kitaifa za mwaka (2012) zinaonyesha Mkoa wa Shinyanga unaongoza Tanzania kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora 58, tatu ni Mara 55, ambapo watoto wamekuwa wakiolewa chini ya umri wa miaka 18.

Hayo yalizungumzwa juzi na mzee wa kimila Ngassa Maganga kutoka Kata ya Mwamala Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo wazee wa kimila, watu maarufu na viongozi wa dini kuhusu namna ya kutokomeza matukio ya ukatili zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Alisema ili tatizo hilo la mimba na ndoa za utotoni lipate kutokomea mkoani Shinyanga na kubaki kuwa historia, ni lazima elimu zaidi ipate kutolewa kwa wananchi hasa wa maeneo ya vijijini, kuachana na tabia ya kuendekeza mila na desturi kandamizi zilizopitwa na wakati za kutopenda kumsomesha mtoto wa kike.

"Tatizo ambalo linaonekana kuwa kikwazo katika kutokomeza mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga, ni jamii bado inaendekeza tamaduni ya mila na desturi kandamizi ambazo zilishapitwa na wakati za kutopenda kusomesha watoto wa kike na kuwaona kama vitega uchumi cha familia katika kuwapatia mali hasa mifugo," alisema Maganga.

"Nina imani kabisa elimu ikitolewa ipasavyo ya kuachana na mila hizi kandamizi, suala la mimba na ndoa za utotoni mkoani hapa litabaki kuwa historia, mimi mwenye baada ya kupata elimu vizuri na kutambua umuhimu wa elimu watoto wangu wote wa kike nimewapeleka shule wengine wapo chuo," aliongeza.

Naye Ofisa Mradi wa Utu wa Msichana kutoka Shirika la Agape mkoani Shinyanga ambao wanajishughulisha na kutetea haki za wanawake na watoto, Sophia Rwazo, alisema wametoa mafunzo kwa wazee hao wa mila, maarufu na viongozi wa dini ambapo watakuwa mabalozi wazuri kwa kupinga vitendo hivyo vya kikatili.

Alisema mradi huo wa Utu wa Msichana, utadumu ndani ya mwaka mmoja kwenye kata ambao unafadhiliwa na Shirika la Mundo Cooperate la nchini Hispania, ambalo linajihusisha na kutetea haki za binadamu, lengo likiwa ni kutokomeza vitendo vya ukatili zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

# Wapewa angalizo kuhusu mabinti

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAFUGAJI wilayani Longido mkoani Arusha wamehamasishwa kusomesha watoto na kuachana na mila na desturi potofu za kuwaozesha mabinti wadogo.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Tawala Wilaya ya Longido, Malack Tateni, wakati akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kitabu cha 'Tanzania ya Sasa' uliofanyika wilayani humo.

Kitabu hicho kimeandikwa na Mwalimu Grace Sarakikya.

Tateni alisema kuwa wilaya hiyo ni ya kifugaji na suala la mwamko wa elimu ndiyo linaanza kuonekana sasa kutokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa za kuhamasisha jamii hiyo kuwekeza katika elimu ya watoto wao bila kubagua mtoto wa kike au wa kiume.

"Hata hivyo tunaendelea na tunahitaji kuhamasisha jamii hii kubadilika sasa na kuchangamkia fursa ya elimu bure inayotolewa na serikali, kwa kupeleka watoto shuleni kwa wingi na kupata wasomi wengi zaidi," alisema.

Alisema ili hilo lifanikiwe ni lazima pia waachane na mila na desturi za ukandamiza.

Malack alimpongeza mwalimu huyo kwa kuamua kuja na kitabu hicho, ambacho kinaelezea kazi alizofanya Rais John Magufuli kwa kipindi cha miaka mitatu, ili kila mmoja ajue, hususani kwa wananchi waliopo vijijini ambapo si redio wala televisheni haziwafikii.

Alisema kupitia kitabu hicho wataona mambo makubwa yanayofanywa na Rais Magufuli.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kitabu hicho, Mwalimu Sarakikya alisema kuwa, lengo la kuandika kitabu Tanzania ya Sasa ni kutokana na kuwapo kwa majadiliano hasi kuhusu serikali ya awamu ya tano kwa miongoni mwa watu.

Alitaja baadhi ya changamoto inayomkabili kuwa ni pamoja na kukosa fedha kwani lengo la kuandika kitabu hicho ni kuwafikia Watanzania waliopo kila kona ya nchi ili watambue mambo ambayo Rais ameyafanya.

"Hivyo naomba mchango wa Sh. 1,000,000 nitoe nakala za vitabu vya kutosha kwa ajili ya kuvisambaza kwa Watanzania wengi," alisema Sarakikiya.

Kwa upande wa Ofisa Biashara Wilaya ya Longido, Paulo Parmeti, alisema kuwa, kitendo kilichofanywa na mwalimu huyo ni kuwapa fursa wanajamii wa Longido kutambua umuhimu wa elimu, kwani wengi wao hawatambui umuhimu wake hasa kuwasomesha watoto wa kike.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (mwenye Tshirt nyeupe), akibadilishana mawazo na wakazi wa Kata ya Tambukareli, katika Manispaa ya Tabora jana, wakati wa kampeni ya kufichua wahalifu katika maeneo mbalimbali mkoani humo. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Mawakala waomba mkono wa serikali

**Woinde Shizza**, ARUSHA

CHAMA cha mawakala wa pembejeo za kilimo na mifugo mkoani Arusha, kimeomba serikali kuwashirikisha katika mchakato wa upangaji wa bei elekezi za mbolea, ili waondokane na ukubwa wa bei unaowapa changamoto wakati wa uuzaji.

Aidha, wameiomba kuangalia namna ya kuwapunguzia gharama za leseni na kodi ya mapato, kwani biashara wanayoifanya ina sura ya kutoa huduma zaidi kuliko biashara.

Akizungumza katika mkutano wa wanachama uliofanyika jijini hapa, mwenyekiti wa chama cha mawakala wa pembejeo za kilimo na mifugo (Araafarma), Titus Rweyemamu, alisema bei kubwa za mbolea ambazo zinapangwa zinawaumiza kwani wateja wengi ambao ni wakulima wanashindwa kuzimudu.

Alishauri, serikali kabla ya kupanga bei hizo iwashirikishe katika mchakato wa upangaji wa bei, kwani wao ndiyo wanafahamu wateja wao wapo maeneo gani na wana uwezo kiasi gani wakumudu bei za pembejeo za kilimo na mifugo.

"Ni imani yetu kuwa tutashirikiana vizuri na serikali kufanikisha lengo la kuhudumia wakulima, ili kufikia malengo yao ya uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kiwango cha juu na hii inawezekana ," alisema. Iwapo watashirikishwa watatoa huduma bora kwa wakulima ambao ni wateja wao, aliongeza Katibu wa chama hicho Humphery Mswia.

Mswia alisema lengo la kukutana pamoja kwenye mkutano huo ni kupitia rasimu ya katiba ya chama hicho, ili kudumisha ushirikiano wa mawakala wote wa pembejeo mkoani hapa.

Aidha, ni kuwakumbusha umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kutoa huduma bora kwa wakulima ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

Alisema, wataendelea kufanya utafiti wa matumizi bora ya pembejeo, dawa na masoko, pia kufanya utetezi na ushawishi kwa wakulima na mawakala wa pembejeo za kilimo na mifugo, pamoja na kutoa elimu ya kuhifadhi na kuendeleza ma ingira kwa wanachama na jamii nzima kwa ujumla.

Ofisa Mipango Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Moses Mabula, alisema serikali itawasaidia bega kwa bega, kuwapa huduma bora wakulima na wafugaji, ili waweze kulima mazao yenye tija pamoja kufuga kisasa.

Alisema lengo la serikali ni kuwafikia wananchi wake ili wapate elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na kuwatafutia wataalamu ambao watawapa mafunzo, ili na wao pia waweze kuwaelimisha wakulima na wafugaji.

"Serikali ipo pamoja nanyi na itashughulikia changamoto zote mlizosema na kuzimaliza kwa ajili ya maslahi ya wananchi wake," alisisitiza.

# Wachimbaji tanzanite wapewa mbinu mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

WACHIMBAJI wa madini ya tanzanite wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuchangamkia fursa ya mfumo mpya wa fedha wa sarafu ya kimtandao.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Addscoin Tanzania Limited, Japhet Raphael, akizungumza jana na wamiliki na wachimbaji hao wa Mirerani, alisema hivi sasa dunia imebadilika, hivyo jamii inapaswa kuchangamkia teknolojia hiyo.

Raphael alisema wachimbaji hao wanashauriwa kuwekeza fedha kwenye mfumo huo, ili kuendana na teknolojia hiyo mpya ya fedha ambayo inatumika dunia nzima.

"Mfumo wetu wa bitcoin wa kampuni ya Addscoin Tanzania, unaweza kuwekeza kuanzia Sh. 200,000 hadi Sh. bilioni 50 na kujipatia faida kwa kila siku hivyo ni fursa nzuri," alisema Raphael.

Meneja wa Addscoin Tanzania, Kanda ya Kaskazini, Amenye Mwakisambwe, alisema wanafanya kazi kwenye mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

"Tunawawezesha watu kumiliki bitcoin kwa kununua vifurushi vyake, hivyo wachimbaji wa madini wanapaswa kuchangamkia fursa hii," alisema Mwakisambwe.

Hata hivyo, baadhi ya wamiliki na wachimbaji hao walisema hawana elimu zaidi na wanahitaji kuelimishwa kuhusu kujiunga na mfumo huo.

Mmoja kati ya wachimbaji hao Samuel Lugemalila, alisema wanapaswa kuelimishwa zaidi kuhusu suala hilo, kwani baadhi ya kampuni zilifanya utapelibaada ya watu kuwekeza.

Mchimbaji mwingine Salum Ngoya alisema ametambua kuwa taasisi hiyo inatumia mfumo wa bitcoin ambao upo sawa na mitandao ya fedha inayotumika kwenye simu za mikononi.

Mmoja kati ya mameneja wa migodi, Zephania Joseph, alisema ameuelewa utaratibu huo japo hajafahamu uwekezaji unavyoanza kufanyika.

Mmiliki mwingine, Abubakary Madiwa, alisema taasisi hiyo inapaswa kuwa na nyaraka za benki kuu, ili watu waiamini zaidi na kuondokana na fikra potofu ya kutapeliwa.

# Msimamizi uchaguzi Hai atangazwa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKATI vyama vya siasa nchini vikijiandaa kutifuana katika uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, imemtangaza rasmi msimamizi wa uchaguzi huo kuwa ni Juma Masatu.

Uchaguzi huo unachukuliwa kama kipimo cha nani anakubalika kuelekea uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020, kati ya vyama viwili hasimu ambavyo ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Masatu alitangazwa jana, wakati wa kikao cha wadau wa uchaguzi wilayani humo ambacho kililenga kumkutanisha msimamizi huyo mpya na viongozi wa vyama vya siasa.

Katika kikao hicho, Masatu aliwataka watakaopata nafasi ya kuchaguliwa kuwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kuwa waadilifu na waaminifu, pindi watakapokuwa wanasimamia uchaguzi huo ili kwenda na taratibu na sheria zilizowekwa.

Akifungua kikao hicho, Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella, alitoa rai kwa viongozi wa dini kufanya makongamano ya maombi kuombea uchaguzi huo wa serikali za mitaa kufanyika kwa amani.

Kwa mujibu wa Wella, ni vyema sasa viongozi wa kisiasa na wa kidini wakashirikiana katika kuwaandaa wananchi kuelekea katika uchaguzi huo ikiwa ni pamoja na kuhimiza zaidi amani na umuhimu wa kuwachagua viongozi hao kwani ni haki yao kikatiba.

Mei mwaka huu, Mahakama Kuu ya Tanzania ilipiga marufuku wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya nchini kusimamia uchaguzi, baada ya mahakama kufuta sheria iliyokuwa inawapa wakurugenzi hao mamlaka ya kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Uamuzi huo utailazimisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuteua watu wake, badala ya kutegemea wateule hao wa Rais, iwapo hautabadilishwa na Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

Katika uamuzi wake, Mahakama Kuu ilisema vifungu 7(1), kinachowapa wakurugenzi mamlaka ya kusimamia uchaguzi, na 7(3) vya Sheria ya Uchaguzi vinakwenda kinyume na matakwa ya kikatiba ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi.

# Vyama vya ushirika 800 vyapata hati chafu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VYAMA vya ushirika zaidi ya 800 nchini vikiwamo vinavyosimamia ushirika wa mazao, vinadaiwa kupata hati chafu kutokana na usimamizi mbovu.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Said Sife, amesema zimo pia sababu nyingine zilizochangia jambo hilo kama ubadhirifu wa fedha za wanachama.

Prof. Sife alikuwa akizungumza na mameneja wa vyama vya ushirika wa mazao (Amcos) kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika cha mkoa wa Simiyu.

Sababu hizo ndizo zinazotajwa kusababisha vyama hivyo kupata hasara ya mabilioni ya shilingi na kuyumba baada ya kushindwa kujiendesha.

"Bado hali ya vyama vya ushirika nchini siyo ya kuridhisha na niwaambie tu ndugu zangu kwamba kuna haja ya kuanza kutoa elimu kwenye vyama vya ushirika kuhusu umuhimu wa kuajiri wataalamu wa ushirika.

Zaidi alieleza: "Lakini tunapaswa kuhakikisha wanachama wanazijua sheria na sera za uendeshaji wa vyama vya ushirika ili kuboresha utendaji wa vyama hivyo kwa maslahi mapana ya wakulima na taifa kwa ujumla."

Katika kikao kazi hicho cha kujengeana uwezo, Mratibu na Msimamizi wa Vyama vya Ushirika katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Beatrice Kimaro, alisema vyama vingi vya ushirika wa mazao vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo masoko na pembejeo za kilimo.

Aidha, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika, Justin Bamanyisa, alieleza ili kufikia ndoto ya sera ya Tanzania ya viwanda, kundi pekee linaloweza kuchukua watu wengi zaidi ni sekta ya ushirika.

"Nyote mnajua kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima na kama tunataka kufanikiwa katika uchumi wa kati, ni lazima kujijengea uwezo zaidi kundi hili," alisisitiza Bamanyisa.

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ni moja ya Taasisi za Elimu ya Juu za Tanzania, ambayo hivi sasa inang'ara kimataifa kutokana na kutambuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. (EAC) kwa ushindi wa kuwa Centers of Excellence (kituo cha umahiri) cha mafunzo ya ushirika na biashara.



Ofisa mradi wa Utu wa Msichana kutoka Shirika la Agape, linajishughulisha na kutetea haki za wanawake na watoto, Sophia Rwazo, akitoa mafunzo kwa wazee wa kimila, maarufu, viongozi wa kidini na wakunga kutoka Kata ya Mwamala, Shinyanga Vijijini juzi, kuhusu namna ya kutokomeza vitendo vya ukatili zikiwamo mimba na ndoa za utotoni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Warioba akerwa makundi ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, ameeleza nia ya serikali ya kuendelea kuzisihi jamii za wafugaji kupunguza makundi makubwa ya mifugo yao na kufuga kisasa ni kutaka kuwaandaa kuzalisha kwa tija.

Alisema uzalishaji wenye tija, utazisaidia jamii hizo za kifugaji kuzalisha pia kulingana na mahitaji ya soko.

Warioba alitoa rai hiyo wakati akizungumza na jamii hiyo ya wafugaji waishio katika Kijiji cha Msarikie, Wilaya ya Moshi.

"Nataka niwaeleze ukweli na mimi ni mkweli siku zote, punguzeni kufuga makundi makubwa ya ng'ombe na mbuzi, badala yake fugeni mifugo michache yenye tija ili kukabiliana na tatizo la malisho lililopo maeneo mengi hivi sasa.

"Iko wazi kwamba ufugaji usiozingatia kanuni bora za ufugaji wa kisasa, husababisha migogoro ya mara kwa mara, kati ya wafugaji na wakulima na hasa kipindi chenye ukame, uongo au kweli," alisema.

Kutokana na changamoto hiyo kutishia ukuaji wa sekta ya mifugo, Warioba alisema serikali inapambana kupatikana na kutumika kwa mbegu bora za mifugo inayotoa maziwa mengi na nyama ili kuondokana na ufugaji huo wa mazoea.

Ameeleza kwa sasa maeneo ya malisho yaliyopo hayatoshelezi, hivyo lengo la serikali ni kuwezesha wafugaji kufuga mifugo michache inayoweza kutumia eneo dogo la malisho na kupata faida.

Badala ya kufuga mifugo mingi ambayo ikifika msimu wa ukame, inakufa kwa kukosa malisho, hivyo kujikuta wakiingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro inayosababisha uvunjifu wa amani.

Isack Jumbe alisema wao hawapingani na ushauri huo na kwamba wapo tayari kutekeleza, isipokuwa wanaomba serikali kuja na mpango maalum wa elimu kwa ajili ya kuwaelimisha juu ya jambo hilo.

Katika hatua nyingine, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa TPC wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania(KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, Robson Mmanga, aliwataka vijana wa jamii la Kimasai kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii hiyo ikiwa ni pamoja na kujihusisha na kilimo cha mazao mbalimbali badala ya kutegemea ufugaji pekee.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 26, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**Watafiti wa sayansi walipowaingiza wadau wao darasa la wadudu, udongo**



Mporomoko maadili unageuza uzazi sehemu moja hadi nyingine Ukurasa 14



Ukurasa 17

**Wanasaikolojia waja na majibu ya vitambi**



# Tembo mharibifu anafuatiliwa na 'CCTV' inayorusha taarifa akitaka kuvuka mpaka

Ukurasa 18

# WMO: Joto kupitiliza, bahari zinafurika

**Mwandishi Wetu**

WAKATI kikao cha Umoja wa Mataifa, kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa duniani kinaendelea jijini New York, kuna takwimu mpya zimeshatolewa kuhusu hatari iliyoko.

Ni takwimu zilizoandaliwa na Shirika la Viwango Duniani (WMO), zikisema zimefanyia kazi ripoti na takwimu mbalimbali za dunia kwa mwaka miaka mitano tangu 2014 na kugundua kipindi cha joto kubwa zaidi duniani.

Sambamba hiyo, ndio imegundulika kuwa kipindi chenye hewa nyingi ya ukaa kutolewa duniani kwa wingi, hata shirika hilo kupendekeza juhudi za ziada kukabili kasoro hiyo kuu.

Wakati historia ikionyesha joto duniani lilipanda kwa nyuzi 1.1 tangu mwaka 1850, waraka huo wa WMO unaonyesha kati ya mwaka 2011 na 2015, joto limepanda kwa nyuzi joto 0.2.

Sababu kuu ya kufikiwa madhila hayo ni kuongezeka kwa hewa ya ukaa duniani, kwa wastani wa asilimia 20 kati ya mwaka 2015 na sasa. Pia kiwango cha bahari nako si shwari, kimeongezeka kwa wastani wa milimita 3.2 tangu mwaka 1993, huku katika ongezeko hilo, kipindi cha miaka 10 kati ya mwaka 2007 na 2016, kumeshuhudiwa ongezeko la kiwango cha bahari kwa milimita nne kila mwaka.



Ufukwe wa bahari, inayoelezwa kuendelea kufurika duniani. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Mporomoko maadili unageuza uzazi sehemu moja hadi nyingine

• Russia yawalegezea wageni • Japan mbioni kuwa ya wazee



Wanafunzi wageni walioko masomoni Russia. Milango yao ya uraia imerahisishwa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

KUNA hisia iliyoenezwa na jamii nyingi, kuwa maendeleoo yanaleta mporomoko wa maadili na kuipeleka dunia kufikia 'mwisho,' kwani mazingira ya kijamiii yanakuwa hayakaliki.

Shida kuu inatajwa kwamba kuna watu wasio tayari kutimiza majukumu yao pasipo shuruti za kimaisha. Ni eneo linaloiingiza dunia katika matatizo makubwa ya kimazingira, yaani uzazi na malezi nje ya mazingira ya kimaumbile, mwisho wake ni hatari ya maisha.

Eneo la kwanza ni mporomoko wa maadili, kupauka kwa ndoa za asili na uhusiano huria, huku kukiwapo uwazi wa jamii na watoto kujua kila kitu wangali wadogo.

> **"Ina maana, wengi wataamua kubaki huko, kuunda familia na kusaidia kuiimarisha nchi hiyo.**

Hilo likiangaliwa kwa karibu, ni masuala yanayotegemeana; watoto kutojua mengi hadi umri mkubwa kumewajengea tabia ya woga, ikiendana na ilivyo mamlaka ya mzazi kwa mtoto.

Jambo la pili, mkuu wa jadi alikuwa na mamlaka kwa kila mtu katika jamii , ikiwamo kumfukuza kijijini hapo mtu anayeaminikika kuwa ni 'mchawi' kwani yalileta visasi vya ukoo.

Kupungua nguvu za mamlaka za jadi, kijamii na familia, zimeleta hicho kinachoitwa 'mporomoko wa maadili' na hakuna nyenzo katika uhusiano wa jadi au zuio la sasa.

Hapo ndiko kunazuka swali la hali ya baadaye kijamii, kama italeta mvurugano wa moja kwa moja au upenyo kimaadili, ambao labda 'hautiliwi maanani vya kutosha' katika misemo ya kawaida.

Moja ya maeneo chanya ya suala hilo ni malezi katika elimu na makuzi, ambako wanajadili jinsi ya kumlea mtoto kimaadili, iwe kumuonya kwa kumshauri kama wataalamu wanavyosema au kwa kumuadhibu kama inavyofahamika katika jadi.

**ADHABU VS USUGU**

Hivi sasa, hata adhabu za kikatili za jadi za kumpiga mtoto viboko hadi aishiwe nguvu, hazipo tena. Kuna suala la ziada linalozua swali, je adhabu inajenga usugu?

Ni swali gumu kulipatia majibu, kwani katika baadhi ya nyumba, kuna eneo la ziada, katika nyumba nyingi hasa za mijini, hata vijijini msimu wa kilimo, wazazi wote wawili wanaondoka asubuhi na wanarudi jioni au hata usiku.

Ni mazingira ambayo watoto wanalelewa na wasichana wa kazi ya wasidizi wengineo na wanajifunza takriban kila kitu kutoka kwao na katika mazingira ya karibu yaani hakuna kilichofichika.

Hapo ina maana kwamba, pale kila kitu kinajulikana hakuna woga wa kuingia katika uhusiano na kuchukulia maisha kama upenyo, hali inayoleta ulazima wa kupata fedha kwa njia yoyote na kupangua nidhamu ya kufaulu.

Kuangalia jinsi mazingira hayo yalivyo au yanavyotatuliwa, kwanza ni kuangalia tatizo la mporomoko wa maadili lilivyojidhihirisha katika jamii tofauti duniani. Ni njia gani zinaweza 'kutoka' katika suala hilo? Kwa jumla siyo rahisi kubashiri ufaulu wake.

**MTIHANI ULIVYO**

Katika baadhi ya nchi zilizoendelea, kuna kanuni au maadili ya ndoa yanafuatwa kwa kina, ambazo suala la kuzaa ni gumu na nyumba nyingi zina mtoto mmoja na siyo rahisi kukuta penye watoto zaidi ya wawili.

Ushuhuda dhahiri ni katika nchi za Mashariki ya Mbali, kuvunja ndoa ni mara chache zaidi ya nchi za Magharibi, lakini bado kuna watoto wachache zaidi.

Pia, nchi za Mashariki zina uthabiti wa kiasi fulani katika maadili, ila uadilifu wao katika uzazi na kulea sasa umepungua

Ni ukanda usio na ukiukwaji dhidi ya uadilifu wa ndoa na kuna viwango vidogo zaidi vya ushoga, ukilinganisha na nchi za Magharibi, kama Bara Ulaya na Marekani.

Inafafanuliwa, watoto wanaozaliwa ukanda wa Mashariki ya Mbali wana msingi bora zaidi wa maadili na ari ya kufaulu katika maisha, ila wapo wachache zaidi.

Mataifa kama Japan, Russia na China yanakabliwa na 'mdudu'wa jamii kuzeeka kwa kasi.

AFYA

# Mporomoko maadili unageuza uzazi sehemu moja hadi nyingine

**WAZEE, KUCHANGANYA DAMU**

Nchini Japan, kunakadiriwa ifikapo mwaka 2030, ambao ni miaka 11 ijayo, theluthi mbili ya wakazi wake tu watakuwa na miaka 60 au zaidi, hivyo Japan itakuwa nchi yenye wazee zaidi na nguvu kazi haba.

Hivi sasa nchi hiyo imeanza kufungua milango ya wageni kuingia kukaa kwa matumaini ya kuongeza idadi ya watu, hatua ambayo haikuwa rahisi zamani kutokana na ukiritimba wa jadi katika nchi hizo.

Nchini Russia hivi karibuni, kuna agizo la utawala wa Rais Vladimir Putin, kwamba wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali wanaofanya masomo ya muda mrefu, wapewe haki ya uraia, kwa mfano baada ya miaka mitano badala ya 10, ilivyokuwa nchi nyingi za Ulaya.

Ina maana, wengi wataamua kubaki huko, kuunda familia na kusaidia kuiimarisha nchi hiyo.

Kuparaganyika kwa eneo lote la Mashariki ya Kati katika miaka ya karibuni, kumekuwa chachu ya jinsi nchi za Ulaya Magharibi zinavyorekebisha kwa hatua na mlingano hasi wa kidemografia, yaani hali ya kupungua uzazi na nguvukazi inakosekana katika maeneo mengi.

Wimbi la kwanza la 'Uamsho Arabuni' kuanzia mwaka 2011, Ujerumani kwa iliingiza wahamiaji zaidi ya 300,000 kwa mwaka, kisha vyama vya kizalendo vikajijenga upya kutaka Ulaya ya Kikristo ya Wazungu na siyo ya Kiislamu. Mkondo wa uhamiaji umepungua na hatari ya ugaidi inafifia, wahamiaji wataongezeka.

Hivi karibuni imebainika ifikapo mwaka 2030, nusu ya maskini au mafukara duniani watakuwa watoto wa Afrika.

Ni kielelezo cha mporomoko wa maadili wa kina zaidi, ukilinganisha na Ulaya, ambako kuna tahadhari ya uzazi, licha ya uhusiano wa kimapenzi yako huru zaidi kwa kijana kila anayefikia umri miaka 18 na suala la kuzaliana ni adimu.

Lakini Afrika, binti anapoingia mtaaani au shule, uwezekano wa mimba ni mkubwa. Hiyo iko huku, mitaji inahamia Afrika kwa wingi kutoka Asia ya Mbali na Ulaya, ambako masoko yao yanapanuka kwa kasi, nguvu kazi nayo inaendelea kuwa nyngi kwa bei rahisi.

Kimsingi, uhamiaji wa watu kutoka eneo moja la dunia kwenda jingine, ni suluhu ya kuporomoka maadilii ya kuzaa na kulea, wakati umaskini barani |Afrika unasukuma wengi kuhamia ng'ambo, wakifika huko wanakuwa na azma halisi ya kufaulu.

Nyumbani wanabweteka, wanaanza tabia mbaya kwa kuwa wana uhakika wa wazazi na ndugu wengine, kimyume na ugenini, wanafaulu kuliko wenyeji na ndiyo sababu ya kuwindwa na Wazulu 'walioporomoka kimaadili' Afrika Kusini, waliokuzwa kujiamini kuwa "wao ni taifa bora' la wapiganaji na wake wengi."

Maporomoko ya maadili yanabadili urithi wa nchi kutoka taifa moja kwenda jingine. Hivyo,wageni wanachukua nafasi zao ndani ya nchi, jamii au kaya zinafaulu kuwa na vinasaba vya upole na upendo na watoto wanaosikiliza maonyo waache mbaya na kulenga kufaulu shuleni na maishani, ndiyo 'wanairithi nchi.'

Hii inajenga kizazi cha familia thabiti zenye madili, watoto wanasoma na kuunda familia mpya, wakizingatia maadili; wanaoshindwa maadili waishie kwenye pombe, kizazi kife.



Wazee wa nchini Japan. **PICHA ZOTE:MTANDAO**

> **Hiyo iko huku, mitaji inahamia Afrika kwa wingi kutoka Asia ya Mbali na Ulaya, ambako masoko yao yanapanuka kwa kasi, nguvu kazi nayo inaendelea kuwa nyngi kwa bei rahisi.**



Wazee wa Kijapani wakifanya mazoezi

AFYA

CHEREKO TASAF

# Historia tangu Uhuru, wajawazito kilomita 8 kwa kitanda cha kamba

• Ilipofunguliwa tu wagonjwa 6,000 • DED achekelea, aahidi kuziba pengo



Jengo jipya la zahanati katika kijiji cha Ughaugha 'A' Wilaya ya Singida Vijijini. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA**

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa Singida**

NI kilio cha muda mrefu ambacho kimekuwa kikiwatesa wakazi wa vijiji vya Ughaugha 'A' Mwahango Wilaya ya Singida Vijijini na mkoani Singida. Shida wanayopigia kelele ni ukosefu wa kituo ambacho kinapaswa kuwakimu na dharura za kiafya.

Wakazi hao wanalazimika kutumia gharama kubwa ya kifedha kwenda mbali kufuata huduma hiyo na wakati mwingine wanapata matatizo kabla ya kuifikia huduma, kutokana na umbali uliopo.

Wapo baadhi ya wanawake wajawazito waliowahi kupoteza maisha na wengine kujifungua njiani, wakipambana katika safari ya kukifuata kituo hicho cha afya.

Japokuwa waliandaliwa mapema na wataalamu wa afya katika vituo vya karibu vinavyotoa huduma hiyo, kuhusu umuhimu wa kuwahi kufikia huduma kabla ya hatua ya mwisho ya kujifungua, lakini walishindwa.

Sababu kubwa ni kutokana na kushindwa kumudu maandalizi yanayohitaji gharama za kifedha katika kipindi cha kusubiri kujifungia.

> **Tasaf wao wamefanya kazi yao ya kuhakikisha wanawajengea wananchi zahanati na kuweka baadhi ya vifaa muhimu, kilichobaki sasa ni kwa serikali kumalizia pale wenzao walipoishia.**

Wanakijiji hao wanasema walishapiga kelele cha kuomba msaada wa kufikishiwa kituo cha afya miaka 'nenda rudi,' lakini walikuwa hawajafikishiwa.

### HATIMAYE WAITIKIWA

Baada ya kilio hicho cha muda mrefu, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) uliguswa na ombi na ukaamua kuwajengea zahanati, likiwa na mtazamo wa kuwapunguzia baadhi ya matatizo yaliyotokana na shida hiyo ya ukosefu wa kituo cha afya.

Wananchi hao wanaishukuru Tasaf kuwajengea zahanati hizo, huku wakikiri kilio chao cha muda mrefu sasa kinaelekea katika ukomo na kwa nyakati tofauti wanasema zaidi ya miaka 50 sasa, vijiji hivyo havikuwa na vituo vya afya na wao kubebeshwa usumbufu mkubwa.

Mwanakijiji wa Ughaugha 'A' Benedicto Agustino, anasema katika kipindi chote hicho walikosa kituo cha afya na kulazimika kwenda umbali zaidi ya kilomita nane kuifuata huduma.

Agustino anaeleza kuwa, iliwagharimu hata wakati mwingine wagonjwa hususani kinamama wajawazito, wana historia ya kujifungua njiani, kabla ya kufikishwa katika kituo cha afya.



Ofisa Tabibu Siaeli Tesha, akimhudumia mgonjwa katika zahanati iliyojengwa na Tasaf, kijijini Mwahango, Wilaya ya Singida Vijijini.

"Tangu kipindi cha Uhuru (mwaka 1961) hatujawahi kuwa na zahanati hapa kijijini kwetu. Huwa tunaenda katika kijiji kingine zaidi ya kilomita nane, japokuwa huko nako ni ya mtu binafsi. Kwa hiyo, unapokuwa na mgonjwa lazima utumie gharama kubwa," anasema Agustino

"Angalau kwa kinamama wajawazito unaweza kujiandaa kifedha ukawekeza 'kidogo kidogo'kwa sababu wanapohudhuria kliniki huwa wanaambiwa 'stage'(hatua) wanazokuwa wamefikia.

"Lakini ukiuguliwa ghafla, huwa inakuwa changamoto kubwa katika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kumpeleka mgonjwa hospitali hadi kufikia hatua ya kukopa," anasema

### VITANDA VYA KAMBA

Augustino anasema, kutokana na changamoto ya umbali wa vituo vya afya, kuna wakati walilazimika kutumia vitanda vya kamba wanavyovitoa majumbani mwao, kuwasafirisha wajawazito kwenda vituo hivyo vya afya.

"Hapa kwetu kijijini kutumia vitanda kubebea wagonjwa tulikuwa tunaona ni kitu cha kawaida. Kinamama wajawazito tulikuwa tunawabeba kuwapeleka wanapoumwa uchungu na wakati mwingine akizidiwa sana. Inabidi kinamama wanaziba nguo zao wanamsaidia anajifungua na sisi tunakaa pembeni," anasema Agustino

"Zamani ilikuwa ikitokea kama hivyo akijifungulia njiani, mnamrudisha nyumbani, lakini sasa wamewawekea masharti magumu. Kwa hiyo, ikitokea hata kama amejifungua njiani, lazima tumfikishe katika kituo cha afya, akachunguzwe yeye na mtoto wake," anasema.

"Tunashukuru sana Tasaf kwa sababu msaada huu wa zahanati kwetu ni zaidi ya mkombozi. Tunaona ni neema kubwa, haya matatizo yote tuliyokuwa tunayapata hatutayaona tena," anaendelea

### MUUGUZI

Muuguzi Msaidizi wa Zahanati ya Ughaugha A, Gyunda Elisha, anasema kituo hicho kilifunguliwa rasmi mnamo Mei mwaka huu na kimekuwa msaada mkubwa kwa kijijini hapo na kwa wanakijiji jirani.

"Ukitaka kufahamu kwamba kulikuwa na tatizo kubwa la huduma ya afya katika kijiji hiki, mwezi tuliofungua tulipata wagonjwa 6,000 hadi tukaishiwa dawa. Tukalazimika kwenda kuomba nyingine," anasema Elisha

Anasema changamoto iliyobaki, ni uhaba wa madaktari na wahudumu, jambo analoamini kwamba serikali italishughulikia.

"Tasaf wao wamefanya kazi yao ya kuhakikisha wanawajengea wananchi zahanati na kuweka baadhi ya vifaa muhimu, kilichobaki sasa ni kwa serikali kumalizia pale wenzao walipoishia.

"Hapa tuko wawili tu, mganga mkuu na mimi muuguzi msaidizi, uhitaji wetu hapa angalau tulipaswa tuwe na wahudumu angalau wanne au watano. Tunaamini kwamba, haya yote yatawekwa sawa, kwa sababu hata nyumba zenyewe hakuna, kwa hiyo tunalazimika kupanga mbali mitaani," anfafanua Elisha.

### DED SINGIDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Singida Vijijini, Rashid Mandoa, anakiri kufahamu tatizo la upungufu wa madaktari na wahudumu katika zahanati hiyo, pia ukosefu wa nyumba zao za kuishi, akiahidi analifanyia kazi.

"Kwanza ninawashukuru Tasaf kwa jitihada zao na kwa kutuona na sisi kutusaidia kutujengea zahanati kwenye vijiji vyetu. Wamefanya kazi kubwa na ninawaahidi kwamba changamoto ndogo ndogo zilizobaki tutazimaliza," anasema Mandoa.

"Hizo nyumba za madaktari na wahudumu tayari zimekwishawekwa katika bajeti na hata suala la kuongeza wahudumu nalo linafanyiwa kazi na litatatuliwa haraka, tunaomba watuamini," anafafanua mkurugenzi.

Mandoa anaenda mbali, kwa kuushukuru mfuko huo kusaidia vijiji vingi katika halmashauri hiyo, wakiingiza mpango na anafafanua kuna vijiji 40 kati ya 84 vya Wilaya ya Singida Vijijini vyenye kaya 7,760 vimenufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Anasema, tangu kuanza mpango huo unaosiamiwa na Tasaf mwaka 2014, kuna wanavijiji wengi waliojikwamua katika jitihada za kuongeza vipato vyao.

"Hiki wanachokifanya Tasaf ni kutoa mbegu kwa wahitaji ambao jukumu lao ni kuhakikisha mbegu hiyo inatoa mazao bora na endelevu," anasema Mandoa, akitoa ufafanuzi kwamba:

"Kwa sasa tumeanza kuona mbegu hii inazaa, kwa sababu wengi wao hivi sasa wanajishughulisha na maisha yao yameanza kuboreka, wamejiunga katika vikundi mbalimbali vya uzalishaji.

> **Tangu kuanza mpango huo unaosimamiwa na Tasaf mwaka 2014, kuna wanavijiji wengi waliojikwamua katika jitihada za kuongeza vipato vyao.**

"Ni kazi kubwa sana Tasaf inafanya na nawapongeza. Kwanza, wanawekeza kwenye rasilimaliwatu hasa eneo la afya na elimu. Hili ni jambo la mfano kwa jamii yenye kiu ya maendeleo na pili wanawekeza katika ujenzi wa uchumi wa taifa, kupitia kuondoa umasikini kwa wananchi wake."

"Kupitia ruzuku hiyo, watoto wengi wana afya, wengi hivi sasa wanapelekwa kliniki na idadi ya wanafunzi hasa wa kike pia imeongezeka shuleni," anahitimsha Mandoa.

***Kesho usikose mwendelezo wa makala ya miradi mingine ya Tasaf.***

## Wanasaikolojia waja na majibu ya vitambi

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa saikolojia wa Kiingereza, wamekuja na hoja kwamba mtu kuwa na kitambi haipaswi kuwa jambo linalomfanya ajihisi aibu muda wote.

Katika ripoti yao maalum ya kitaalamu wanasema hilo si chaguo binafsi hata kumfanya aone aibu katika maisha binafsi. Hivyo, maoni yao kwa, umma ni haja ya kubadilika lugha inayohusiana na usimamizi wa maisha ya vitambi.

Hapo wana mapendekezo ya matumizi; kama ilivyo kwa 'wenye ulemavu' na si 'walemavu' ndio vivyo hivyo iende kwa 'mtu mwenye kitambi' na si 'ana kitambi.'


Pia, wataalamu hao wana mtazamo unaokinzana na wenzao wa afya, kwamba kitambi kisitambuliwe kama ugonjwa, kwani ni tafsiri yenye maana kubwa kumbadilisha mtu kitabia.

Kingine kupitia ripoti yao ya kitaalamu, wanashauri wataalamu wa afya wafunzwe namna sahihi wanavyoweza kuzungumzia mbinu za kupunguza uzito kwa 'watu wenye vitambi.'

Nchini Uingereza kunaelezwa si salama zaidi kihistoria kuhusiana na mustakabali wa vitambi kwa jumla. Viwango vimeongezeka kwa asilimia 18 kati ya mwaka miaka 12; kati ya mwaka 2005 na 2017.

Ni takwimu zenye tafsiri ya kawaida kwamba katika kila kundi la watu wanne, kati yao mmoja ana kitambi. Pia, kunaelezwa zaidi ya asilimia 65 ya wenye uzito wa ziada mwilini, kwa wastani mmoja wao ana kitambi. Hapo ndipo Chama cha Wanasaikolojia Uingereza kinapoliona kuwa jambo tata na inafafanua kupitia ripoti yake kuwa: "Watu wanaonekana zaidi kuwa na afya duni kwa upande wa uzito wao ni ambao kijenetekia wako hatarini kuongeza vitambi."

Wanaleleza kundi lingine kwa tafsiri:"Wale ambao maisha yao yanaelekezwa



Mwenye kitambi akifurahia maisha. **PICHA : MTANDAO**

na kazi, shule na mazingira ya kijamii yanayochangia wasifanye sana kazi."

Uzoefu wa kisaikolojia unaonyesha nusu ya wazazi walio na vitambi wanapata huduma ya kukabiliana nayo hivi sasa. Wataalamu bingwa wana maoni ya kitaalamu kuwa, watu hao pia walipata shida utotoni.

Kuna dai la kitalamu kuwapo baadhi watu wanapokuwa na vitambi wanatawaliwa na aibu mbele ya jamii, ilhali bado wanaendekeza kula bila ya kanuni na mwili kuongezeka maradufu.

Mtaalamu wa vichekesho, James Corden, ana mchango wake katika hoja hiyo akitamka: "Kama vichekesho vitawafanya wanene kupunguza uzito, hakutakuwapo watoto wanene shuleni."

Mtaalamu Dk. Angel Chater, anasema wanasaikolojia wanapaswa kuwasaidia wataaluma wa afya juu ya kuwasiliana na wanaowahudumia, masuala ya vitambi.

"Kama kutibu vitambi ingekuwa jambo rahisi, basi tunsingekuwa hapa na tusingeandika ripoti hii," anasema Dk. Charter, kutoka Chuo Kikuu cha Bedfordshire, Uingereza.

"Unaweza kuwa na nafasi nzuri duniani, lakini kama huna nafasi nzuri ya kupata mlo sahihi, mazimgira bora. Maisha yako yatakuwa magumu," anaongeza.

Ushauri wa wataalamu hao uliomo katika ripoti malaum ya kitaalamu ni kwamba, iwapo serikali haitajikita vilivyo katika kukabili vitambi kama inavyofanya kwa uvutaji sigara, shida hiyo kukabili vitambi.

Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wanasaikolojia wa Uingereza, Sarb Bajwa ana maelezo:"Tumechukua hatua katika ngazi zote kwa miongo, kuanzia sera za serikali kumsaidia mtu mvutaji peke yake, hivi sasa tuanaona kupungua kiwango kikubwa cha uvutaji

"Wanasaikolojia wana ujuzi wa kisayansi na kitabibu kuwasaidia huduma za afya, wanaofanya hayo. Tunaweza kusaidia si kwa kuandaa usaidizi wa mmoja mmoja pekee, bali kupitia sera za umma inayosaidia kujenga mazingira ambayo watu watavikwepa vitambi kirahisi."

MAZINGIRA

USHUHUDA HIFADHINI THAILAND

# Tembo mharibifu anafuatiliwa inayorusha taarifa akitaka ku

• Inatajwa ni teknolojia ya kwanza duniani • Mwanakijij

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa Thailand**



Meneja Mawasiliano wa kampuni ya simu ya True Corporation Plc, Rommuk Plachom, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari na wataalamu wa uhifadhi wa Thailand na Tanzania.



Kiongozi wa ask
wanavyopokea
kupokea taarifa

NCHI za Asia zimefanikiwa kutatua migogoro baina ya wanyama na binadamu kwenye hifadhi za taifa na maeneo yaliyohifadhiwa.

Hiyo ni baada ya ushirikiano kati ya kampuni za simu, kutumia teknolojia ya kisasa ya kupiga picha tembo wanapotaka kwenda kwenye makazi ya watu na kutuma taarifa kwa askari wanyamapori.

Teknolojia hiyo ni ya kwanza kutumiwa barani Asia. Imewekwa kwenye hifadhi za taifa kwa ushirikiano kati ya Mfuko wa Kimataifa wa Kampuni za Simu na Hifadhi, katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo kwa jamii.

Waandishi wa habari walio kwenye programu maalum ya kuandika habari za kupinga ujangili wa wanyamapori, walitembelea maeneo yaliyohifadhiwa nchini Thailand, ambako ndiko njia kuu na soko la bidhaa za wanyamapori kwa Asia. Hapo, walitembelea hifadhi mbalimbali.

Programu hiyo inafadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani, Kitengo cha Uhifadhi (USAID Protect) ikishirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (Jet). Ni timu ya waandishi wa habari 10, watano wanatoka Tanzania na idadi kama hiyo wa Thailand.

Huko, waandishi walitembelea Hifadhi ya Taifa la Kuiburi, iliyopo Kusini Mashariki mwa nchi hiyo, yenye aina tano za wanyama.

Hifadhi ya Kuiburi yenye ukubwa wa mita za mraba 969, ilianzishwa mwaka 1999 katika jimbo la Prachuap Khiri Khan, eneo lenye milima ya Tenasserim, ikiwa kwenye maeneo la Pran Buri na Sam Raio Yot . Takwimu za mwaka 2017, zinaonyesha hifadhi hiyo iliitembelewa na wastani wa wageni 40,592 kwa mwaka.

### ASKARI KIONGOZI

Kiongozi wa askari wanyamapori wa Kuiburi, Panithan Pinitpuangchon, anasema kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya True Corparation Plc nchini humo, wanatumia teknolojia hiyo kujua walipo tembo na wanawarejesha hifadhini.

Anasema, ndani ya hifadhi kuna jumla ya kamera 28 na inakadiriwa kuwapo tembo 237, kati yao dume 60 na majike 168. Kwa kutumia taarifa za makao makuu ya ofisi hiyo, askari wanyamapori wenye silaha waliogawanyika katika makundi manne kuchukua hatua.

Anasema, kamera hizo zimewekwa katika umbali wa mita 500 hadi kilomita moja kutoka eneo la jamii, ili kutoa muda wa kutosha kwa

> **Baadaye tuliamua kuwa na kituo chenye vifaa vya kisasa na 'application' itakayotuma taarifa ya haraka kwenye simu za askari na kwenda moja kwa moja eneo lililoonyeshwa.**

askari kulifikia eneo husika.

Huko nyuma, mgogoro kati ya wanyama na watu ulikuwa mikubwa, kiasi cha tembo wengi kufa kutokana na kupigwa na umeme na ndipo Mfalme wa eneo hilo alipokuja na mkakati wa pamoja kuwalinda tembo hao.

### CHANZO CHA UBUNIFU

Meneja Mawasiliano wa kampuni ya simu ya True Corporation Plc, Rommuk Plachom, anasema betri za kamera hizo zina uwezo wa kukaa na chaja kwa mwezi mmoja hadi miwili.

Zinapiga picha mnato na zina uwezo wa kupiga video, lakini haitumiki kwa sababu huenda ingechukua chaja nyingi na ndiyo maana zimewekwa kwa ajili ya kupiga picha pekee.

Anasema, ni hatua ya namna ya kurejesha kwa jamii kupitia kutatua kero inayowasumbua. Walibaini wananchi wanaoishi kando mwa hifadhi wanakumbana na changamoto kubwa.

Plachom anasema, changamoto iliyopo ni ulaji na uharibifu wa mazao, pia nyumba kusambaratishwa, ikiendana na maafa, ndiyo maana ibabuniwa suluhisho la kutafuta teknolojia ya kuwafuatilia tembo wanapokaribia makazi ya watu kwa saa 24.

"Kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Uhifadhi Dunia (WWF), tumekuja na suluhisho hilo ambalo litakwenda kuondoa changamoto kwa jamii na kuimarisha ujirani mwema, pamoja na utunzaji mazingira kwa kuwafukuza tembo, kabla hawajavamia mashamba ya wananchi," anasema Plachom.

Jinsi gani kamera inafanya kazi, Palchom ansema kamera hizo zilizowekwa umbali wa mita 500 hadi kilomita moja kutoka kwenye makazi ya watu, inapiga picha umbali wa mita tano hadi sita na kuituma haraka

Anasema, wahusika wa hifadhi wanapopokea taarifa zinapopokelewa, huwatuma askari wanyamapori wa katika eneo husika, wanaowawahi tembo hao, kabla hawajafikia katika eneo la wananchi.

"Tuliamua kupitia programu ya kurejesha kwa jamii na kushirikiana na WWF. Tulifikiri namna gani tunaweza kutumia teknolojia kutambua tembo walipo na askari wanyamapori kuwarejesha hifadhini, kabla hawajasababisha madhara," anasema na kuongeza:

"Imechukua miaka miwili, kutokana na ukweli kuwa teknolojia hii haijawahi kuwapo eneo jingine duniani. Kutumia teknolojia hii inahitaji kibali cha serikali, kwa kuwa tunakwenda kuweka satelaiti kwenye hifadhi, lakini mwisho tulifikia muafaka na mwisho tulijenga mnara nje ya hifadhi."

Anasema, walifanya utafiti kwa miaka mwili na kubaini kuna tembo 25 wanaoenda kwenye mashamba ya watu kila mara, njia zao na muda, ndipo walivyofikia uamuzi kuweka kamera kwenye njia hizo.

"Ilikuwa ngumu mwanzoni, kwa kuwa tulitumia simu kwa picha kwenda kwenye simu ya askari wazichambue na kufanya maamuzi.

"Baadaye tuliamua kuwa na kituo chenye vifaa vya kisasa na 'application' itakayotuma taarifa ya haraka kwenye simu za askari na kwenda moja kwa moja eneo lililoonyeshwa," anasema.

"Tulianza na eneo la mfano na hadi Oktoba mwaka jana, tulianza rasmi na hadi sasa tuna picha zaidi ya 3,000 za tembo wanavyofukuzwa.

"Kabla walikuja mara 4,000, lakini toka ziwekwe kamera na wafukue mara kwa mara wameharibu mazao ya wanachi mara mbili kwa kupita eneo ambalo halina kamera.

Aidha, anasema kuna ongezeko la tembo wastani wa 50 kwa mwaka, ambayo takwimu hupa-

# ...a na 'CCTV' ...vuka mpaka

## ...i alipwa kilekile alichopoteza



...kari wa wanyamapori wa Kuiburi, Panithan Pinitpuangchon, akifafanua ...taarifa na kamera zinavyofanya kazi, kwenye chumba maalum cha ... hizo . **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI**



Askari wanyamapori wa Hifadhi ya Taifa ya Kui Buri, akionyesha jinsi kamera zinavyofungwa kwenye mti katika mapito ya tembo.

tikana kwa kupima vinasaba kwa kutumia kinyesi na kwamba wanaendelea kuongeza jitihada za kutumia teknolojia.

"Tumefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa teknolojia imesaidia sana na kwa sasa, askari wanajua tembo wako wapi," anasema na anaendelea:

Askari kiongozi huyo, anafafanua kwamba wamechagua kamera, kwa kuwa haiwagusi wanyama kiasi cha kuwafanya wasifurahie maisha yao, tofauti na matumizi ya nyaya za umeme

**FIDIA IKOJE?**

Kwa mujibu wa Sheria za Wanyamapori na Uhifadhi ya Thailand, mwananchi anayeharibiwa mazao yake, anafidiwa serikali mazao kwa anayemiliki ardhi kisheria.

"Kama huna hatimiliki ya ardhi, hulipwi fidia, na kinacholipwa ni mazao kwa kiasi kilichoharibiwa, kama waliharibu mti wa mwembe unapewa mti wa mwembe," anasema.

**JAMII JIRANI**

Plachom anasema, jamii inanufaika na utalii hasa nyakati ambazo siyo za mavuno, kwa kutembeza watalii kwa kutumia magari yao na kupata fedha moja kwa moja kupitia umoja wao uitwao Kuiburi Eco Tourism Club.

> **"Tanapa inasaidia miradi ya kipaumbele ya wananchi husika, inatoa asilimia 70 ya gharama za mradi wa kijiji husika katika eneo la afya, maji na elimu.**

Waongoza watalii waliozungumza na Nipashe, wanasema wameunda umoja wa jamii inayozunguka hifadhi na wanapata kipato kwa kuwa gari moja la watalii linalipa fedha Thai Baht 850 (sawa na Sh. 64,000) ambazo mgawanyo wake ni dereva Sh. 500 mwongoza watalii Sh. 170, hifadhi inapata Sh. 130 na chama kinapata Sh. 50.

Wanasema, wanafurahia kazi hiyo kwa kuwa inawaingizia kipato na kuwa sehemu ya hifadhi na kwamba wanapoona wanyama wametoka hifadhini hutoa taarifa kwa haraka na kwamba kila mwisho wa wiki makundi ya wanafunzi hutembezwa hifadhini ili kujenga moyo wa kupenda uhifadhi.

Wanasema, huduma za kijamii kama shule, miundombinu, huduma za afya na nyinginezo ni wajibu wa serikali.

**SIRI YA WANYAMA**

Tanzania ambayo kwa sasa ina utajiri wa jumla ya hifadhi za taifa 22, eneo la hifadhi ya Ngorongoro, mapori ya akiba 32, mapori tengefu 18, jumuiya za uhifadhi za jamii 38 kati yake 16 zimesajiliwa rasmi pamoja na maeneo ya wazi, kote kuna changamoto ya wanyama kufanya uharibifu kwa wananchi.

Wataalamu wanasema, tembo ana uwezo mkubwa wa kuhifadhi kumbukumbu mna uhai wake ni zaidi ya miaka 100.

Katika umri huo, huendelea kukumbuka njia alizopita na wazazi wake na nyakati za kutafuta maji na malisho huenda kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kupata mahitaji muhimu na wanapopitia, hukumbana na shughuli za kibinadamu.

Pia, tabia ya wanyama hawana mipaka kama ilivyo kwa binadamu, hupita kwenye njia yao na kutumia wanachokikuta kama kinawafaa, na ndiyo maana migogoro hutokea kama ilivyo kwa eneo la wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Tukio la karibuni ni tembo hao kutoka Hifadhi ya Mkomazi Tanga, walivamia vijiji vya kata ya Usangi na Shingatini mkoa wa Kilimajaro, walikomjeruhi mtoto.

Tukio lingine mwezi huu, ni jumla ya nyumba 39 katika vijiji vya Longaloniga, Matale na Mwasengela mkoani Simiyu, zilibomolewa na tembo waliokula mahindi yanayokadiriwa ni kiasi cha magunia 30.

**HOJA BUNGENI**

Katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni mwaka 2017/18 iliyowasilishwa na Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii, Peter Msigwa, anasema ipo migogoro inayoumu muda mrefu na kuwagharimu wananchi wengi, mkasa ukianzia kwa wanyama ambao ndio fahari ya nchi.

Anatoa mifano ya maeneo ya Wilaya ya Bunda inayopanaka na Pori la Akiba la Grumeti, katika vijiji vya Kegonga na Masanga; Ulanga katika vijiji vya Iputi na Lupilo, ambako migogoro imesababishwa na kutokana na wanyama kufanya uharibifu kwenye makazi ya watu.

Kamishna Msaidizi Willam Mwakilema wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), anasema simba tisa waliuawa huko Serengeti kwa kuwekewa sumu, baada ya wanyama hao kula mfugo wa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi.

Kamishna William, anasema kutokana na ongezeko la migogoro kati ya wananchi na hifadhi, sababu kubwa ni kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Tanapa kwa kushirikiana na wadau wameweka mpango huo kwenye vijiji jirani.

**UJIRANI MWEMA TANAPA**

Kamishina Msaidizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Godwell Ole Meing'ataki, anasema suala la ujirani mwema kwenye hifadhi za taifa ni muhimu, kuhakikisha jamii inayozunguka hifadhi inaona umuhimu wake kupitia manufaa ya jumla ya kijamii.

Anasema, uhifadhi endelevu kwa ajili ya maendeleo, unawezekana iwapo jamii itashirikishwa na kuwa sehemu ya hifadhi, ikiwamo kunufaika na huduma kama zahanati, shule maji na miradi mingine itakayotatua changamoto zao.

Tanapa, ilianzisha kupitia mpango wa Ujirani Mwema ulioanza mwaka 1988 katika vijiji vya Ololosokwan, Soitsambu na Oloipiri vilivyopakana na Hifadhi ya Taifa Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Programu hiyo ilisambaa hadi kufikia mwaka 1992 kwenye Hifadhi za Taifa za Tarangire, Ziwa Manyara na Arusha, na baadaye ilisambazwa kwenye hifadhi zote mwaka 1994 na 95.

Ole Meing'ataki anasema mbali na kupeleka miradi yenye makubaliano ya wananachi wa vijiji husika lakini wanatoa elimu ya uhifadhi kwa kutembelea shule, vikundi, kusaidia matumizi bora ya ardhi na kuanza vitalu wa miti.

Nyingine inalenga kutatua migogoro kupitia vikao, mikutano ya vijiji, semina na mafunzo mbalimbali, michezo na kutumia vyombo vya habari kutoa elimu.

"Tanapa inasaidia miradi ya kipaumbele ya wananchi husika, inatoa asilimia 70 ya gharama za mradi wa kijiji husika katika eneo la afya, maji na elimu," anasema.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo, kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2009/10 Tanapa imesidia miradi ya maendeleo 451 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni Sh. milioni 16.6.

Kwa upande wa mafunzo, jumla ya vikundi 85 vyenye wanachama 185 vilisajiliwa na kupewa mafunzo, na kwa sasa kuna vikundi vipya 38 vyenye watu 190 kwenye hifadhi saba.

Fidia ikoje? Inaelezwa kwamba, iwapo mnyama atasababisha kifo kwa mwananchi kinatolewa kifuta machozi cha Sh. milioni moja, na fidia nyingine hutegemea na tathimini iliyofanywa na kubaini kiwango cha uharibifu.

MAZINGIRA

# Watafiti wa sayansi walipowaingiza wadau darasa la wadudu, udongo

- Misamiati migumu 'imepitwa na wakati'
- Wakulima wafunuliwa pa kuanzia ardhini

**Na Margaret Malisa, aliyekuwa Tanga**

NI muda mrefu sasa kuna madai habari za kisayansi haziandikwi ipasavyo katika vyombo vya bahari. Hapo kunazaa swali, kwanini hilo?

Jibu la awali kuchukua nafasi ni kwamba, kukosekana ushirikiano kati ya watafiti wa kisayansi na wanahabari, ikiambatana na dai la ugumu wa lugha inayotumiwa na wanasayansi kuwasilisha ama taarifa ya ujumbe wao.

Kwa maana nyingine mahali hapo kuna pengo ambalo serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), imeamua kuwakutanisha wanahabari na watafiti kutoka Kanda ya Mashariki, kutafutia jibu pengo hilo.

Hapo mtazamo zaidi ni kuwajengea uwezo wanahabari kupata njia rahisi ya kukitumia Kiswahili, kufikisha matokeo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa walengwa, husasani wananchi, kupitia mafunzo hayo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Costech, chini ya ufadhili wa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA).



Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania Dk. Zablon Nziku akiwaonyesha waandishi wa habari majani bora yanayotumika kwa malisho ya mifugo, wakati Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), ilipofanya ziara na waandishi habari katika taasisi za utafiti zinazofanya kazi zake. **PICHA: MARGARET MALISA**

### MTAFITI COSTECH

Dk. Bakari Msangi ni Ofisa Utafiti Mkuu Kiongozi kutoka Costech, anasema tayari wanahabari wa kanda tatu wameshapatiwa mafunzo, akiwataja maeneo yao ni: Zanzibar, Kanda ya Kusini na Mashariki. Pia wanaotarajia kumalizia katika mikoa iliyobaki nchini.

Anasema, kote walikotoa mafunzo, wameshaanza kushuhudia matokeo mazuri ya habari zinazoandikwa kisayansi, hivyo kuwafikishia walengwa taarifa yenye mwonekano chanya.

Katika hilo, wapo wahusika mahsusi kwa watunga sera wanaotaka kutumia taaluma ya kisayansi na ushahidi wa kitafiti kwa ajili ya kufanya maamuzi, akieleza namna pekee ya maamuzi yenye tija, ni kuwa na taarifa za kitafiti zenye ushahidi.

Kwa mujibu wa Dk. Msangi, aina hizo za taarifa zina msaada katika kuongoza ufanyaji maamuzi na kuyatumia katika maendeleo ya taifa.

"Utafiti ni shughuli ambayo inatumia mambo mengi ya uwekezaji, kwani zinatumika fedha nyingi kuwasomesha watafiti, kuandaa maeneo ya utafiti na utafiti wenyewe hadi ukamilike serikali inatumia gharama kubwa," anasema Dk. Msangi na anaongeza:

"Hivyo ni muhimu kuhakikisha kila unachokipata, kinatumika kuendelea kuongeza uzalishaji na tija kwa taifa."

Anasema, kutokana na Tanzania kuwa na vituo vingi vya utafiti wa kisayansi, ni wazi wanahabari baada ya mafunzo watajielekeza katika uandishi wa habari za kisayansi, kwa kuzingatia ukweli kwamba wamejijengea daraja la kazi yao na watafiti.

"Tayari tumeona matokeo ya wanahabari waliopata mafunzo katika kanda zingine ambazo tumetoa mafunzo haya. Nina imani hata ninyi mtafanya hivyo ndio lengo hasa la Costech kuona mnashirikiana na watafiti, ili tuone sayansi na teknolojia zinazoibuliwa na watafiti nchini zinafika kwa jamii," anasema Dk. Msangi.

Pia, anawataka watafiti waliohudhuria mafunzo kutoka vituo mbalimbali nchini, kujenga mazoea ya kukutana na wanahabari, ili kuwapa taarifa za kisayansi zinazofanyika katika vituo vyao.

Miongoni mwao ni Dk. Zabron Nziku, anayeshukuru kwamba mafunzo yamekuja katika wakati muafaka kwa maendeleo ya kukuza sayansi.

> **"Kabla ya kuanza kulima, sehemu ya kwanza mkulima anatakiwa kujua aina ya udongo wake kabla ya kufikiria mbegu bora ama mbolea na kadhalika.**

### MAABARA & WADUDU

Watafiti wanazungumzia teknolojia ya kuzalisha katika vituo vyao na kugundua kemikali ya kufukuza wadudu aina ya mbung'o wanaosababisha magonjwa ya malale kwa binadamu na nagana kwa wanyama.

Ofisa Utafiti wa Mifugo, Deusdedit Malulu, kutoka Wakala wa Maabara ya Vetenari Tanzania (TVLA), kutoka kituo cha Tanga, anasema wamegundua mnyama aitwaye kuro. Harufu yake inaweza kumfukuza mbung'o kwa asilimia 60 kuliko kemikali zilizoko sokoni.

Anasema, kwa kushirikiana na kiwanda cha A TO Z cha Arusha, sasa wako katika hatua za mwisho kuzalisha vifaa vitakavyotumika na kusambaza kemikali hiyo.

"Kifaa hicho kitakuwa kinafanya kazi ya kumlinda mnyama asing'atwe na mbung'o, kinaweza kufungwa sikioni kwa ng'ombe na kitakuwa kinatoa harufu iliyowekwa ndani ya kifaa hicho, ambayo itasambaa na kumfukuza mbung'o," anasema mtafiti huyo.

Anataja faida za kifaa hicho ni nyingi. Mojawapo ni kupunguzia gharama za kuogesha mifugo.

Mtafiti mwingine, Dk. Zabron Nziku, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Kituo cha Tanga, anasema taasisi hiyo inafanya utafiti wa malisho bora ya wanyama na kuzalisha mitamba bora ya ng'ombe na mbuzi, kisha kuwauzia wafugaji.

Anafanunua kuhusu upande wa uzalishaji wa mitamba bora ya ngombe na mbuzi, kwamba wanachanganya mbegu za jamii tofauti za ngombe na mbuzi ili kupata aina moja, inayokuwa na ubora zaidi na kutoa maziwa mengi na yenye ubora.

Dk. Nziku anasema, katika suala la malisho bora, TALIRI wanashirikiana na taasisi ya kimataifa za utafiti wa mifugo, ikiwamo ya nchini Kenya - ILRI, kufanya utafiti na majaribio ya malisho bora tofauti kwa mifugo, kupitia uchanganyaji wa aina za vinasaba ili kupata malisho bora.

### ZIARANI TANGA

Ni mafunzo yanayowalenga wanahabari kutembelea vituo vya utafiti, wajifunze kwa vitendo, namna watafiti wanavyofanya kazi. Utekelezaji wake ulitua katika Kituo cha Kilimo cha Utafiti cha Mlingano, kilichoko mkoani Tanga.

Dk. Sibaway Mwango, ni Mratibu wa Utafiti wa Rasilimali Ardhi za Kilimo nchini, anayeratibu wa utafiti na ubunifu wa kituo cha kilimo cha Mlingano, mkoani Tanga, anayesema kilimo nchini kimekuwa na changamoto kubwa kwa sababu ya kukosa tija ya kitaalamu.

Analalamika kwamba wakulima nchini hawafuati kanuni bora za kilimo wanapokuwa shambani, sababu kuu ni kwamba wanaendekeza mazoea na kushindwa kufikia faida ya kilimo chao.

"Kabla ya kuanza kulima, sehemu ya kwanza mkulima anatakiwa kujua aina ya udongo wake kabla ya kufikiria mbegu bora ama mbolea na kadhalika," anatamka na kuendelea:

"Hii itasaidia kupata mazao yenye ubora na hata mbolea kila zao linahitaji mbolea yake kulingana na unachotaka katika zao lile. Mfano muwa, unachotaka kuvuna katika muwa ni sukari. Kama utajua uweke mbolea gani, utajikuta unapata muwa mkubwa, lakini usiokuwa na sukari."

Dk. Mwango anawataka wakulima, kabla ya kuanza kulima wahakikishe wanawatumia watafiti kupata ushauri, ili waweze kulima na kupata faida.

Hata hivyo, anasema kwa sasa wana mkakati wa kushirikiana na Halmashauri husika kuangalia namna ya kuwafikia wakulima na kuwapa mafunzo ya kilimo, waweze kulima kwa tija na kuinuka kiuchumi.



# Sugu alalamikia polisi msibani, Chalamila amjibu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MSIBA wa Diwani wa Viti Maalumu, Enea Mbegale (Chadema) jijini Mbeya, umewakutanisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (Chadema) na kila mmoja kunena mazito.

Viongozi hao walikutana wakati wa kuaga mwili wa diwani huyo katika viwanja vya CCM -Rwanda Nzovwe, jijini Mbeya huku 'Sugu' akilalamikia Jeshi la Polisi mkoani humo kumzuia kufanya mikutano ya hadhara na wananchi wake kinyume na Katiba ya nchi.

Alisema mara nyingi amekuwa akiliandikia barua Jeshi la Polisi kutoa taarifa za kufanya mikutano ya hadhara, lakini anakataliwa kufanya mikutano hiyo bila sababu za msingi hali inayomlazimu kutumia mikusanyiko ya misiba kuzungumza na wananchi wake.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania mikutano ya hadhara inaruhusiwa na yeye kama mwakilishi wa wananchi anapaswa kulitaarifu Jeshi la Polisi kuhusu kusudio lake la kufanya mkutano kwa lengo la kuomba ulinzi na sio kuomba kibali.

"Kwenye misiba tunakuja kwa ajili ya kulia na kufarijiana na wafiwa, lakini kutokana na Jeshi la Polisi kunizuia kufanya mikutano nalazimika kufanya siasa kwenye maeneo kama haya kitu ambacho sio sahihi, sasa mimi nakuomba wewe kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kuniruhusu nizungumze na wananchi wangu," alisema Sugu.

Alisema kwa sasa Bunge halionyeshwi kwenye televisheni kama ilivyokuwa awali na kwamba njia pekee ya mbunge kupeleka mrejesho wa vikao kwa wananchi ni kupitia mikutano ya hadhara, lakini bado nayo anazuiliwa kuifanya. Alisema wakati mwingine Jeshi la Polisi limekuwa likimwelekeza akaombe kibali cha kufanyia mikutano kwa watendaji wa kata kitu ambacho alisema ni kumkosea heshima yeye kama mwakilishi wa wananchi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila alisema eneo la msibani sio la kufanyia siasa na badala yake watu wote bila kujali tofauti ya itikadi zao za kisiasa wanatakiwa kuungana na kuenzi mema ya marehemu.

Alisema pamoja na kwamba aliyefariki ni diwani anayetokana na Chadema, lakini alikuwa anawahudumia wananchi wote wa Jiji la Mbeya bila kujali chama wanachotoka. Chalamila alisema diwani huyo pamoja na wenzake walikuwa wanajadili mambo ambayo yalikuwa msaada mkubwa kwa maendeleo ya wananchi wa jiji hilo. "Ninachoweza kushauri kwa sasa ni kwamba tuige mema ambayo mheshimiwa diwani alikuwa anayafanya na yale ambayo tunaona ni mabaya tuachane nayo maana hayatatusaidia chochote," alisema Chalamila.

# Mbeya yaunda kikosi kazi ukusanyaji mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imeunda kikosi kazi maalumu cha kusimamia ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti upotevu wa mapato yake ya ndani.

Akizungumza na Nipashe juzi ofisini kwake, Mweka Hazina wa Jiji hilo, Amede Ng'wanidako, alisema kikosi kazi hicho kimeundwa kama sehemu ya mikakati ya kulikwamua Jiji kutoka katika nafasi ya mwisho kwenye ukusanyaji wa mapato.

Alisema kikosi hicho kinaundwa na wataalamu wa mapato ambao wanafanya kazi kwa muda wa siku sita za wiki kikifuatilia makusanyo ya mapato ikiwamo kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kwa kutumia mashine za EFD.

Ng'wanidako alisema siku ya Jumamosi wakuu wote wa idara wanaungana na kikosi kazi hicho kufuatilia makusanyo ya mapato kwenye vyanzo vyote vilivyopo.

"Mbali na kikosi kazi hicho, lakini tumenunua mashine za elektroniki za kukusanyia mapato 150 ambazo zimesambaa mitaani na zinatumiwa na maofisa wetu kukusanyia mapato kutoka kwenye vyanzo vyote," alisema Ng'wanidako.

Vilevile alisema halmashauri hiyo imefunga mfumo maalumu wa kukusanyia mapato katika Soko la Kimataifa la Mwanjelwa ili kuwarahisishia wateja kulipa mapato na kuboresha miundombinu ya masoko yote.

Hata hivyo, alisema wamefungua akaunti nne za kukusanyia mapato kutoka kwenye benki nne tofauti ili kuwarahisishia wananchi kulipa mapato na kwamba akaunti hizo zimeunganishwa kwenye mfumo mmoja.


Pia alisisitiza kuwa jiji hilo limebuni chanzo kipya cha mapato ambacho ni kutoza ushuru kwenye madini ya ujenzi ambayo ni mchanga, kokoto na mawe ambayo awali yalikuwa hayatozwi tozo ya aina yoyote.

Kwa upande wake mchumi wa halmashauri hiyo, Saad Mtambule, alisema kwa sasa inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kuchangia miradi iliyoibuliwa na wananchi.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ukarabati wa shule kongwe ya msingi Azimio iliyopo katika Kata ya Sisimba na kuibadili kuwa ya mchepuo wa Kiingereza ambayo imekarabatiwa kwa gharama ya Sh. milioni 360.

Miradi mingine ni ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Samora kunakofanyika ujenzi wa ukumbi na mabweni kwa gharama ya Sh. milioni 180.

"Kwenye sekta ya afya tumechangia Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Nzovwe, tumechangia pia ukarabati wa Kituo cha Afya Iyunga na tumetumia Sh. milioni 31.5 kwenye ujenzi wa machinjio ya kisasa Sabasaba," alisema Mtambule.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), Mkoa wa kihuduma Kibaha wakidhibiti uvujaji wa maji kwenye bomba la inchi 30 katika eneo la Visiga, Kata ya Saheni mkoani Pwani, jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Hospitali Mbarali yakamilika 90%

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

UJENZI wa Hospitali ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya umefikia zaidi ya asilimia 90.

Akizungumza na Nipashe ofsini kwake juzi, Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, alisema baadhi ya majengo yamekamilika kwa asilimia 90 isipokuwa moja ambalo limekamilika kwa asilimia 98 na jengo la wazazi limefikia asilimia 75.

Alisema sehemu kubwa iliyobaki ni umaliziaji ikiwa ni pamoja na kupaka rangi ya awamu ya pili na kuweka milango kwenye baadhi ya majengo ambayo yamekamilika.

Alisema kwa sasa mafundi wanaendelea na kazi ya kukamilisha maeneo hayo yaliyobakia ili hospitali hiyo ifunguliwe na iendelee kutoa huduma.

"Kwa kiwango kikubwa ujenzi wa hospitali yetu umekamilika japokuwa bado baadhi ya maeneo machache ambayo tumeelekezwa tuyaboreshe na muda sio mrefu itakamilika na kufunguliwa, kilichobakia ni milango na rangi kwa baadhi ya majengo," alisema Mfune.

Alisema mwezi Mei mwaka huu akiwa ziarani wialayani humo, Rais Dk. John Magufuli aliagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuhakikisha ujenzi wa hospitali hiyo unakamilika kabla ya Julai Mosi.

Aliwataka mawaziri wa wizara hizo kushirikiana kusimamia ujenzi wa hospitali hiyo ili ifunguliwe na wananchi waanze kupata huduma za matibabu.

Awali ilibainika kuwa nyaraka za mwanzo za ujenzi wa hospitali hiyo zilikuwa zimepotea katika mazingira ya kutatanisha na hivyo kusababisha ujenzi wake kukwama.

Serikali Kuu ilitoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo, lakini kutokana na changamoto mbalimbali bado ujenzi huo haujakamilika.





# Bashe awakomalia wazalishaji mbegu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amezitaka taasisi za umma na binafsi zinazohusika na uzalishaji mbegu kuacha kutegemea msimu katika kutekeleza jukumu hilo, ili kuzalisha mbegu za kutosha.

Bashe alisema hayo jana, wakati akifungua kikao cha wataalamu wa kilimo kutoka sekta binafsi na ya umma ambacho kimelenga kutoka na mwongozo wa upatikanaji wa mbegu bora.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya mbegu zinatoka nje ya nchi, hivyo taasisi hizo zinatakiwa kubadili uzalishaji wa kutegemea msimu kwa kuzalisha mara moja kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Bashe, taasisi hizo zinatakiwa kutafuta suluhisho la kudumu la changamoto ya upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali nchini.


"Tuondokane na uzalishaji wa kutegemea msimu kwa kuzalisha mara moja kwa mwaka. Ifike mahali tuzalishe mara tatu kwa mwaka ili kuwapo na mbegu za kutosheleza," alisema.

"Sisi wizara tunahitaji kujua, sekta ya kilimo inahitaji mbegu kiasi gani ndiyo maana nimeamua kukutana na nyie kujadili suala hilo ili mwisho wa siku tutoke na lengo moja na upatikanaji wake uwe wa uhakika na mfumo wa usambazaji ambao utamwezesha mkulima kuipata mbegu hiyo kwa wakati," aliongeza.

Aidha, alisema pamoja na kuhakikisha upatikanaji mbegu za kutosha pia ziwe za gharama nafuu ambazo mkulima atamudu.

"Mkifanya hivyo itakuwa rahisi hata kukutana na wawekezaji kuwaeleza nini tunahitaji katika uwekezaji kwenye suala la kilimo," alisema. Alitolea mfano wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ambayo alisema imekuwa ikizalisha mbegu wakati msimu wa upandaji tayari umepita hali inayoharibu malengo ya mkulima.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao wa Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimago, alisema wataalamu wana jukumu kubwa la kuhakikisha wanatimiza malengo ya Watanzania katika sekta ya kilimo.




Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Gank Nyamsogoro (wa pili kushoto), akikabidhi zawadi ya begi kwa Mkurugenzi wa Huduma za Afya Ustawi wa Jamii (Tamisemi), Dk. Ntuli Kapologwe, wakati wa kongamano la tatu la afya, lililoandaliwa na chuo hicho, kwa kushirikiana na St. Frasco na wataalamu wa sekta ya afya, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ulinzi binafsi watakiwa kuboresha maslahi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JESHI la Polisi limewataka wamiliki wa kampuni binafsi za ulinzi Tanzania kuboresha maslahi ya askari wao ili wasijiingize kwenye vitendo vya uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Simon Sirro, katika sherehe za kufunga mafunzo ya miezi mitatu kwa askari wa sekta ya binafsi ya ulinzi Tanzania (TSIA), jijini hapa. Alizitaka kampuni kizo kulipa mishahara mizuri kwa askari wao ili kuwaepusha kujiingiza kwenye vishawishi au kurubuniwa kufanya uhalifu.

"Lazima muwawezeshe maslahi mazuri wafanyakazi wenu pamoja usafiri wa kwenda kwenye maeneo ya malindo ili kuwaepusha na kurubuniwa na wahalifu," alisema.

Muroto alisema askari hao wanahitaji maslahi mazuri kama wafanyakazi wengine, hivyo maslahi yao yakiboreshwa watasaidia kuitangaza sifa nzuri ya kampuni husika.

Pia alisema kuna baadhi ya askari wa kampuni hizo hawana usafiri, hivyo wanatembea na silaha barabarani kwa miguu hali inayohatarisha usalama wao na jamii.

Aidha, alisema askari hao wanahitaji mafunzo ya mara kwa mara ili kuzibaini na kupambana na mbinu mpya za kihalifu katika jamii. Kamanda Muroto aliongeza kuwa askari hao walihitimu mafunzo hayo ni sehemu muhimu ya ulinzi katika jamii kwa sababu wanalisaidia Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu.

Naye msimamizi wa mafunzo hayo, Kidwadi Kalinga, alisema mafunzo hayo yalianza Julai Mosi, mwaka huu, yakiwa na askari 250 kutoka kampuni 28 za ulinzi mkoani hapa kwa kusimamiwa na polisi.

Hata hivyo, Kalinga alisema kati ya askari hao, waliomaliza ni 207 na wengine walishindwa kumaliza kutokana na kufukuzwa kwa sababu ya utovu wa nidhamu na wengine kutoroka.

Alisema katika mafunzo hayo walifundishwa ukakamavu, mbinu za kiulinzi, ukamataji, ulinzi wa raia na mali zao, doria na namna ya kujilinda wakiwa kwenye maeneo yao ya kazi.

Mkurugenzi wa Sekta ya Ulinzi Tanzania (TSIA), Isaya Marcel, alisema mafunzo hayo ni agizo la IGP Sirro aliyoagiza wakati wa kikao cha pamoja kilichofanyika Mei, mwaka huu.

Marcel alisema katika kikao hicho, mkuu huyo aliagiza askari wa kampuni zote za ulinzi binafsi kupewa mafunzo na polisi bila kujali kuwa walipitia mafunzo kwenye majeshi mengine.

# Kundi la matapeli laibukia Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imebaini kuwapo wimbi la matapeli ambao wamekuwa wakiwarubuni wafanyabiashara wadogo (machinga) kwa kuwapatia maeneo ya wazi yanayomilikiwa na taasisi za kidini ili kufanyia biashara.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema matapeli wamekuwa wakidanganya makundi hayo kuwa wana uwezo wa kuwapatia maeneo ya wazi yakiwamo yale yanayomilikiwa na taasisi za kidini na kujipatia kiasi kikubwa cha fedha kwa udanganyifu huo.

"Mfano kuna utapeli umefanyika eneo moja lililopo katikati ya jiji ambalo linamilikiwa na taasisi ya kiislamu. Kuna utapeli umefanywa wa upimaji kwa lengo la kuwaweka wamachinga wanaofanya biashara zao msikiti wa Nunge suala ambalo ni kuwadanganya kwa kuwa eneo hilo si la biashara," alisema.

Ofisa huyo alisema maeneo yote yanapatikana kwa mujibu wa sheria na taratibu za jiji na hata kama eneo hilo linamilikiwa na taasisi yoyote iwe ya kidini au watu binafsi wenye mamlaka ni halmashauri husika na si vinginevyo.

Kwa upande wao, baadhi ya wakazi wa jiji walikiri kuwapo kwa udanganyifu huo ikiwa ni pamoja na uuzaji wa maeneo ya wazi kwa ajili ya kufanya shughuli za kibiashara.

Mmoja wa wakazi aliyejitambulisha kwa jina la Ngonyani alisema utapeli huo ni kweli upo ikiwamo eneo la taasisi za Kiislamu kuvamiwa kwa malengo ya kutaka kuwauzia ili waweze kuhamishia biashara zao hapo.

Mjumbe wa taasisi ya kiislamu ambayo inamiliki eneo hilo, Max Mbutu, alikiri kutokea upimaji wa eneo hilo na kusema kuwa tayari hatua za awali za kuzuia utapeli huo zimefanyika na kuwataka wakazi kujihadhari na matapeli hao.

# Askofu ataka amani ilindwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Augustino Shayo, amewataka waumini wa dini zote kuilinda amani iliyopo nchini kwa kuepuka kutoa matamko yanayoweza kuihatarisha tunu hiyo.

Shayo aliyasema hayo juzi wakati wa kuhitimisha mkutano wa siku mbili wa kimataifa kwa viongozi wa dini uliokuwa ukifanyika visiwani Zanzibar.

Alisema kuendelea kuwapo kwa ushirikiano miongoni mwa waumini wa dini mbalimbali kumeimarisha amani na utulivu nchini.

Pamoja na kushirikiana katika shughuli za maendeleo kwenye jamii, Askofu Shayo alisema waumini hao wamekuwa chachu katika kudumisha amani kwa jamii ya Watanzania.

Aidha, alisema kuna haja ya kuilinda amani hiyo iliyodumu nchini tangu taifa lilipopata uhuru na kusisitiza kwa viongozi wa dini kutumia nafasi waliyonayo katika jamii kwa kuwashawishi wananchi kudumisha amani.

Naye Profesa Issa Haji Zidi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), alisema kwa namna ya serikali inavyotambua juhudi zinazofanywa na viongozi wa dini katika kuhakikisha jamii inaendelea kuishi kwa furaha, upendo na amani, ni jambo la kujivunia.

Alisisitiza umuhimu wa kuendelezwa kwa mikutano kama hiyo sehemu mbalimbali kwa vile itasaidia kuimarisha uhusiano mwema kati ya dini moja na nyingine pamoja na kuhakikisha amani inadumishwa.

Alisema wanaadamu wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwapa zawadi ya neema ambayo katika baadhi ya mataifa duniani imekosekana, hivyo kuishi kwa vurugu na mapigano.

Katibu wa Muungano wa Makanisa ya Kiinjili kutoka Ujerumani, Mchungaji Dk. Jochen Motte, alisema uongozi wa kanisa hilo utaendelea kushirikiana na mataifa, taasisi na mashirika mbalimbali duniani yaliyojitolea kusimamia amani.

Alisema faida ya amani huchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la uchumi na kuimarika kwa ustawi wa jamii.

Alisema hali hiyo hutokana na wanajamii kupata fursa pana zaidi ya kujikita katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na hatimaye pato la taifa kukua kutokana na uimarishaji wa miundombinu ya sekta tofauti.

Mkutano huo uliowashirikisha viongozi wa dini na wanazuoni wapatao 70 kutoka Afrika, Asia na Ujerumani ulikuwa na ujumbe wa amani unaohimiza kuzishinda vurugu na kujenga jamii isiyokuwa na utengano.

Pia ulikuwa na lengo la kupinga aina zote za misimamo mikali, ubaguzi wa rangi, rushwa na matumizi mabaya ya nguvu kisiasa na na kiuchumi pamoja na udhalilishaji wa kidini kwa kuhalalisha vurugu zinazofanywa kwa jina la imani.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akizungumza na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri apigia chapuo Bandari ya Mkoani

**Na Rahma Suleimman,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA katika kisiwa cha Pemba wametakiwa kutumia huduma za Bandari ya Mkoani kwa ajili ya kushusha bidhaa zao yakiwamo makontena kutokana na kuimarika kwa ubora wa huduma.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mohamed Ahmada, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Magogoni, Shekhe Hamad Matar, aliyetaka kujua kwa nini wafanyabiashara kutoka Pemba bado hawatumii bandari hiyo.

Ahmada alisema katika Bandari ya Mkoani Pemba tayari liko eneo la kuweka makontena mara yanaposhushwa kutoka katika meli likiwa na uwezo wa kupokea makontena 22 kwa wakati mmoja.

Aidha, alisema wafanyabiashara mbalimbali wameelimishwa kuhusu uwezo wa bandari hiyo kupokea mizigo ikiwamo makontena.

Hata hivyo, alisema tatizo lipo kwa wafanyabiashara wenyewe ambao bado hawajatumia fursa hizo ambazo zinatolewa katika bandari hiyo. "Serikali imeimarisha kwa kiwango kikubwa uwezo wa Bandari ya Mkoani Pemba kupokea mizigo na makontena yapatayo 200. Tatizo ni wafanyabiashara wenyewe hawako tayari kuleta mizigo yao," alisema. Alisema baadhi ya wafanyabiashara wa Pemba wanatumia Bandari ya Wete kwa ajili ya kupeleka bidhaa zao mbalimbali ikiwamo saruji kutokana na unafuu.

"Nilitembelea Bandari ya Wete Pemba na kuona bidhaa mbalimbali zinazotoka Mombasa zikiwasili na kushushwa hapo. Nilipowauliza wafanyabiashara waliniambia wanatafuta unafuu na urahisi wa kufika mzigo kwa haraka," alisema.

# Mafanikio makubwa elimu watu wazima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema imepata mafanikio kwa asilimia 84 katika elimu ya watu wazima kwa kuliwezesha kundi hilo kujuwa kusoma na kuandika.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chumbuni, Miraji Khamis Mussa, aliyetaka kujua mafanikio ya kisoma cha watu wazima na maendeleo yake.

Pembe alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bado inaendelea kusimamia na kuendesha elimu ya watu wazima kwa lengo la kuhakikisha hakuna mtu asiyejua kusoma na kuandika.

Alisema mikakati ya kujua kusoma na kuandika ni agizo la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na matamko ya kimataifa yanayotaka kuona kwamba ujinga na kutojua kusoma unatokomezwa.

Naibu Waziri alisema madarasa ya elimu ya watu wazima yapo nchini kote Unguja na Pemba yakiendelea kuwapatia elimu kundi hilo.

Alisema wanafunzi 227 wanaendelea na kisomo cha watu wazima kwa upande wa Pemba, wakati 278 wako Unguja.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea na mikakati yake ya kuwapatia watu wazima kisomo ambacho kitawawezesha kufuta ujinga wa kutojua kusoma," alisema.

Alisema madarasa hayo yanaendelea vizuri na wizara kwa kushirikiana na kamati za wazazi za halmashauri, inaendelea kuyaunga mkono kuona

# Ulaji samaki Tanzania aibu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema kiwango cha ulaji wa samaki kwa Watanzania kipo chini sana licha ya taifa kuwa na rasilimali hiyo kwa wingi.

Alisema taifa limebarikiwa kuwa na maziwa, mito, bahari na mabwawa ya wafugaji lakini ulaji wa kitoweo hicho hauridhishi.

Alieleza kuwa takwimu zinaonyesha kuwa ulaji wa samaki nchini ni kilo nane kwa mwaka, ikilinganisha na kiwango cha Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba inapaswa kuwa kilo 20.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini Mwanza wakati akizindua kadi ya uvuvi jijini Mwanza uliofanywa kati ya Benki ya Posta (TPB) na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wavuvi Tanzania (Chakuwata).

Chakuwata na TPB wamekubaliana kukopesha fedha wanachama hao kwa lengo la kurasimisha kundi hilo na kuwakwamua kiuchumi.

Ulega alisema anashangazwa kuona kiwango cha ulaji wa samaki kikiwa chini sana licha ya Tanzania kuwa na samaki wengi na kwamba takwimu zinaonyesha samaki waliovuliwa mwaka jana ni tani 450,000, huku mahitaji ni tani zaidi ya tani 700,000.

"Tangu hafla hii ianze hapa sijaona wavuvi mnacheka au mnafurahia maneno yanayozungumzwa na viongozi. Najua hamu yenu ni kutaka kusikiliza kama serikali itakuja na tamko mbadala la kuruhusu mtumie zile nyavu tulizozikataa.

Pia natambua mnatumia sababu ya kwamba nchi zile za upande wa pili zinaendelea kutumia nyavu ambazo sisi Tanzania tumezizuia," alisema.

Aliwaambia kuwa sheria za makubaliano ya kutumia nyavu zilipitishwa na nchi zote, lakini kama upande wa pili bado hawazingatii Tanzania itaendelea kusimamia sheria na makubaliano hayo.

Alisema kama haitoshi bado itafuatilia kuona kinachofanyika huko upande wa pili.

"Leo tumekutanishwa hapa kwa jambo kubwa sana ambalo tumeona ninyi wavuvi mnapaswa kuwezeshwa ili kufanya shughuli hii kwa kutumia vifaa vyenye ubora. Hivyo TPB imekuja hapa kwa ajili ya kumtambua mtu mmoja mmoja na kikundi, ndio maana mnaingia makubaliano kupitia chama chenu," alisema Ulega.

Aliwaambia anataka kiwango cha ulaji wa samaki kitoke kilo nane kwa mwaka kifikie angalau kilo 20 zinazopendekezwa na WHO.

Ulega alisema bado haamini takwimu zinazotolewa kwamba sekta ya uvuvi inachangia pato la taifa kwa asilimia 1.7 ikiwa inashika nafasi ya nne, ambapo aliwataka wahusika wa kukusanya takwimu kufanya unyambulisho wa matumizi ya samaki kuanzia minofu, mifupa, utumbo, mabondo na matamvua.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa TPB, Sabasaba Moshingi, alisema ikiwa taasisi za fedha zitasogezwa kwa wananchi, itakuwa ni rahisi taifa kupambana na umaskini na kufanikiwa kukwamua jamii kwa pamoja.

Alisema tangu benki hiyo ianzishwe na kukakabidhiwa benki zingine zilizokuwa zinasuasua katika uendeshaji, imeendelea kupata faida kila mwaka, ambapo mwaka jana ilipata faida ya Sh. bilioni 17. 4 na kulipa gawio kwa serikali miaka mitatu mfululizo.

"Leo tunaingia makubaliano na Chakuwata hivyo tunawaomba wavuvi ile tabia ya kukaa na fedha nyumbani au kwenye mifuko yenu iishe, fungueni akaunti hapa leo na tuanze kukopeshana kulingana na masharti nafuu kabisa," alisema.

Mwenyekiti wa Chakuwata, Rigobert Mpemba na Katibu Mkuu wa ushirika huo, Bakari Kadabi, walieleza kufurahishwa na ushirikiano wa serikali.



Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Ziwa, Uthmaan Madati, akiwasha gari la mfano atakalopewa mshindi wa Tigo chemsha bongo, wakati wa ufunguzi wa msimu wa Tigo Fiesta Saizi Yako na bahati nasibu ya Tigo chemsha bongo, jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaooza mabinti sasa kuona mkono wa chuma

**Na Happy Severine,** ITILIMA

SERIKALI imewaasa wazazi kuacha kuwageuza mabinti kuwa mitaji na chanzo cha mapato kwa kuwaoza badala yake wawasomeshe ili wawe msaada kwa familia hapo baadaye. Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William ole Nasha, alisema hayo jana wakati wa ziara yake wilayani Itilima mkoani Simiyu, baada ya kukagua ujenzi wa mabweni ya wasichana ya Sekondari Nkoma.

Aidha, alikagua pia ofisi ya wadhibiti ubora na jengo la Chuo cha Ufundi Stadi (Veta) linalojengwa katika Kijiji cha Kanadi wilayani humo.

Alisema hadi sasa serikali imetumia Sh. bilioni 308 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu ya elimu na sekondari, na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ikipatiwa Sh. bilioni tano, fedha zilizotolewa ndani ya miaka minne.

Akizungumzia suala la mabinti alisema: "Kuna baadhi ya wazazi wanashawishi watoto wao kufanya vibaya katika mitihani yao ya mwisho ili wasiendelee na sekondari. Niwaombe msishawishi watoto wa kike, tena msiwawekee vikwazo vya kukatisha masomo."

Aidha, alisema: "Mtoto wa kike ana nafasi ya kupata elimu sawa na wa kiume na pia mtoto wa kike ni wa serikali, hivyo mnaowakatisha masomo mtakiona cha moto," alisema Naibu Waziri ole Nasha.

Aliongeza kuwa serikali na wadau wa elimu waendelee kutoa hamasa ya elimu kwa jamii, wanafunzi wa wazazi ili miundombinu ya elimu inayojengwa iweze kutumika. Naibu Waziri aliongeza kuwa ndani ya miaka minne Simiyu imepiga hatua ya ufaulu wa wanafunzi na kufikia asilimia 66, huku usimamizi wa fedha za miradi ya elimu ikifanyika kwa umakini.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa mabweni hayo, Mkuu wa Sekondari ya Nkoma, Sara Matonya, alisema mabweni hayo yatagharimu Sh. milioni 304 na kukamilika mradi huo kutachochea hamasa ya wanafunzi wa kike kusoma kwa bidii kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia.

Alisema kila bweni linabeba wanafunzi 80 na wanafunzi hao wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 15 kufika shuleni, pia mahudhurio ya wanafunzi wa kike yameongezeka kutokana na kuepuka vishawishi na mimba zilizowakatisha masomo.

Wazazi na wanafunzi hao wameipongeza serikali kutoa elimu bila malipo na kuifanya jamii kuongeza ari ya kusoma, mahudhurio darasani kuongezeka na ufaulu.

# Kalemani awapa kazi wataalamu

**Na Futuna Seleman,** MKURANGA

WIZARA ya Nishati, imewapa mwezi mmoja wataalamu wa nishati kufanya mapitio ya bei za gesi viwandani ili kuwawezesha wawekezaji kuzalisha kwa tija.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alitoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) na ile ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (Pura) kufanya mapitio hayo.

Alisema hayo alipozindua matumizi ya gesi asilia katika kiwanda cha Lodhia Group cha kufua vyuma kilichopo Kisemvule wilayani Mkuranga Mkoa wa Pwani, ambacho awali kilikuwa kikitumia mafuta mazito. Akizungumza baada ya kukagua shughuli za kiwanda hicho pamoja na kufanya uzinduzi alisema: "Mje na bei mwafaka ambazo haziathiri uwekezaji wa TPDC na haziathiri uwekezaji wa wenye viwanda lakini pia zisiathiri mapato ya serikali."

Alifafanua kuwa bei ya sasa inaanzia Dola 4.7 hadi 7.72 kwa uniti moja, ambayo imekuwa kikwazo kwa wawekezaji.

Aidha, alisema TPDC inatarajia kukusanya kati ya Sh. milioni 85 hadi 120 kwa mwezi, sawa na Sh. bilioni 1.02 hadi 1.4 kwa mwaka kutokana na matumizi ya gesi asilia katika kiwanda cha Lodhia, ambayo hadi sasa ni futi za ujazo 200,000 kwa siku.

Alifafanua kuwa mbali na makusanyo hayo kwa serikali kwa upande wa kiwanda, kupitia matumizi ya gesi asilia, kimepunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa zake kwa zaidi ya asilimia 40 ikilinganishwa na gharama zilizokuwa zikitumika kwa ajili ya mafuta mazito.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, alipongeza jitihada za wizara hiyo, kusambaza umeme na gesi kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Lodhia, Sailesh Pandit, alisema Wizara ya Nishati, TPDC na Tanesco ikiwapa ushirikiano mkubwa katika kuongeza tija ya uzalishaji kwa kuwapatia nishati pasipo vikwazo.

# Wabunge waanza kumchunguza Trump

**WASHINGTON,** Marekani

CHAMA cha Democrats nchini Marekani kimeanzisha uchunguzi rasmi dhidi ya Rais wa nchi hiyo, Donald Trump, kuhusiana na madai kwamba alitaka usaidizi kutoka kwa taifa la kigeni ili kumwangamiza hasimu wake wa kisiasa.

Tangazo lililotolewa na Spika wa Bunge la Congress, Nancy Pelosi, lilitoa ruhusa rasmi kwa kamati kuchunguza mazungumzo ya simu za Rais Trump na kiongozi wa Ukraine ili kubaini endapo alifanya kosa linaloweza kusababisha afanyiwe uchunguzi wa kuondolewa madarakani.

**Wiki hii Rais Trump alikiri kumwomba Rais wa Ukraine kuchukua hatua ambazo zitamnufaisha kisiasa, Rais lazima awajibishwe.**

Hata hivyo, Rais Trump amekanusha madai hayo na amezitaja juhudi za kumtuhumu kama hila chafu dhidi yake, huku kukiwa na uungaji mkono mkubwa kutoka kwa wafuasi wa Chama cha Democrats juu ya uchunguzi huo unaoweza kumwondoa madarakani.

Katika tangazo lake Pelosi alisema kuwa kamati nyingine sita zinazofanya uchunguzi wa masuala mengine dhidi ya Rais Trump zitaendelea na uchunguzi wao chini ya uchunguzi wa sasa.

Endapo uchunguzi huo utaendelea, Bunge la wawakilishi litapiga kura mashtaka yoyote yatakayobainika, wabunge wa Democrats ndio wengi katika bunge la congress wanaweza kupitisha uamuzi wa kumshtaki.

Hata hivyo, maamuzi hayo yanaweza kupelekwa katika Bunge la Seneti ambako theluthi tatu ya wabunge inahitajika kupitisha maamuzi ambako wabunge wa Republicans wataweza kuzuwia mashtaka.

Mzozo huo ulichochewa na ripoti za jasusi aliyefichua malalamiko kuhusu simu ambazo Rais Trump alimpigia mwenzake wa Ukrain Volodymyr Zelensky.

Hata hivyo bado haijabainishwa nini marais hao walizungumza, lakini Democrats wanamshutumu Rais Trump kutishia kusitisha msaada wa kijeshi kuishinikiza Ukraine kuchunguza madai ya rushwa dhidi ya makamu wa rais wa zamani, Joe Biden na mtoto wake wa kiume Hunter.

Rais Trump alikiri alimzungumzia, Joe Biden na Zelensky lakini alisema alikuwa akijaribu kuitaka Ulaya iingilie kati kutoa msaada kwa kuitishia kusitisha msaada wa kijeshi.

Pelosi alisema kuwa Rais Trump alifanya kosa la ukiukaji wa sheria na kuyataja matendo yake kama uvunjaji wa wajibu wake kikatiba.

"Wiki hii Rais Trump alikiri kumwomba Rais wa Ukraine kuchukua hatua ambazo zitamnufaisha kisiasa, Rais lazima awajibishwe," alisema Pelosi.

Wakati huo huo, Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Taifa la Ujasusi nchini Marekani, Joseph Maguire, alikataa kushirikisha Bunge la Congress ripoti ya mtu aliyefichua taarifa za shutuma dhidi ya Rais Trump.

Maguire anatarajiwa kutoa ushahidi mbele ya kamati ya umma ya ujasusi leo.

Kura ya maoni iliyoendeshwa na Shirika la A YouGov ilieleza kuwa asilimia 55 ya Wamarekani wangeunga mkono kushtakiwa kwa Rais Trump ingethibitishwa kwamba Trump alisitisha msaada wa kijeshi kwa Ukraine ili kuwashinikiza maofisa wa nchi hiyo kumchunguza Joe Biden. **BBC**



Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi ambaye ametangaza kuanzisha uchunguzi rasmi wa kumfungulia mashtaka Rais Donald Trump. **PICHA: REUTERS**

## Kenya, Somalia zakubaliana ushirikiano

**NAIROBI,** Kenya

SOMALIA na Kenya zimekubaliana kufanya kazi pamoja katika juhudi za kuboresha uhusiano baina yao.

Hatua hiyo imekuja baada ya Rais wa Misri, Abdelfatah Al Sisi, kuwapatanisha Marais Uhuru Kenyatta wa Kenya na mwenzake wa Somalia, Mohammed Abdullahi Farmaajo.

Upatanisho huo ulifanyika baada ya kufanyika kwa mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN).

Viongozi hao wameafikiana kuwa watafanya kazi pamoja bila ya kuathiri kesi juu ya mpaka kati ya mataifa hayo mawili inayoendelea katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (ICJ).

Somalia ilienda katika Mahakama ya ICJ ikitaka mpaka wa baharini kati yake na Kenya kuchorwa upya ili uweze kushuka chini ukipita mpaka wake wa ardhi badala ya kwenda mashariki.

Kenya iliishutumu Somalia kwa kuendelea kutangaza mauzo ya mafuta hayo kwa wawekezaji licha ya kwamba eneo hilo bado linamgogoro.

Kenya ilidai kuwa Mogadishu imekuwa ikitumia ramani ambayo inaingilia himaya ya Kenya. Hata hivyo, Mogadishu imepinga tuhuma hizo.

Kenya ilisema kwamba baadhi ya kampuni zimeanza kutafuta mafuta katika maeneo hayo yanayodhaniwa na mataifa yote mawili.

Tayari kundi moja la wataalamu wa baharini nchini Kenya wameiomba serikali kutotumia nguvu na badala yake kutumia diplomasia kwa minajili ya amani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi.

Kundi hilo limesema kwamba iwapo Kenya itapoteza kesi hiyo kwenye mahakama hiyo ya kimataifa itasalia nchi isio na bahari na italazimika kuiomba Somalia na Tanzania ruhusa kwa meli zake kuingia katika Bahari ya Mombasa.

Hiyo inamaanisha kwamba kesi hiyo itaendelea licha ya Kenya kuendelea kutafuta suluhu nje ya mahakama hiyo. **BBC**

## Waziri Mkuu Uingereza agoma kujiuzulu

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson (pichani), amepuuza wito wa kujiuzulu, baada ya uamuzi wa mahakama ya juu kwamba hatua yake ya kuahirisha bunge ilikuwa kinyume na sheria.

Uamuzi huo wa mahakama ya juu zaidi nchini Uingereza umeungwa mkono kwa kauli moja na majaji wote 11, hali ambayo imezidisha uzito wa uamuzi huo, matatizo kwa Waziri Mkuu, Johnson.



Rais wa mahakama hiyo, Lady Hale alisema hatua ya serikali ilikuwa na malengo ya kulitatiza bunge kufanya majukumu yake.

"Kwa hiyo mahakama imehitimisha kwamba uamuzi wa kumshauri Malkia kusitisha shughuli za bunge ulikuwa kinyume na sheria, kwa sababu matokeo yake yalilitatiza bunge, au yalilizuia bunge kufanya majukumu yake ya kikatiba, bila sababu yoyote ya msingi," alisema rais huyo wa mahakama ya juu ya Uingereza.

Akizungumza kwa mara ya kwanza baada ya uamuzi huo wa mahakama mjini London, Johnson ambaye yuko mjini New York Marekani akihudhuria mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN), amepuuza wito uliyotolewa na wanasiasa mbalimbali wakimtaka ajiuzulu, akisema kuwa kwa maoni yake, uamuzi wa mahakama ya juu haukuwa sahihi.

Johnson alisema: "Inabidi niseme kwamba napingana vikali na uamuzi wa majaji. Sidhani kama ni sahihi, lakini bila shaka tutasonga mbele na vikao vya bunge vitafanyika tena."

Katika hukumu yake, mahakama ya juu ilieleza kuwa hivi sasa ni wajibu wa viongozi wa bunge kuamua muda wa kuanza tena vikao vyao, na tayari spika wa baraza la chini, John Bercow, alisema milango ya bunge huko Westminster itafunguliwa siku ya Jumatano (jana).

Spika huyo alisema uamuzi wa mahakama ya juu ni wa kihistoria, na kwamba raia wanayo haki ya kuona wawakilishi wao wakitimiza majukumu yao ya kikatiba ya kuishinikiza serikali kuwajibika. **DW**

# Wawekezaji walalamika utitiri wa kodi, umeme

**Mwandishi Wetu,** RUVUMA

WAFANYABIASHARA na wawekezaji wa Mkoa wa Ruvuma wameeleza kero mbalimbali zinazochangia kukwamisha ukuaji wa uwekezaji mkoani humo ikiwamo tatizo la umeme kukatika huku baadhi ya wafanyabiashara wakilalamikia utitiri wa kodi.

Wametoa malalamiko yao kwenye mkutano kati ya serikali na sekta binafsi unaohusisha wawekezaji, wafanyabiashara na jopo la mawaziri saba wakiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, uliofanyika wilayani Songea.

Katika mkutano huo wa kusikiliza kero na changamoto zao, wameeleza jinsi umeme unavyosumbua hali inayochangia uzalishaji kuzorota na kuiomba serikali kushughulikia tatizo hilo ili waweze kujikwamua kiuchumi. Baadhi yao walemalamikia tatizo la wingi wa tozo zinazotozwa na halmashauri na Serikali Kuu na kuiomba kuangalia namna ya kurekebisha tatizo hilo kwa kuwa lengo siyo kukwepa kulipa kodi, bali ziwe zinalingana na biashara wanazofanya.

Akijibu baadhi ya kero hizo kwa kushirikiana na mawaziri wengine, Waziri Kairuki alizikumbusha mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maamuzi ya serikali kwa kuhakikisha kodi, tozo na ada zilizofutwa na serikali haziendelei kutozwa kwenye maeneo yao.

"Kwa namna yoyote, tusiwe kikwazo bali tuwezeshe sekta binafsi izidi kustawi na hivyo kuchangia kikamilifu katika uchumi wa taifa kwa kulipa kodi, kwa ajili, kuzalisha bidhaa na kutoa huduma kwa wananchi," alisema Waziri Kairuki.

Alisema serikali inasisitiza ulipaji wa kodi na tozo mbali mbali kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na taifa kwa ujumla.

"Nasisitiza kuwa kila mfanyabiashara na mwekezaji ana wajibu wa kulipa kodi na tozo stahiki kwa serikali kwa kufanya hivyo, itakuwa na uwezo mkubwa wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji," alisema Waziri Kairuki.

Pia, alisema viongozi na watendaji kuanzia ngazi ya halmashauri na mkoa wanapaswa kuhamasisha uwekezaji katika mikoa yao na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ili kuimarisha ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

"Napenda kuwahakikishia kuwa, changamoto ambazo zimejadiliwa katika kongamano hili tutazitafutia ufumbuzi wa haraka ili kuboresha mazingira ya kufanyia shughuli zenu kwa manufaa ya nchi nzima."

Waziri Kairuki alisema wamepata mengi kuliko walivyotarajia na kuwaomba wawekezaji hao na wafanyabiashara wazingatie mwelekeo wa serikali ili kwa pamoja waweze kujenga uchumi wenye manufaa kwa watu wote.

"Kwa mara nyingine tena, niwahimize wananchi kwa ujumla kuwa jinsi uchumi wetu unavyokua fursa pia za uwekezaji zinaongezeka, ukuaji wa uchumi unaongeza uwezo na ukubwa wa mahitaji," alieleza.

Aliwataka wawekezaji ambao wameshaingia kwenye uwekezaji na biashara, wasichoke kutafuta fursa katika sekta mpya zinazoletwa na maendeleo ya kiuchumi na mabadiliko ya teknolojia.



Meneja Mwandamizi Kitengo cha Amana kwa Wateja wa Benki ya Akiba Commercial Bank Plc, David Korosso, akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa huduna mpya ya akaunti ya uwekezaji ijulikanayo kama Akiba Lengo Investment Plan jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Dora Saria (kushoto) na Meneja Uwekezaji wa benki hiyo, Fatuma Kigembe. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi watakiwa kutulia madai volkano

**Na Dotto Charles**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (pichani chini), amewataka wananchi wa eneo la Ndembezi na Shinyanga kuwa watulivu wakati uchunguzi ukiendelea katika eneo lilipotokea tope zito linalovuja kutoka chini ya ardhi na kudaiwa kuwa ni volkano.

Hayo ameyasema jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kutoa taarifa juu ya kutokea kwa hali hiyo ambapo alisema serikali ilichukua hatua za haraka na wataalamu wa jiolojia walifika katika eneo la tukio na kufanya uchunguzi.

Alisema uchunguzi uliofanywa na wataalamu hao kutoka taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kwa kushirikiana na ofisi ya madini ya Mkoa wa Shinyanga Septemba 20, mwaka huu umebaini kuwa hiyo ni volkano ya tope na si volkano.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa tafsiri sahihi ya volkano ya tope ni hali ya kububujika kwa tope la udongo kutoka chini ya ardhi linaloambatana na maji kama chemchem likiwa na joto la kawaida tofauti na uji uji wa miamba ambao huwa na joto kali hali inayosababishwa na nguvu za asili zinazotokana na mtikisiko na mgandamizo wa matabaka ya miamba na udongo wa chini ya ardhi ingawa shughuli za kibinadamu huchangia kutokea kwa matukio kama hayo.

Telack aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.



# Ndugulile ataka wanawake kugombea uongozi S/Mitaa

**Na Kelvin Innocent**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amewataka wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi wa kiserikali na kushiriki katika uchaguzi ujao.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza katika Tamasha la 14 la Jinsia jijini Dar es Salaam lililoandaliwa na TGNP Mtandao jijini Dar es Salaam, akilitaka shirika hilo lihamasishe wanawake kushiriki katika uchaguzi ujao.

Dk. Ndugulile alisema amekuwa akiongea na kinamama wengi hasa wa jimboni kwake kuhusu kuchangamkia nafasi za uongozi, lakini bado kuna ugumu kwao kujitokeza kugombea nafasi.

"Jimbo langu lipo hapa Dar es Salaam (Kigamboni), nina mitaa 67, lakini ukiangalia mitaa hiyo wenyeviti wa serikali za mitaa ni wanawake wawili tu.

"Sasa, hatuwezi tukapiga hatua kama katika msingi wa uamuzi ambao ndiyo ngazi ya mtaa, hatuna wawakilishi wanawake," Dk. Ndugulile alisema.

Aliwataka TGNP Mtandao kuwa mstari wa mbele wa kuwahamasisha wanawake kujitokeza kushiriki katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa.

"TGNP kazi ni moja hii tuhamasishe wanawake kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na wakamate nafasi za uwenyeviti," alishauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alisema malengo ya tamasha hilo ni kusherehekea na kudadisi safari yao ya miaka 25 ya ukombozi wa mwanamke pamoja na kutoa nafasi ya kujifunza ili kupanua maarifa katika masuala ya kijinsia.

Lilian alisema: "Tungependa kuona watoto wetu wa kike wasome, wamalize bila ya kukatishwa na mimba za utotoni, kwa miaka inayokuja 25 tuhakikishe kwamba hakuna mtoto anatoka shule kwa mimba za utotoni."

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI


## KUPOTEA KWA PASIPOTI



EVA ISARIA LYATUU
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, AB 815487 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji mwaka 2016.

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

KL/MOS/RB/326899/2019

215433402

---

IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA
AT BUKOBA
RM.CIVIL CASE NO: 11/2019

MUSSA OMARY .................................... PLAINTIFF
VERSUS
ALLY MOHAMED ............... ..............1ST DEFENDANT
JAMES GAIDON ...................................2ND DEFENDANT
LASAR LOGISTICS CO, LTD..................3RD DEFENDANT

**NOTICE OF MENTION**

TO: JAMES GAIDON
P.O.BOX DAR-ES-SALAAM.

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for MENTION on the 15RD day of OCTOBER, 2019 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D LUAMBANO -RM. Your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 23th day of SEPTEMBER, 2019.

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

115433202

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS PETER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S0156/0140** kilichotolewa na TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL mwaka 1999.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MS/RB/555/2008.**

115433002

## KUPOTELEWA NA CHETI CHA MATOKEO CHUO CHA MIPANGO MWANZA



**VAILETH WILIAM YUNGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHAKE CHA MATOKEO (TRANSCRIPT) CHENYE NAMBA **IRDP-LZC/CRP/15/2178** CHA CHUO CHA MIPANGO MWANZA KILICHOTOLEWA NA NACTE MWAKA 2016.

YEYOTE ATAKAE KIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:
**GR/RB/1608/2019**

115432902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DEUS DICKSON MUKARE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA SPRINTER MODER AE 110 BODY TYPE SALOON YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 962 BTT** YENYE CHASSIS NAMBA **AE II03009991** NA ENGINE NAMBA **5AH 171389.** TAARIFA YA POLISI **KHM /TR/ RB/2247/2018.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

115432202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Lissa Daniel Kalokola** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0248-0528 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya
Sekondari Marian Girls.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Report Namba:**
**991089954783**

115429302

## KUPOTEA KWA CHETI



**BENEDICT M. SEMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato nne chenye index namba **S.686/0016** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1997 katika shule ya Sekondari Chato.
Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/STA/RB/324603/2019**

115430502

---

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo Tanga Mjini**

**Usimamizi wa Mirathi Namba 143/2019**

**Ombi la Ibrahim Joram kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu Thomas Leonard Bocco**

**Kwa yeyote anayehusika.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe: 24/9/2019**

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

115432602

## WUZHOU INVESTIMENT CO L.T.D

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.276-BZP** aina ya SANLG,yenye Chasis namba **LBRSPJB54J9017086,**Engine namba **SL157FMI18919695.** Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/TR/746/2019.**

1154325O2

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 172/2019**

**Ombi la JOSEPH RIKERESE MTATIRO NA NSHAMA MTATIRO MARWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PRISCILLA RAPHAEL EGOLOGOLO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/09/2019.

Tarehe 05/9/2019
Sahihi ya Hakimu

1154324O2


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MAN UTD YAWEKA REKODI YA MAPATO




**LONDON,** England

MAPATO ya Klabu ya Manchester United yameongezeka kwa rekodi mpya ya kiwango cha pauni milioni 627 kwa mwaka kufikia Julai mwaka huu.

Hii ni licha ya klabu hiyo kukabiliwa na msimu mgumu wa 2018-19 uliochangia kuondoka kwa kocha Jose Mourinho na timu hiyo kumaliza msimu ikiwa katika nafasi ya sita.

Mapato yanayotokana na matangazo ya biashara yaliimarika kwa asilimia 18, kutokana na mkataba mpya wa Uefa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku mauzo ya kibiashara yakisalia kama yalivyokuwa.

Lakini timu hiyo inatarajia mapato na faida kushuka katika msimu wa 2019-20 baada ya kushindwa kufuzu katika Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Klabu hiyo kwa sasa ni ya nane katika Ligi Kuu ya England baada ya kuanza msimu kwa mchezo wa kiwango cha chini. Imeachwa nyuma ya Liverpool kwa pointi 10 na pointi tano nyuma ya mahasimu wa mji mmoja na mabingwa watetezi, Manchester City.

Kuna hatari kwa klabu hiyo kuishia nyuma ya wapinzani wake wa miaka mingi Ulaya kuipata haki ya kutambulika kuwa klabu tajiri duniani.

Wiki iliyopita mabingwa wa Uhispania, Barcelona walitangaza wanatarajia kupitisha kiwango cha mapato ya thamani ya pauni milioni 883 kwa mara ya kwanza msimu huu.

Licha ya kuongezeka kwa mapato hayo, Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward amesema klabu hiyo inathamini ufanisi wa mchezo uwanjani kwa kiwango cha juu.

Alisema: "Tunaendelea kuuangalia mpango wetu wa kujijenga upya na kuendelea kuimarisha mfumo wetu wa vijana, kwa mujibu wa falsafa ya klabu na kocha.

# Uefa yatangaza viwanja vya fainali

**LYON,** Ufaransa

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka vya Ulaya (Uefa), limetangaza viwanja vitakavyotumika kuwa mwenyeji wa michezo kadhaa ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu kadhaa ikiwamo msimu wa 2020/2021.

Uefa wametangaza viwanja mwenyeji wa fainali tatu zijazo za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo msimu wa 2019/2020 mchezo wa fainali utachezwa Ataturk Olimpiyat Stadı nchini Uturuki katika mji wa Istanbul.

Huku fainali ya msimu unaofuatia wa 2020/2021 mchezo huo utachezwa katika Uwanja wa St Petersburg nchini Urusi.

Hayo yametangazwa katika mkutano wa Kamati ya Uefa uliyofanyika nchini Slovenia juzi, huku ikitajwa kuwa maamuzi hayo yameangalia vitu vingi ikiwamo hoteli, miundombinu kwa maana ya ufikaji wa mashabiki kirahisi.

Mwaka 2022, fainali itachezwa kwenye Uwanja wa Allianz Arena nchini Ujerumani na mwaka 2023 utachezwa Wembley jijini London nchini England.







# *Infantino aigeukia Italia ubaguzi*

**MILAN,** Italia

RAIS wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Gianni Infantino amesema Shirikisho Soka la Italia, linatakiwa kuwachukulia hatua kali mashabiki wanaojihusisha na matendo ya ubaguzi wa rangi kama wanayofanya kule Uingereza.

Katika mchezo wa Jumapili kati ya Atalanta na Fiorentina, uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2, ulikuwa na viashiria vya kibaguzi, ikiwa ni mwendelezo wa aina hiyo ya matukio kwenye soka la Italia.

"Hauwezi kuwa na ubaguzi wa rangi katika jamii au katika mpira wa miguu," alisema Infantino. "Huko Italia, hali haijabadilika."

Katika mchezo wa Jumamosi wa Ligi Kuu Italia Serie A, mchezaji wa Fiorentina na timu ya Taifa ya Brazil, Dalbert alimweleza mwamuzi kuwa yeye ndiye aliyelengwa kwa nyimbo za kibaguzi, mchezo huo, ulisimamishwa kwa muda.

Tamko la wazi lilipotolewa juu ya tukio hilo kupitia spika kubwa zilizosikika uwanjani hapo, wimbo huo, haukusikika tena na mchezo ukaendelea.

Wiki iliyopita, mashabiki wa Cagliari walishutumiwa kumfanyia ubaguzi wa rangi, mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Romelu Lukaku anayeichezea Inter Milan.

Hiyo ilikuwa ni mara ya tatu kwa Cagliari kutuhumiwa mashabiki wake kuwa na vitendo vichafu vya ubaguzi wa rangi katika miaka miwili iliyopita.

"Ubaguzi unachanganywa na elimu, ulaaniwe," akaongeza Infantino. "Tunatakiwa kuwabaini wale wanaofanya vitendo hivyo na kuwatupa nje ya uwanja. Kama ilivyo nchini England, uhakikisho wa adhabu. Hauwezi kuogopa kulaani wabaguzi, tunahitaji kupigana nao hadi watakapoacha."

# VALVERDE: DUNIA INASIMAMA KITU KIBAYA KIKIMTOKEA MESSI




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, amesema kwamba, dunia inasimama kama kitu kibaya kinamtokea Lionel Messi wakati akizungumzia kuhusu hofu ya majeraha yake.

Messi alitolewa nje kipindi cha pili wakati Barca ikiibuka na ushindi uliohitajika zaidi wa mabao 2-1 dhidi ya Villarreal kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, juzi Jumanne usiku kutokana na kuonekana kuumia.

Nahodha huyo wa Barca alikuwa akianza katika mchezo wake wa kwanza msimu huu baada ya kutoka kuumia kigimbi cha mguu na Valverde alisema ilikuwa hatari kuendelea kumchezesha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

"Wakati kitu kibaya kinamtokeo Messi dunia inasimama, sio hapa tu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sidhani kama ameumia kwa kiwango kikubwa. Tunatakiwa kuchukua tahadhari. Tutaona kesho (jana Jumatano), siwezi kuzungumza chochote kwa sasa.

"Alikuwa ameumia kwa muda mrefu na hatutaki kuwa kwenye hatari yoyote kwa sasa."

Antoine Griezmann na Arthur kila mmoja alifunga bao kuiwezesha Barca kupata ushindi huo, na kutuliza presha kwa kocha Valverde baada ya kuanza vibaya msimu.

Valverde pia alizungumzia umuhimu wa matokeo hayo baada ya timu yake kupata kipigo cha kushtukiza kutoka kwa Granada Jumamosi.

"Kuna wakati unapata kitu sahihi na kuna wakati unapata kitu kisichosahihi. Ushindi huu ulikuwa muhimu zaidi kwetu," alisema.

## Sarri ataka Juve kuimarisha ulinzi



**TURIN,** Italia

MAURIZO Sarri amebainisha kwamba, Juventus lazima iimarike kwenye safu yake ya ulinzi licha ya mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kupanda kileleni mwa msimamo baada ya ushindi dhidi ya Brescia.

Juve ilitoka nyuma na kushinda mabao 2-1 dhidi ya Brescia iliyopanda daraja Jumanne na kupanda kileleni dhidi ya wapinzani wao Inter, ambao wamecheza mechi chache.

Alfredo Donnarumma alianza kuwafungia Brescia kabla ya Jhon Chancellor kujifunga na Miralem Pjanic aliyetokea benchi alifunga la ushindi kwenye mchezo huo ambao Mario Balotelli alianza dhidi ya Juve.

Juve ilipata ushindi huo bila ya mshambuliaji wake, Cristiano Ronaldo, ambaye aliachwa kwa hofu ya kuwa majeruhi.

Pamoja na ushindi huo, Sarri ambaye ni kocha wa zamani wa Chelsea alisema kwamba safu yake ya ulinzi haikucheza vizuri na inatakiwa kuimarika zaidi.

"Tumeimarika kwenye kupiga pasi katika mfumo wetu wa 4-3-1-2 tuliocheza," alisema Sarri akiiambia DAZN.

"Niliona kama kuna hatua zaidi zimechukuliwa na tulitengeneza nafasi nzuri za kufunga.

## *Mauricio Pochettino haelewi kinachoendelea Spurs*

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino anahisi kwamba Tottenham kutokuwa na kikosi kilichotulia kumechangia kuanza vibaya kwa msimu mpya wa 2019-20.

Spurs ilitolewa kwenye michuano ya Kombe la EFL juzi Jumanne kwa penalti 4-3 na timu ya Daraja la Pili, Colchester United.

Hawajashinda mchezo wa ugenini kwenye Ligi Kuu tangu Januari na wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi, wakiwa pointi sawa na Burnley na Sheffield United, baada ya kufungwa mabao 2-1 na Leicester City wikendi iliyopita.

Spurs pia walitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Olympiacos kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi huu, na hivyo kumfanya Pochettino kuendelea kuwa na wakati mgumu.

Kiungo nyota, Christian Eriksen mkataba wake unamalizika 2020 na mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark, alikosa penalti yake kwenye mchezo huo.

Mabeki, Jan Vertonghen na Toby Alderweireld pia wapo kwenye mwaka wao mwisho wakati Spurs na Pochettino anaona kutojulikana kwa majaliwa ya wachezaji wake kwenye kikosi hicho kunaathiri matokeo.

Alipoulizwa kwa nini Spurs wapo kwenye wakati mgumu, aliwaambia waandishi wa habari: "Nafikiri tulizungumza mno kuhusu uhamisho wakati wa kipindi cha maandalizi ya msimu mpya.

"Tuna uzoefu na soka na ni muhimu kujua kwamba uvumi uliotawala wakati wa kipindi cha maandalizi msimu mpya kuhusu uhamisho wa wachezaji, umeathiri kwa kiwango kikubwa kikosi chetu."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# EMERY: BELLERIN KWA MAN UNITED BADO

●●● Nadhani hapana, hawezi kuwa tayari kuanza Old Trafford, labda ndani ya mawazo yake ndiyo...

**LONDON,** England

UNAI Emery haamini kwamba Hector Bellerin atakuwa tayari kuanza kikosi cha kwanza wakati Arsenal ikiiva Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England, licha ya kucheza kwa mafanikio makubwa juzi, Jumanne.

**Bellerin, amekuwa nje ya kikosi tangu Januari kutokana na kukabiliwa na majeraha ya goti, lakini juzi alihitimisha kukaa nje baada ya kutokea benchi wakati Arsenal ikishinda mabao 5-0 kwenye mechi ya Kombe la Ligi (EFL Cup) dhidi ya Nottingham Forest.**

Beki huyo wa kulia raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 24, aliingia dakika ya 77 kuchukua nafasi ya Kieran Tierney aliyeichezea Arsenal kwa mara ya kwanza, na kusaidia kupatikana kwa bao la tatu lililotiwa nyavuni na Joe Willock.

Bellerin alikuwa mchezaji muhimu katika kikosi cha kwanza cha Arsenal kabla ya kuwa majeruhi, lakini kocha mkuu Emery hatarajii beki huyo wa kulia kuharakishwa kuanza katika safari ya kuifuata United Uwanja wa Old Trafford Jumatatu.

Alipoulizwa kuhusu Bellerin katika mkutano na wanahabari, Emery aliwaambia waandishi wa habari: "Alitaka kucheza kwa dakika 90. Alisema yupo tayari na alitaka kucheza.

"Nadhani hapana [hawezi kuwa tayari kuanza dhidi ya Manchester United]. Labda ndani ya mawazo yake ndiyo. Tunahitaji kumsikiliza daktari.

"Dakika za kwanza zilikuwa zakushangaza kwake... Kitu cha muhimu zaidi ni mtazamo wake. Anataka kutusaidia."

Rob Holding aliweka alama ya kurejea kwake akitokea kuuguza majeraha ya goti yaliyomweka nje ya uwanja kwa takriban miezi 10 kwa kufunga bao la kichwa ambalo liliiweka Arsenal kuwa mbele kwa mabao 2-0.

"Ni sahihi kuwa na mbadala katika nafasi ya beki wa kati. Hamasa yake, dakika zake nzuri. Kila siku katika mazoezi anatusaidia kuwa na kiwango zaidi kama timu," Emery alisema kuhusu Holding.

"Alihitaji kupata dakika na kujiamini. Ilikuwa ni mechi sahihi. Alichoka kidogo mwishoni, alikuwa na furaha."

Gabriel Martinelli alifungua akaunti yake ya mabao kwenye mechi yake ya kwanza katika klabu hiyo.

"Tulisubiri na kumtazama [Martinelli], namna gani anaweza kujizatiti akiwa nasi," aliongeza Emery. "Alicheza vizuri sana wakati wa maandalizi ya msimu mpya akifanya vizuri katika mazoezi kwa kujitoa na kiwango.

"Nilizungumza naye na kumtaka kuwa na subira kwa nafasi yake ya kufanya kama vile alikuwa akifanya. Usiku wa leo [juzi] amelifanya hilo. Alistahili hilo.

"Yeye ni mnyenyekevu sana, anapigana, ana njaa ya kupata nafasi hiyo ya kutusaidia."

## ZISIKUPITE

### MANDZUKIC AWINDWA UNITED

MANCHESTER United itamuwinda mshambuliaji wa Juventus, Mcroatia Mario Mandzukic, 33, na straika wa Barcelona, Mfaransa Ousmane Dembele, 22, katika dirisha la Januari. ***(Independent)***

### GERRARD KUMRITHI KLOPP

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kocha Rangers na nahodha wa zamani wa 'Wekundu' hao, Steven Gerrard ni mtu sahihi wa kumrithi wakati atakapoamua kuondoka hapo Anfield. ***(Four Four Two)***

### CARROLL HADI KRISMASI

BENCHI la utabibu la Newcastle United, linahofia mshambuliaji Muingereza Andy Carroll, 30, hatakuwa fiti vya kutosha kuanza mechi hadi Krismasi wakati huu akiendelea kujiweka fiti kurejea akitokea kuuguza majeraha ya kifundo cha mguu. ***(Telegraph)***

### BECKHAM KUMBEBA SOLARI

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Santiago Solari yupo katika mazungumzo ya kuwa kocha wa kwanza kuinoa timu ya David Beckham, Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MSL. ***(The Athletic)***

### ZAHA KUSEPA ZAKE JANUARI

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26, bado anahitaji kuondoka Crystal Palace na atalazimisha kuondoka Januari. ***(Calciomercato)***

### POGBA KUISHIKA PABAYA UTD

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 26, ataitaka klabu hiyo kumlipa mara mbili ya mshahara wake wa sasa wakati huu akitaka kujaribu kulazimisha kuondokana kwenda kujiunga na Real Madrid. ***(Express)***

### SEVILLA KUMWACHIA LOPES

SEVILLA ipo tayari kumruhusu kiungo Mreno Rony Lopes kuondoka katika dirisha la usajili la Januari, na Newcastle inamfuatilia mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City. ***(Gol Digital - in Spanish)***

### POCHETTINO SOKONI JANUARI

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino amefunguka kuhusu kuwa bize sokoni katika dirisha la Januari baada ya kikosi chake kung'olewa kwenye Kombe la Ligi na timu ya Daraja la Pili, Colchester. ***(Express)***

### ARSENAL MDOGOMDOGO

MKURUGENZI Mtendaji wa Arsenal, Vinai Venkatesham, amesema hakuna uwezekano wa klabu hiyo kuwa bize sokoni Januari baada ya usajili mkubwa waliofanya majira ya joto. ***(Standard)***

### KLOPP AMZUIA BREWSTER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amemwambia mshambuliaji kinda Rhian Brewster, 19, asiende kucheza nje kwa mkopo msimu huu, na nyota huyo wa kimataifa wa England U-21 jana alikuwa akijiandaa kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya MK Dons kwenye mechi ya Kombe la Ligi (Carabao Cup). ***(Four Four Two)***

### UNITED YAMFUATA TONALI

MANCHESTER United imetuma mashushu kwenda kumtazama kiungo kinda wa Italia U-21, Sandro Tonali akiichezea Brescia dhidi ya Juventus juzi. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## DStv yaja na chaneli ya Pop Up ya ZIFF

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni miezi michache baada ya kufanyika kwa tamasha kubwa la filamu Zanzibar (ZIFF), DStv imetangaza kufungua chaneli maalum (pop-up Channel) kwa muda wa siku mbili ili kuweza kuonyesha filamu mbalimbali zilizofanya vizuri katika tamasha hilo.

Filamu hizo ni kutoka katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Tanzania, Kenya, Afrika Kusini, Marekani, Iran, Morocco, Nigeria, Cape Verde na Zimbabwe huku chaneli hiyo ikiwa ni DStv 197 na itakuwa wazi kwa siku mbili Jumapili wiki hii na Jumatatu ijayo kuanzia saa 12 jioni hadi saa 4:30 usiku.

Miongoni mwa filamu zitakazoonyeshwa ni pamoja na filamu maarufu ya SEMA ambayo imewahusisha waigizaji na wachekeshaji maarufu nchini, Timamu (Mr. Beneficial, Mjeshi, Ebitoke, Onestory Kweka) ambayo inatarajiwa kuwa kivutio kikubwa kutokana na ubora wake na umaarufu wa waigizaji hao.

Akizungumzia uamuzi wa DStv kufungua chaneli maalum kuonyesha filamu hizo, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema kuwa unalenga kulitangaza zaidi tamasha la ZIFF pamoja na kuwapa watu ambao hawakuweza kuhudhuria tamasha hilo fursa ya kuona filamu mbalimbali zilizoonyeshwa.

"Hii ni fursa kwa watu kuona yaliyojiri ZIFF na tunafurahi kuwa mbali na kwamba kulikuwa na filamu kutoka mataifa mbalimbali ulimwenguni, filamu zetu za Tanzania pia zilifanya vizuri kwenye tamasha hilo.

Naye mwigizaji wa filamu ya SEMA, Brian Mrikaria maarufu kama 'Mr. Beneficial' alisema kuonyeshwa kwa filamu yao katika chaneli hiyo maalum ya DStv ni kitu cha kujivunia kwani pia itasaidia kuonyesha kuwa Tanzania tuna vipaji na tunaweza kufanya vitu vyenye viwango vya kimataifa.

## Tatu wanawake zakwama kusajili

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku nne kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, mabingwa watetezi wa ligi hiyo, JKT Queens wametajwa kuwa ni moja ya timu tatu ambazo hazijakamilisha mchakato huo, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alizitaja timu nyingine ambazo hazijawasilisha usajili wake kuwa ni pamoja na Baobab Queens ya Dodoma na Panama FC ya mkoani Iringa.

Ndimbo alisema kuwa shirikisho linawakumbusha viongozi wa klabu hizo, kuhakikisha wanakamilisha mchakato huo mapema na hakutakuwa na muda wa nyongeza kwa ambaye atashindwa kusajili kwa wakati.

Alisema wanazitaka pia klabu zote zinazotarajiwa kushiriki ligi hiyo, kuendelea na maandalizi ya msimu mpya, kwa sababu ligi hiyo ndio inayotoa idadi kubwa ya wachezaji wanaoichezea Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars).

# TANZANIA U-20, KARUME BOYS KUKINUKISHA LEO

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ya Tanzania Bara inatarajia kukutana na "ndugu" zao wa Zanzibar (Karume Boys), katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jinja, Uganda.

**Mechi hiyo ya mwisho ya hatua ya makundi ni ya kukamilisha ratiba kwa Tanzania Bara ambao wana point i nne sawa na Kenya, wameshafuzu hatua ya robo fainali wakati Zanzibar nayo inahitaji ushin-di ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.**

Kocha Mkuu wa timu hiyo ya U-20 ya Tanzania Bara, Zuberi Katwila, alisema jana kwamba mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu, kutokana na wachezaji wa timu hizo mbili kufahamiana vema.

Katwila alisema kuwa amewaandaa wachezaji wake kupambana na kuhakikisha wanapata matokeo mazuri huku pia akitoa nafasi kwa nyota wote kuonyesha uwezo wao.

"Kihistoria tunapokutana Bara na Zanzibar, huwa ni mechi ngumu, tumejiandaa na tunatarajia kukutana na ushindani, nimewaandaa wachezaji wangu kuongeza umakini katika mchezo huo ili tuweze kupata matokeo mazuri," alisema Katwila.

Naye Kocha Mkuu wa Karume Boys, Nassor Salum, aliliambia gazeti hili kuwa vijana wake wako tayari kuwakabili Tanzania Bara na anaamini watapata ushindi katika mchezo huo wa leo.

"Tumeshawaona wapinzani wetu wanavyocheza katika mechi zao mbili za kwanza, tutapambana kuhakikisha tunatumia mapungufu yao ili kupata ushindi, malengo yetu ni kusonga mbele katika mashindano haya na kubwa ni kuchukua ubingwa," Salum alisema.

Karume Boys yenyewe ina pointi tatu baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi yake ya pili dhidi ya Ethiopia ambao wanaburuza mkia katika kundi hilo.

Mechi nyingine za mwisho za hatua ya makundi katika mashindano zitakazochezwa leo ni kati ya Kenya dhidi ya Ethiopia, wakati Sudan Kusini wataikaribisha Somalia.



Kutoka kushoto ni Mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Abdallah Ahmed, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas akifuatiwa na Mkuu wa Huduma za Kidigitali Tigo Tanzania, Ikunda Ngowi, wakati wa kuwasiliana na washindi wa simu wa Promosheni ya Faidika na Jero. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Washindi Faidika na Jero wa Tigo, SportPesa hawa*

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI watano wa Promosheni ya Faidika na Jero inayoendeleshwa na Kampuni ya Tigo Tanzania na SportPesa Tanzania wametangazwa jana jijini Dar es Salaam.

Promosheni hiyo ilizinduliwa wiki iliyopita ambayo inawahusisha wateja wa TigoPesa pekee wanapocheza na SportPesa, ambapo mshindi wa kwanza aliyetangazwa jana ni Franky Victor Kimambo kutoka Kimara Temboni jijini Dar es Salaam aliyejishindia simu ya smartphone.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema hiyo ndiyo droo yao ya kwanza kuchezeshwa tangu promosheni hiyo ilipozinduliwa na kwamba kila wiki wataendelea kutoa washindi saba watakaocheza na kambuni hiyo.

Aliongeza kuwa simu hizo smartphone zitatolewa kwa washindi wadogowadogo kabla ya siku ya mwisho ambapo gari mpya aina ya Renault Kwid litakabidhiwa kwa mshindi mwishoni mwa mwezi ujao, huku akifafanua kuwa unaweza kubashiri kwa kuanzia na kiasi cha shilingi 500 tu.

"Nawapongeza sana washindi wa smartphone wiki hii ambao ni ndugu Frank Kimambo, Raphael Mwangila, Seif Mkumba, Baraka Sanga na Ally Ally."

Kwa upande wa Ikunda Ngowi, Mkuu wa Kitengo cha Huduma ya Kidigitali Tigo Tanzania, alisema: "Ni muda muafaka kwa Watanzania kufanikiwa kwa kupata ushindi wa gari jipya lenye kilomita sifuri na simu za smartphone ambazo hizo zitatolewa kwa washindi watano watakaopatikana kwa kila wiki.

"Kwa jero unapata gari na simu hizo kwa kupitia promosheni hii inayoendelea ya Faidika na Jero ambayo inawahusisha wateja wa tigo watakaobashiri kupitia TigoPesa," alisema Ngowi.

Michezo
Alhamisi Septemba 26, 2019
Nipashe



Emery: Bellerin kwa Man Utd bado UKURASA 30

AKAUNTI...



Mshambuliaji wa Arsenal, Mbrazil Gabriel Martinelli (kushoto), akifungua akaunti yake kwa timu hiyo kwa kutupia bao la kwanza katika ushindi wa mabao 5-0 walioupata kwenye mechi ya Kombe la Ligi (EFL Cup) dhidi ya Nottingham Forest iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi na straika huyo kucheka na nyavu mara mbili, huo ukiwa ni mchezo wa kwanza kwake kuichezea Gunners. **HABARI UK. 30**

## Yanga yawasili uwanja wa vita

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga, wametua 'uwanja wa vita' (mji watakacheza mechi yao) katika mji wa Ndola, Zambia ili kuendelea na "mawindo" yake ya kuwavaa Zesco FC, imeelezwa.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, aliliambia gazeti hili jana kuwa kikosi cha timu hiyo tayari kimeshafika Ndola na maandalizi kuelekea mchezo huo wa marudiano utakaochezwa keshokutwa yanaendelea vizuri.

Mwakalebela, Katibu Mkuu wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), alisema uongozi wa klabu hiyo unafurahi kuona morali ya kila mchezaji iko juu na kinachosubiriwa ni muda wa mchezo kufika.

"Tuliweka kambi fupi Lusaka na leo (jana), muda wowote kuanzia sasa tutaanza safari ya kuelekea Ndola, tunamshukuru Mungu mambo yanakwenda vizuri, tunaahidi tutapambana ili kupata ushindi Jumamosi, tunataka kuendeleza rekodi yetu katika mashindano ya kimataifa," Mwakalebela alisema kabla ya kuwasili Ndola.

Yanga itashuka uwanjani Jumamosi ikiwa na kumbukumbu ya sare ya bao 1-1, waliyoipata Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Mshindi wa mchezo huo, atatinga katika hatua ya makundi na timu itakayopoteza itaangukia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kucheza mechi ya mtoano nyumbani na ugenini kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya shirikisho.

# Maxime: Simba hii ni zaidi ya Stars

**Na Somoe Ng'itu**

### Afafanua si mechi nyepesi, lakini Brigedia Jenerali Gaguti asema hawatachomoka, huku...

NI zaidi ya mechi! Wakati Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti akieleza anatarajia kukiongoza kikosi cha Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa watetezi, Simba utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba ili kupata ushindi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mecky Maxime ameonya kwa kueleza wanakutana na timu bora Afrika ambayo ina ubora kuliko timu ya taifa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Gaguti, alisema anataka kuona Kagera Sugar inashinda katika mechi hiyo ya leo na michezo mingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye ardhi ya mkoa huo.**

Kiongozi huyo alisema kuwa amepanga kuongoza kampeni hiyo ya kuhakikisha Kagera Sugar inapata ushindi katika mechi zote za nyumbani, ili malengo ya kutwaa ubingwa wa msimu huu yatimie.

"Nataka ubingwa wa msimu huu ubaki Kagera, tunaanzia na mchezo wetu wa Alhamisi (leo), mikoa yote 26 isikie, mtu yeyote anayekanyaga Kagera, lazima aondoke na kichapo, lazima wajue hivyo, ikiwezekana wasije kabisa, walipe faini kabisa, sisi tubaki na pointi tatu," alisema Gaguti.

Lakini Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Maxime, alisema si mechi rahisi na anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na ubora wa kikosi cha Simba.

Maxime alisema kuwa, inahitajika utulivu na umakini unapocheza na mabingwa hao watetezi, kwa sababu wana wachezaji wenye uzoefu na wanaozidi baadhi ya timu za Taifa mbalimbali.

"Simba ni timu bora Afrika, na inazidi baadhi ya timu za taifa, ina wachezaji wengi wazoefu, hivyo hautakuwa mchezo mrahisi pamoja na kwamba tumejipanga vizuri," alisema Maxime.

Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji Patrick Aussems alisema amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mechi za msimu uliopita na kuingia uwanjani leo wakiwaza ushindi tu.

"Matokeo ya msimu uliopita yawe hamasa ya kufanya vizuri katika mechi ya kesho (leo), tumejiandaa kupambana ili kupata ushindi na tunatakiwa kuwaonyesha kwamba sisi ni Simba," alisema kocha huyo.

Mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere ambaye ana mabao matatu na Miraji Athumani, wanatarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo yenye pointi sita huku Kagera Sugar yenye pointi tisa na wamecheza mchezo mmoja zaidi, wakiwa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo.

Simba ilitua mapema jana mkoani Kagera kwa Ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania na jana jioni ilifanya mazoezi mepesi katika Uwanja wa Kaitaba tayari kwa mechi hiyo ya leo.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo, ni katika Uwanja wa CCM Samora mkoani Iringa, ikiwakutanisha wenyeji Lipuli FC dhidi ya Mbeya City kutoka jijini Mbeya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >